MJADALA WA MWEZI KENGEJA – PEMBA 19/3/1995

- **RISALA ZA MKUU WA WILAYA NA KADHI WA WILAYA YA MKOANI**
- **KHUTBA YA AFISA TAWALA WA WILAYA**

Assalaam Alaykum Warahmatullah wabarakat-hu.

Ndugu waislamu. Kwa niaba ya mkuu wa wilaya, nimesimama hapa kuzungumza machache kuhusiana na mkusanyiko wetu huu.

Kwa bahati mbaya mkuu wa wilaya mwenyewe amedharurika na huu ujumbe itabidi uwafike, kwa niaba yake nimesimama hapa kuufikisha ujumbe huo.

Tulikuwa na mambo matatu muhimu. Moja limeelezwa kwenye kanda, yaani historia ya mkushanyiko huu.

Kwa kifupi kabisa nitairudia. Ni kwamba mnamo mwezi Shaaban, baada ya watu wa Kengeja wapatao 40 kwa mujibu wa barua na orodha yao walimuandikia barua bwana kadhi wa wilaya ya Mkoani, kutaka kutatua matatizo yao, kama yalivyokwisha kuelezwa. kabla;yaani kufunga swala kifuani, kufunga Ramadhani kabla. kufuturu kabla na mengineyo.

Bwana kadhi alichukua hatua za kuja Kengeja na kukutana na pande zote mbili. Upande mmoja ukaomba kongamano au mkusanyiko kama huu. Bwana kadhi akakubali.Baada ya kukubali akaja wilayani, kwa serikali ya wilaya. Akatuomba tushirikiane naye katika kuandaa shughuli hii.

Kwa sababu shughuli hii twategemea itatatua matatizo mengi yaliyopo. Na pengine itazuia mengine ambayo hayajajitokeza ;ofisi ya mkuu wa wilaya ilikubali kushirikiana naye kuandaa mkutano huu.

Kwa hivyo ofisi ya mkuu wa wilaya imeshiriki kuandaa mkutano huu kwa ombi la bwana kadhi. Lengo kama lilivyoelezwa ni kutatua matatizo yaliyokwisha jitokeza na wala si kutanua matatizo. Lengo ni kuyamaliza.

La pili, ni ombi kwa sote tuliokusanyika hapa. Kwa wasikilizaji,huu ni mkutano wa dini ya kiislamu.Hakuna sababu ya kupiga makofi hata kama utafurahi.Pia hakuna sababu ya kuzomea hata kama utakasirika kiasi gani. Mambo haya yanaweza yakaleta fujo. Hatimae yakaja matokeo ambayo hatukuyatarajia .

Hakuna sababu ya kupiga kofi, hakuna sababu ya kuzomea, wala sababu ya kuonesha ushabiki wa aina yoyote ambao utamuathiri mwengine.

Kwa upande wa masheikh na pande zote mbili,naamini kwamba adui yetu Iblisi katika mikutano kama hii wala hatumi mtoto.Huhudhuria yeye mwenyewe, na pengine huchukua askari wake wote, wale anaohisi watamsaidia kuvuruga mikutano kama hii.

Kwa hivyo tunawaomba masheikh wa pande zote mbili tusaidiane katika kumdhibiti Iblisi.Tusaidiane asije akatugeuza kutoka kwenye lengo tulilolikusudia.

Namalizia kwa kusema kuwa,uhai wa mkutano wetu huu, utatokana na amani na utulivu tutakaousababisha sisi wenyewe tuliopo hapa. Pindipo tukiona amani na utulivu vinaharibika tutamchukulia hatua yoyote atakayesababisah vurugu hilo.

Tutamchukulia hatua hizo kwa ajili ya usalama wa wengine,haidhuru hata kama baadae atalalamika.

Kwa hayo machache naomba kumkabidhi ukumbi mheshimiwa kadhi wa wilaya ya Mkoani, kwa sababu yeye ndiye mwenyekiti wa mkutano huu, ili aendelee kwa misingi na taratibu za kidini kama ilivyokusudiwa.
Ahsanteni.

MHESHIMIWA KADHI WA WILAYA YA MKOANI

Akaanza na dua ya ufunguzi halafu akaendelea:-

Kwanza natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu subhaanahu wa taala aliyekupeni uwezo na nguvu za imani ya Uislamu kuja katika uwanja huu kusikiliza na wengine kutoa hoja ili dini yetu ya uislamu iendelee bila kupigwa vita na hao maadui wa kiislamu.Na inshaAllah Mwenyezi Mungu atatupa tawfiq.

Jambo la pili!. Nimetoa kanda; rekodi yake, ili kila mmoja afahamu wazi, nini sababu ya kukushanyika hapa, na nani ambaye aliuomba mkushanyiko huu, na ni nani ambaye aliyekubali ombi lake mpaka tukafika hali hii.

Nataraji kwamba tutaendelea na kongamano; mkutano huu kwa usalama na utulivu mpaka tufikilie mahala ambapo kila mmoja ajijue kuwa afanyavyo ndivyo au sivyo.

Baada ya kumalizika kongamano hili sitosema lolote kuhusu kongamano hili, bali nitachukua fursa Ijumaa ijayo kama nilivyofanya mara ya mwanzo, kuja kuelezea maendeleo ya kongamano lote, pamoja na kuelezea namna gani tutaweza kushauriana na kuendela kuishi kwa usalama katika uislamu, huyu bila kumbughudhi yule.

Rasmi natangaza kuwa kongamano liko wazi.*Wassalaam alaykum warahmatullaah wabarakathu.*
Baada ya kongamano kufunguliwa rasmi kwa risala za mkuu wa wilaya na kadhi wa wilaya ya Mkoani, akapewa nafasi mzungumzaji aliyekuwa na hoja za Ansaar Sunna kuhusu mwezi. Akaanza:

SKH. YUSSUF HAMZA YUSSUF

Jina langu ni Yussuf Hamza Yussuf, niliyezaliwa katika kijiji hichi cha Kengeja.

Nimesoma katika madrasa (shule) hii ya Kengeja. Nikamaliza kwenye madrasa ya Tumekuja;Zanzibar, mwaka 1976.

Baadae nilijiunga na chuo kinachoitwa Alharamain; Dar –es-Salaam. Nikamaliza masomo yangu nikafanya mtihani. Nikajiunga na Chuo Kikuu cha Ummul Qurra; Makkatul Mukarrama.

Niliishi kwenye mji huo mtakatifu kwa muda wa miaka sita. Nikachukua shahada yangu na kurejea Zanzibar.

Nikapangiwa kufanya kazi kwenye chuo cha kiislamu mwaka 1989. Niliendelea kufundisha kwenye chuo hicho kwa muda wa miaka mitatu.

Baadae nikachukua uhamisho kurudi hapa nyumbani Kengeja, ambapo wizara ikanipangia kufanya kazi kwenye shule hii ya Kengeja.

Kwa vile nimekwenda kusoma na natakiwa katika Uislamu nitoe mchango wangu, nikaanzisha madrasa niliyoipa jina la Madrasatu Tarbyatul Islamiya; Chuo cha malezi ya kiislamu.Hiyo ilikuwa Tarehe 11/1/1992.Hiyo ndiyo historia yangu kwa ufupi tu.

Ikhwatul Ikram] Ndugu zangu watukufu. Kabla sijaanza utangulizi. Kadhia yetu ya kwanza ambayo tutaizungumza ni juu ya kulazimu watu fulani kufunga kwa kuonekana mwezi sehemu fulani. Jee wazanzibari wafunge kwa kuonekana mwezi Kenya au Uganda, au Sudani au Saudia.Au kwa kuonekana mwezi Misri, Malaysia. Indonesia na kadhalika.

Audhubillahi mina shaittaanir rajiim]. Najilinda kwa Mwenyezi Mungu na shetani aliyefukuzwa kutoka rehema ya Mwenyezi Mungu.
Bismillaahir Rahmaanir Rahiim]. Naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuwaneemesha waislamu na makafiri hapa duniani, na Mwenye kuneemesha waislamu tu yawmul Qiyaama.

Alhamdulillaah]. Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu. Rabil Aalamiina] Mlezi wa viumbe wote.Wabihii] Na kwake yeye Mwenyezi Mungu. Nastaiinuhu] Tunataka msaada wake atusaidie yetu. Wanastaghfiruhu] Na tunataka msamaha wake atusamehe makosa yetu.Wanauudhubillaah min shuruuri anfusinaa] Na tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu na shari za nafsi zetu.Wamin sayyiaati a'amalinaa] Na ubaya wa matendo yetu tunayo yafanya siku zote.
Man yahdihi Llaah] Mwenye kuongozwa na Mwenyezi Mungu katika njia ya sawa. Falaa mudhwila Llaah] Hapana wa kumpoteza.Faman yudhw-lil] Na mwenye kufuata upotevu mpaka akapotea. Falan tajida lahuu waliyan murshidan] Hatapata kabisa wa kumuongoza katika njia ya sawa.
Wa ash-hadu] Na nathibitisha.An- lailaaha illa Llaaha] Kwamba hapana Mola anayepasa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu. Wahdahu] peke yake. Laa shariika – lah] Hana mwenzi Mwenyezi Mungu subhaanahu wa taala .

Wa ash- hadu] Na Nathibitisha. An-na Muhaamadan] Hakika ya Muhammad. Abduh] Ni mja wake. Wa rasuuluhu] Na ni mjumbe wake. Alladhiy] Muhammad ambaye. Ad-da L-amaanata] Ametekeleza amana alopewa.Wabalaghar- Risaalat] Na ameufikisha ujumbe alopewa kwetu ;wa uislamu. Wanassahal umma] Na amewabembeleza watu kuingia kwenye dini ya Mwenyezi Mungu.

Wa jaahada fiy sabiili Llaahi haqan jihaadih] Na akaipigania dini ya Mwenyezi Mungu upeo wa jihadi yake.Hataa ataahul yaqiin] Mpaka yakamfikia mauti. Wa huwa yaquul]

Naye Mtume Muhammad yuwasema. Allaahumma sh –had] Ewe Mwenyezi Mungu Shuhudia. Qad Balaghtu] Nimeufikisha ujumbe ulionipa.Na hakika, Mtume Muhammad swalla Llaahu alayhi wa ssallaam kaufikisha ujumbe kwetu.

Ndugu zangu waislamu maneno haya aliyasema Nabii Muhammad swalla Llaahu alayhi wa ssallaam kwenye kiwanja cha Arafat kwenye hijjatul Wadaa-i.

Baada ya maneno hayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliiteremsha aya isemayo;
{ LEO NIMEKUKAMILISHIENI DINI YENU, NA KUKUTIMIZIENI NEEMA YANGU, NA NIMEKUPENDELEENI UISLAMU UWE DINI YENU----- } QUR-5:3

Ilipoteremka aya hii, ndugu zangu waislamu sayyidna Omar Ibn Khattaab alifurahi sana, na sayyidna Abubakar Sidiq alilia sana.

Alifurahi sana sayyidna Omar kwa sababu dini ya Mwenyezi Mungu imeshakamilika. Na alilia sana Sayyidna Abubakari kwa sababu alihisi Mtume Muhammad swalla Llaahu alayhi wa ssallaam ndio anaiaga dunia.

Siku hiyo Mtume swalla Llaahu alayhi wa ssallaam aliuusia umma, akawaambia:
[TARAKTU FIY-KUM MAA LAN TADHWILUU ABADAN IN TAMAASIKUM BIHI. KITAABU-LLAAH WA SUNNATIY].***Nimewaachieni waislmu jambo ambalo mukishikamana nalo hamutapotea milele;kitabu cha mwenyezi mungu na sunna zangu.***

Skh Yussuf Hamza alipofika hapo, alihisi baadhi ya wasikilizaji walikuwa na haraka ya kusikia zaidi hoja zake,juu ya mwezi na wengine walianza kupoteza ustahamilivu. Ikabidi awatanabahishe.

Ndugu waislamu!, ningeomba musinishughulishe, kwa sababu muda upo, niwacheni nizungumze kwa utaratibu nilioupanga na ufasaha. Kwa sababu mimi leo ndiye mzungumzaji mkuu.Leo ni siku ya mtu kuyaeleza yale ambayo anayaitakidi yamo katika moyo wake, na yamo katika vitabu. Nastahiki nipewe muda wa kutosha na nisikilizwe. Tusiwe na haraka.

{ ENYI MLIOAMINI!, MTIINI MWENYEZI MUNGU NA MUMTII MTUME (SWALLA LLAAHU ALAYHI WA SSALLAAM) NA WALE WANAO KUTAWALIENI MAMBO YENU MIONGONI MWENU (NYINYI WAISLAMU).NA MUKITATIZANA KATIKA JAMBO (NYINYI WAISLAMU) LIRUDISHENI KWA MWENYEZI MUNGU NA MTUME (SWALLA LLAAHU ALAYHI WA SSALLAAM) IKIWA MUNAMUAMINI MWENYEZI MUNGU NA SIKU YA MWISHO. HAYO NDIYO BORA ZAIDI NA NDIYO YENYE MWISHO MWEMA } Qur'an – 4:59.

Qaala almufasir Ibnu Kathiir].Amesema mfasiri Ibnu Kathir. Wa haadhaa amrun minal-Laah] .Hii ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.Bi an-na kulla sha'iy].Kwamba kila kitu. Tanaz-za-a n- naas] watakachotatizana watu. Fiy] katika jambo hilo. Min

usuuli diin] Liko kwenye Qur'an na mafunzo ya Mtume wake swalla llaahu alayhi wa ssallaam . Wa qaala Taala] Na akasema Mtukufu Allah subhaanahu wa taala.

Laa!} Naapa kwa Mola wako Mlezi!. {HAWATAAMINI MPAKA WAKUFANYE WEWE NDIYE MUAMUZI KATIKA YALE WANAYOKHITILAFIANA;KISHA WASIONE UZITO KATIKA NYOYO ZAO JUU YA HUKUMU UTAYOTOA. NA WANYENYEKEE KABISA} . Qur'an – 4:65.

Wa qaala Ta-ala] Na akasema tena Mtukufu Allah subhaanahu wa taala :

{ HAIWI KWA MUUMINI MWANAMUME WALA MUUMINI MWANAMKE KUWA NA KHIYARI KATIKA JAMBO MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE WANAPOKATA SHAURI KATIKA JAMBO LAO. NA MWENYE KUMUASI MWENYEZI MUNGU NA MTUME WAKE BASI HAKIKA AMEPOTEA UPOTOFU ULIO WAZI} Qur'an – 33: 36.

Kwa hivyo ndugu waislamu, baada ya kufika hapo. Sasa tutulie kimya ili tuianze maudhui yetu.

Tutaanza kwa aya ya 185 ya Suratul Baqara inayosema: {MWEZI WA RAMADHANI AMBAO IMETEREMSHWA HUMO QUR'AN KUWA NI UWONGOFU KWA WATU, NA HOJA ZILIZO WAZI ZA UWONGOFU NA UPAMBANUZI. BASI ATAYEKUWA MJINI KATIKA MWEZI HUU NAAFUNGE. NA MWENYE KUWA MGONJWA AU SAFARINI BASI ATIMIZE HISABU KATIKA SIKU NYENGINE. MWENYEZI MUNGU ANAKUTAKIENI YALIYO MEPESI WALA HAKUTAKIENI YALIYO MAZITO, NA MTIMIZE HIYO HISABU, NA MUMTUKUZE MWENYEZI MUNGU KWA KUWA AMEKUONGOENI ILI MPATE KUSHUKURU}

Faman shahida min- kumush- shahra fal – yaswumh.Hicho ndicho kipande ambacho leo tutaanza kuongea nacho. Kwa nini?. Kwa sababu kuna tafsiri nyingi twazisikia. Na baadhi ya watu wasema **MWENYE KUUONA MWEZI BASI AFUNGE**.

Mimi nasema hiyo siyo tafsiri sahihi. Wala hakuna tafsiri hiyo katika taifa la Kiislamu. Kwamba faman shahida min- kumush- shahra fal yaswumh] Kwa maana atakayeuona mwezi afunge.Tafsiri hiyo hakuna.

Kwa bahati nzuri tu, tunazo tafsiri nyingi hapa. *Akanyoosha mkono kuonesha rundo kubwa la vitabu kwenye meza mbele yake; upande wao.*Atakayekuwa ana wasiwasi basi wapo watu wamekwisha zitayarisha watampatia ili asome.

Twaib!, Tutaitafsir faman – shahida neno kwa neno mpaka tupate maana yake.

Neno shahida katika lugha ya kiarabu halina maana moja.Kwa sababu wasema waarabu; Alkalimatu laisat lahaa ma'ana illa idhaa wudhiat bijumlat] Neno katika lugha ya kiarabu halina maana kamili mpaka uliweke katika ibara au sentensi ndio litadhihiri maana yake.

Kwa hivyo unaweza ukasema kwa lugha ya kiarabu. shahid-tuhu yaf'al kadhaa] Nimemuona ayanafan jambo fulani. shahid-tu muhammada ya'akulu twaama] Nimemuona Muhammadi anakula Chakula.

Lakini neno hilo hilo ukilitumia kwa mudhwaa ri''u, uksasema ash-hadu an-laa – ilaaha illa llaahu]; lageuka maana yake. Haiwi kuona tena. Inakuwa nathibitisha. Hapa inakuwa **Nathibitisha kuwa hapana mola anayepasa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu.**

Kadhalika Shahida ina maana ya haadhara. Na hii had-dhara ndiyo iliyotumika kwenye tafsiri zoote. Had-dhara siyo kuona.

Lakini muulizaji anaweza akaniuliza. Hivyo waweza kutupa dalili kuwa shahida yatumika kwa maanaya had-dhara mbali na kwenye tafsir? . Jawabu ni ndiyo !.

Nani atakayetupa dalili?. Ni kiongozi wetu Nabii Muhammad swalla llaahu alayhi wa ssallaam katika Hijjatul wadaaiy. Asema; Liyubaaligh shaahidu minkum L-ghaaib]. Liyubaaligh] Naafikishe.Ashaahidu ayyi haadhiru]Aliyepo. Minkum L-ghaaib] Kati yenu kwa asiyekuwepo.

Na ushahidi mwingine wa maneno yake Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam ni Laa taswumanna mraatun wa Baaluha Shaahidun] Na asifunge mwanamke na mumewe yupo. Funga gani? ;Ya sunna. Kwa sababu mumewe aweza akataka burudani. Akitaka yeye asema "Aah leo ni Jumatatu mie nafunga!. Ni mpaka apewe ruhusa na mumewe. Ndio maana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akasema Laa taswumanna] Na asifunge kabisa. Wa baaluha shaahidun.

Kipi tunachokitafuta? Ni Shaahidun kwa maana ya had-dhara.

Ndio tumeshaweka wazi kuwa shaahidu ina maana tatu; kuona, kuthibitisha na kuhudhuria. Hii kuhudhuria;had – dhara ndiyo aliyoikusudia Mwenyezi Mungu sub haanahu wa taala. katika tafsiri zote.

Kwa hivyo itakuwa Faman haad-dhara] kwa yule ambaye atakayekuwepo, yaani haad-dhirun, muqiimun fiy L-baladi.

Tafsiri hiyo ndugu zangu, itakuwa ishafahamika. Lakini twende mbele kidogo mpaka tuweze kuichanganyisha kwa maana sahihi.

Faman shahida min- kumush –shahra]. Sasa naja kwa neno shahara. Neno shahara ndugu zangu waislamu, kwa wale wanaolitafsiri kuwa ni mwezi.Basi si mwezi mwandamo alilokusudia Mwenyezi Mungu hapa.

Neno shahara kwa bahati nzuri Jalla Jalaaluhu katika Qur'an kalitumia mara 21.Mara zote hizo ni kwa maana ya siku 29 au 30; yaani mwezi.Wazungu waita *MONTH*!

Kwa hivyo Shahar maana yake ni mwezi; yale masiku. Sasa ukiniuliza; "Haya, ule mwezi mwandamo tuuite vipi? . Una majina yake kwa kiarabu. Ule; jina lake la kwanza ni hilaalu, muthana yake Hilaalani.,Jam'u yake ni Ahilla. Kwa kauli yake Mwenyezi Mungu, {YAS-' ALUUNAKA ANIL-'AHILLA--};QUR'AN – 2:189.

Ama, maana ya pili, ule mwezi unaitwa Qamarun. Kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu aliposema kwenye Suat Yaasin, { WAL-QAMARA QADDARNAAHU MANAAZILA HATAA 'AADA KAL-URJUUNIL-QADIIM} Qur'an - 36: 39
Maana nyengine ule mwezi waitwa Badrun, kwa dalili ya ile kaswida tunayoisoma siku za maulidi, Twalaal Badru alaa-inaa min thaniaat il Wadaa'i].

Hivyo mwezi ule, una majina matatu; Hilaalun, Qamarun na Badrun. Hayahusiani kabisa na shahar, ambalo maana yake ni masiku 29 au 30.

Sasa tuje pale Falyasumhu]. Wanaposema afunge. Sivyo!. Tafsiri siyo!.

Kwamba Fal yaswumhu] afunge. Sivyo!. Kwa sababu ingekuwa fal yaswumt-hu] afunge. Lakini mbele kuna nini? Kuna hee, na ni dhwamir.

Watu wa Nahau wasema Alhaaw dhwamirul muttaswilu mabni i u alaa dhwami fiy mahal-li nas'bi, maf'uulun bihii]; *AN OBJECT* wazungu waita.

Sasa kwa maana hiyo itakuwa vipi na imeshazidi jengo?. Waarabu wasema ziyaadatul mabnaa yadul-lu alaa ziyadatul ma'ana] Ukiliona neno limezidi jingo, na maana yake nayo hubadilika ikawa imezidi.

Kwa hivyo itakuwa vipi?. Falyaswumhu] na aufunge.Alhaaw ya'udu ilaa Shahri, Li anna dhwamira ya'udu ilaa aakharil makaani] kwa sababu dhwamiri inarudi pahali palipokuwa karibu. Kwa hivyo itakuwa na aufunge.

Mtazame Skh Abdallah Saleh Farsy alivyoifahamu na kuifasiri ibara hii. Itakuwa na maana hiyo hiyo tuliyoifasiri. Ayyi] Yaani; {NA ATAKAYEKUWA KATIKA HUO MJI NAUFUNGE--}
Halafu,Qur'an ndugu zangu waislamu haiwaachi watu hivi hivi, imejifasiri yenyewe. Tazama hapo mbele. Allah subhaanahu wa taala asemaje? ; WAMAN – KAANA MARIIDHWAN AW ALAA SAFARIN] Akiwa mmoja kati yenu ni mgonjwa. Au yuko safarini; hayupo katika mji. FA-'IDDATUM MIN 'AYYAA – MIN 'U-KHAR] Aje alipe katika siku nyengine,zile siku zilizobakia. Kwamba zilizokusudiwa kufungwa ni siku.

Kwa hivyo ni wazi kabisa kwamba atakayekuwepo katika nchi, ukamfikia ule mwezi wa Ramadhani na aufunge. Alhamdulilaah natumai imefahamika.

Siyo wale wasemao faman shahida min- kumush – shahra falyaswumh] Atakayeuona mwezi afunge. Hutaipata tafsir hiyo mpaka siku ya kiyama.

Tunaendelea!. Tumeshaipata aya hiyo, sasa hatujajua mwezi wathibiti vipi?. Huu mwezi wa Ramadhani utathibiti vipi?. Hiyo aya haijatupatia mwezi ati!.

Kazi hii ya kuthibiti mwezi tutamwachia Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam mwenyewe. Yeye ndiye atakayetwambia leo; Mwezi uthibit vipi?.

Kwanini tumwachie Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam? . Aah!, Twamwachia yeye kwa sababu Mwenyezi Mungu atwambia!: { KWA ISHARA WAZI NA VITABU. NASI TUMEKUTEREMSHIA WEWE UKUMBUSHO ILI UWABAINISHIE WATU YALIYOTEREMSHWA KWAO.WAPATE KUFIKIRI}- Qur'an ANNA HL; 16,44.

Kwa hivyo mbainishi wetu ni Nabii Muhammad swalla llaahu alayhi wa ssallaam. Ndiye atakayetwambia mwezi waandama vipi. Haya twambie Yaa Rasuulallaah!. Hupo lakini maneno yako yapo. Tumsikilize Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam. Mwenye vitabu kaa vizuri huko!.

Qaala Rasuulu Llaah swalla Llaahu alayhi wassallam] Amesema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake.
Faidhaa ra'aitum L-hilaala] Mutakapouona mwezi. Faswuumuu] Basi fungeni. Waidhaa ra'itumuuhu]Na mutakapouona, Fa'afttiruu] Basi fungueni, kuleni sikukuu. Muttafaqun Alayhi] Ni hadithi haina wasiwasi. Kaipokea Bukhari na imamu Muslim kwa itifaaq.

Kama alivyotutaka bwana kadhi katika barua yake, kuwa kila tutakalolisema tulitoleee dalili. Tumefurahi sana, Li an-na diinu daliilu yaa shaykhul mudhwam].

Hadithi hiyo iko katika KITAABUUL MAJMU'I, SHERH ALMUHADHAB LIL IMAAMIN NAWWAWIY, jz6, swafhat 269.Mwenye kitabu nambie, kitabu hiki kina umri .wa miaka mingapi?. Haraka haraka!, niwaambie wazee
Aliyepewa dhamana ya vitabu akajibu,kuwa kina umri wa miaka 739; skh Yussuf akaendelea:-
MAJMU'I ni kitabu cha mkuu wa madh-hebi ya Imamu Shaafiy, sote twamjua hapa. Akitajwa tu twamjua kuwa ndiye mkuu wa kishaafiy. Lakini ndio umethibiti mwezi?.

Waqaala swalla llaahu alayhi wa ssallaam] Na amesema mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake. "In shaahida shaadidaan-i"] Wakiuthibitisha mwezi mashahidi wawili. "Ayyi Muslimaani] waislamu, "faswuumuu"] basi fungeni, "waafttirruu"] na kuleni sikukuu. Rawaah Ahmad] ameipokea imamu Ahmad.

Anil Abdulrahmaani bin Zayd bin Khattaaabi, min kitaabi RAWDHWATIN NAADIYA, .sherh Durarul Bahiya. Juzuu ya 1 swafhat 328

Naleta na hadithi ya tatu ili tufahamu vizuri jinsi gani Mtume swalla llaahu alayhi wa .ssallaam anavyotuthibitishia namna mwezi unavyoandama
Waqaala swallallaahu alayhi wa sallalam].Na akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu .rehema na amani ziwe juu yake

Swuumuu liru'yatih"] Fungeni kwa kuonekana kwake, ukisema kwa kuuona shauri yako." Pia itabidi uweze kutupa dalili na tafsiri. Twaib!.'Wa afttiruu"] na kuleni .sikukuu ,liru'yatih] kwa kuonekana kwake

Hii hadithi inaendelea huko mbele, lakini kitabu nilichokifungua ni kitabu **BIDAY-ATUL MUJTAHID WA NIHAYATUL MUQTASWID**, juzuu ya 1, swafhatu 207. Na hadithi .yenyewe ni Muttafaqun alayh; haina wasiwasi

Naitaja tu kuwa ni muttaffaqun alayh, pamoja na kwamba tumeambiwa kuwa yupo mzee wa musttalahul hadith, na tunakubaliana na sheikh Kadhi. Alhamdulillaah na sisi tunao .wajumbe wa musttalahul hadithi walioko nyuma yangu, bi idhni laahi ta'ala
Kwa hivyo ndungu zangu waislamu, tunatoa katika hadithi hizi tukufu za Mtume wetu swallaahu alayhi was-sallam kuwa mwezi wa Ramadhani huthibiti kwa kuonekana kwa mwezi. Hii ni njia moja.

Ama njia nyengine ya kuthibiti Ramadhani ni njia ya mawasialiano, yaani kupata habari juu ya kuonekana kwake huo mwezi.Kwa sababu yawezekana kuonekana mwezi jimbo moja na jimbo jengine usionekane, au kuonekana mkoa mmoja na mkoa mwengine usionekane. Kama inavyotokea hapa kwetu.Mmara nyingi hupewa habari tu kuwa umeonekana Tabora au Mwanza na siku nyengine huonekana mikoa yote ya Tanzania .pamoja na Unguja na Pemba

Mara nyengine huonekana sehemu ndogo tu ya nchi, kama ilivyotokea Ramadhani hii iliyopita. Sehemu zote haukuonekana mwezi, isipokuwa ukaonekana Lamu, lakini watu walikula sikukuu. Hawakula kwa uroho; ni kwa sababu ya mawasiliano tu, kwa kupata .habari kuwa mwezi umeandama

Tumekula sikukuu au wamekula sikukuu, kwa sababu ya kupata mawasiliano tu. Mikoa 20 ya Tanzania haukuonekana mwezi, mikoa mitatu ya Unguja hawakuuona mwezi na mikoa miwili ya Pemba mwezi haukuonekana. Mikoa yote ya Kenya hawakuuona mwezi, isipokuwa kitongoji kidogo tu cha Lamu ndio waliotupa macho angani na Mwenyezi Mungu akawabahatisha kuuona mwezi. Wakatuletea habari, nanyi mukala!. Inaonesha habari nazo zapokelewa!.

Sasa tumuulize Mtume wetu mtukufu. Habari za kupewa zapokelewa?. Yeye atatujibu, tuone iwapo masheikh zetu wamepatia au wamekosea, kwa sababu na wao ni binadamu, .lakini natumai wamepatia

Twaib!. Sikiliza vizuri maneno ya mtakatifu Mtume aliyesifiwa na Mwenyewe Allah subhaanahu wa taala.Anatusimulia Ibn Omar (R.A) kwa kusema; " Tara'a N-nasu L-hilaala, fa akhbartu Rasuula Llaah swalla llaahu alayhi wa sallam, An-niy ra'aituhu faswaama, wa amara n-naasa bi swiyaamihi", rawaah Abu Dawud wal Haakim wa ibnu Hibaan].

Hadithi hii nimeitoa kwenye kitabu cha **BIDAYATUL MUJTAHID WA NIHAYATUL .MUQTASWID**, juzuu 1, swafhat 209

Jamani!, masheikh zangu watukufu mulioko mbele yangu. Yawezekana kitabu hicho pengine hakipo, lakin una uwezo wa kumwambia huyo aliyeko nyuma yangu, niletea niione eenh!. Twaib!, tunaendelea.

Asema Tara'a N-naasu L-hilaala] waliuona watu mwezi.Fa akhbartu rasuula Llaah], nikampa habari Mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake.

"Faswaama"] akafunga Mtume rehema na amani ziwe juu yake.Wa amara n-naasa biswiyaamihi"]na akawaamrisha watu kufunga kwake.. Siku hiyo, Mtume rehema na amani ziwe juu yake,pamoja na macho yake matukufu sana ,yeye pamoja na maswahaba zake wengine pale Madina hawakuuona mwezi. Aliyeuona ni Ibnu Omar na watu wengine.Lakini walipo kuja mpa habari,Mtume aliukubali, akawaamrisha watu wafunge. Kwa hivyo yaonesha kuwa mawasiliano nayo Mtume rehema na amani ziwe juu yake alikuwa anayakubali. Twaib!, natoa hadithi nyengine.

Wa'ani Ibni Abbas radhia Llaahu an-humaa qaala. Ja'a a'arabiyu ilaa n-nabiy swalla Llaahu alayhi wasallam- faqaala inniy ra'aitu L-hilaala, ya'ani Ramadhaani, faqaala at-tash-hadu an laailaah illa Llah?. Qaala naam!. Qaala at-tash –hadu an-na Muhammada RassuuluLLaah?. Qaala Naam!. Qaala ya Bilaal adhin bin-Naasi fal yaswuumuu ghadan, Min kitaabi Rawdhati n-nadia; sherh Durarul Bahiya juzuu 1, swafhat 327.,

Kitabu hicho nilichokitaja kina umri wa miaka 108.Sasa ndugu zangu naifasiri hadithi hiyo, pengine wengine hawajui kiarabu.

Asema; Wa'ani Ibni Abbas] Na kutoka kwa Ibnu Abbas,Radhia Allaahu an humaa] Mwenyezi Mungu awawie radhi. Qaala] amesema. Ja'a a'arabiyu] alikuja bedui. A'arabiyu ndugu zangu, maana yake ni mtu wa shamba. Bedui ni mtu wa shamba kwa kizungu waita *Bushman*. Ilaa n-nabiy] kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam. Faqaala] akasema huyu mtu wa shamba kumwambia Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam . In-niy ra'aitu L-hilaala] hakika mimi nimeuona mwezi. Ya'ani Ramadhani] mwezi wa ramadhani.

Faqaala] Akasema Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam. **Angalia vizuri hapo ndugu yangu muslamu.** Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alilomuuliza yule Bedui baada ya kusema kuwa kauona mwezi peke yake majabalini huko!, au majangwani. Alimuuliza hivi:- attash-adu an laa ilaaha illa Llaah?] Unathibitisha ya kuwa hapana Mola anayefaa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu?.

Qaala] Akasema yule Bedui. Naam]! Ndiyo!. Qaala] akasema tena Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kumuuliza yule bedui.

At-tash-hadu an-na Muhammadan Rasuula Llaah?] Hivyo wathibitisha kuwa hakika ya Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu?. Qaala] akasema yule bedui, naam!] Ndiyo.Qaala] Akasema Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam.Yaa Bilaal!] Ewe Bilali!.Adhin bin Naasi] Watangazie watu.Falyaswuumuu ghadan] Waje wafunge kesho.

Haya jamani! tujiulize,siku hiyo huyu bwana Mtume na maswahaba zake hawakuuangalia mwezi?.Waliungalia! mwezi 29, lakini pamoja na utukufu wa macho yake na kwa vile Mwenyezi Mungu subhaanahu wa taala ataka kutufundisha namna ya kuandama mwezi, Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam wala maswahaba hawakuuona mwezi pale Madina.

Aliyeuona ni bedui mbaali huko!. Akatoka akaja mpaka akafika Madina. Ilikuwa ni usiku tayari, watu washaamua watafunga mwezi 30 kesho. Lakini Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alipojibiwa na huyu Bedui, akapokea habari;akamwambia Bilali adhini, watangazie watu.

Tukijiuliza kwanini atangazie watu?. Kwa sababu ishakuwa ni Lailatu Ramadhani si usiku tena wa mwezi wa Shaabani. Kwa hivyo watu watangaziwe waje wafunge kesho.

Twasoma nini kwenye hadithi hii ndugu waislamu?. Twasoma ya kwamba haya ni mawasiliano ya mbali. Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kayapokea vile vile. Kwa sababu bedui hakuulizwa, wewe watoka mji gain?, hata ukatuletea habari hii?. Alipompa tu, na akamthibitishia kuwa yeye ni muislamu, basi pale pale Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliupokea mwezi wake.

Ndiyo maana maulamaa wengi hapa kwetu wasema “Habari ya mtu mmoja tu kwa kufunga sie tutafunga”, kwa sababu Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kaikubali habari ya mtu mmoja.

Ewe ndugu yangu mwanamke na mwanaume uliyehudhuria, tega sikio sasa. Kwa sababu huko mbele utakuja ona mambo!.

Twaib!.**Hadithi ya mawasiliano ya mbali sasa**. Ani Abii Umari ibnu Anas ani umumati lahu, min as haabin nabii swalla llaahu alayhi wassallam. Inna rakiban aw rakiba, jaa-uw ilaa nnabii swala Llaahu alayhi wassallam. Yash –haaduuna annahum ra’awuw L-hilaala bil amsi, fa amarahum an yufttiruu,waidhaa asbahuw yaghaduw ilaa muswalaahum].

Hadithi hii rawaahu Abu dawuud wal Baihaqiy. Na tumeitoa hadithi hii kutoka kitabu cha **ALMAJMUI**, sherh ALMUHADHAB, mujalad 5, swafhat 27. Na tumeitoa tena hadithi hii kutoka **SUBULIS SALAMI**, juzuu ya 2, uk 63. Naitafsiri kwa lugha ya kishwahili. Sikiliza vizuri.

Ani abii Umari ibnu Anas] kutoka kwa babi Umari mtoto wa Anas.Ani umumat lahu], kutoka kwa maami zake, min Ashaabin nabii] na ni miongoni mwa maswahaba wa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.

Inna rakiba jaa-uw] hakika msafara ulikuja. Ilaa nnabiy swallallaahu alayhi wassalam] kwa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake.Yash-haduuna] wakamthibitishia.Annahum] hakika wao; huo masafara.Ra’awuw, L-hilaala] waliuona mwezi. bil Amsi] jana. Mwezi waliuona jana.Faamarahum an yufttiruu] Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam

akawaamrisha wafungue, wale sikukuu.Waidhaa asbahuu] na wakishaamka siku ya pili. Yaghaduw ilaa muswalaahum] Waamkie sikukuu yao na miswala yao.

Twasoma nini ndugu waislamu kwenye hadithi hii?. Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam atufundisha nini kwenye hadithi hii?. Angalia matendo ya Mtume tunayojifundisha kwenye hadithi hii.

Ilikuwa mwezi 29, watu wakauona mwezi katika msafara wao. Nao walikuwa kwenye vipando. Ama hawakutubainishia kipando hicho kilikuwa ni ngamia au farasi.Kwa sababu kila mmoja katika wanyama hawa ana mwendo wake. Ikiwa ni farasi ana mwendo wa sawa na hata gari wa kasi ya meli 100 kwa saa.

Kwa kifupi ni kwamba Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliwapokea wasafiri hao waliotoka mbali, waliouona mwezi jana, walio kuja zao moja kwa moja wee! mpaka kukacha siku ya pili. Wakaja zao wee ! mpaka wakafika Madina.

Inasemekana walikuja baada zawali, kiasi inakisiwa ni saa 10 za jioni walipofika, tokea jana walipouna mwezi.Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam na maswahaba zake walikuwa wamefunga ili kutimiza siku ya 30. Kwa sababu wao hawakuona mwezi pale Madina, wala hakuja bedui yoyote aliyekuja kuwajulisha kuwa mwezi mimi nimeuona majabalini. Ndipo ikabidi watimize siku 30.

Sasa je Mtume alipopewa habari kuwa sisi tumeuona mwezi jana!..... Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliwaambia watu fungueni!.Angalia, ilikuwa bado masaa mawili tu. Hakuwauliza mwatoka masafa gani nyie, ili pengine apate kutaradad, kwa sababu masafa yana matlai, au pengine masafatul qasr na pia taqarubil Bilaadi. Hakuwauliza hayo.

Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliwaambia fungueni. Bilal aliamrishwa awaambie watu wafungue. Kwa nini?, Hii ni kutokana na sababu mbili kubwa.Kwanza, wakati Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alipopata habari ilikuwa ni mfunguo mosi,si Ramadhani tena.Itakuwaje watu waendelee kufunga mfunguo mosi!.

Sababu ya pili ni kuwa Mwemyezi Mungu kaandika kwenye Lawhil-Mahfuudh kuwa siku ya sikukuu kwa waislamu kufunga ni haramu. Itakuwaje yeye Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam awafungishe watu siku ambayo ni haramu?.

Ndipo akawaambia watu fungueni.Nasi ndio twala tena!, ruhusa ishatoka!. Wanawake ikiwa washapika wakaanza kuonja. Mnada ushatoka kuwa tufungue.

Hivyo Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliwafuturisha watu kwa sababu hizo mbili kubwa. Hapo twasoma nini?. Kuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam hakuzingatia lolote;bali kazingatia habari tu. Hayo ndiyo mawasiliano ya mbali aliyoyapokea bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam
Mwendo huu ndio alioishi nao Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam , yeye na maswahaba zake. Walikuwa hawazingatii jambo lolote kwa mwezi wa Ramadhani ila kwa .kuona mwezi kwa macho au kwa kupata habari kutoka kwa wenziwao waislamu

Nikurudishe nyuma kidogo tu; kwa sababu kuna habari nyingi. Ni kwamba ujuwe kuwa Ramadhani ilifaradhishwa tarehe 10 mwezi Shaaban mwaka wa pili (2) Hijriaya.Kwa hivyo Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam mwenyewe kafunga si chini ya miaka 8 ndipo akaondoka duniani.

Wakaishi hivyo, yeye na maswahaba zake, hakuna tofauti yoyote. Akaondoka bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam katika ulimwengu.Akakaa ukhalifa wa kwanza Sayyidna Abuubakar (RA) kuwaongoza waislamu kwa muda wa miaka $2^1/_2$, hakujatokezea mtafaruku wowote.

Akakaa ukhalifa Sayyidna Omar ibn Khattabi baada ya kufa sayyidna Abubakar (RA) kwa muda wa miaka 10 hakujatokezea mtafaruku wowote.Akafariki Sayyidna Omar, kwa kuuliwa na kafiri Abu Lu'ului. Akakaa ukhalifa Sayyidna Uthman bin Affan kwa kipindi cha muda wa miaka 13, hakujatokezea mtafaruku wowote. Waislamu wanakwenda vizuri ;wanafunga na kufungua kwa kuonekana mwezi na kwa kupata habari.

Akabeba ukhalifa Sayyidna Ally bin Abitaalib kwa kipindi cha takriban miaka 3, hakujatokea tatizo lolote, waislamu wanakwenda sawasawa, mpaka mwenyewe Sayyidna Ally bi Abitaalib akasema "Mie kufunga siku moja ya Shaaban ni bora kwangu kuliko kuja nikala siku moja ya Ramadhani."
Kwa sababu Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema; Mtu kula siku moja tu ya Ramadhani kwa kukusudia au kwa kufanya uzembe wake mwenyewe, basi ajuwe kuwa hata akifunga milele hawezi kuilipa siku ile. Ndio maana maswahaba walikuwa na hadhari sana.

Sasa jee?, hizi hitilafu jee?, hizi zilizotukutanisha hapa jee?, Ndugu waislamu zilianza liini?. Tega sikio.

Ndugu waislamu, baada ya kuuliwa Sayyidna Ally bin AbiTatib kwa matatizo yake, yeye .na bwana Muawiya bin Sufiyani, ikabidi abayiwe sayyidna Hussein

Lakini Sayyidna Hussein ukhalifa hakuuweza. Ikabidi wakubaliane na Muawiya. Ampe ukhalifa Muawiya. mpaka atakapokufa Muawiya ndipo achukue sayyidna Hussein.

Hivyo ni historia, nafikiri mwaifahamu ndugu waislamu, sitaki niiendeleze, Tuende hapo .mbele

Yaliyotokezea baada alipokaa sayyidna Muawiya. Kwanza alihamisha dola, yaani makao makuu ya serikali ya kiislamu, kutoka nchi ya Iraq na kuipeleka kwenye nchi ya Sham; Syria. Akawa yeye Muawiya yuko katika nchi ya Syria.

Hapo ndugu waislamu, ndipo kilipoanza hicho kisa kilichotufanya tuje tukutane hapa leo. Twaib! Kisa chenyewe kinaitwa kisa cha Kuraib.

Kuraib ni miongoni mwa watabiina. Alikuwa ni mtumisi wa Abdullahi bin Abbas. Sasa kilitokezea vipi?. Sikiliza ndugu yangu.

Naisoma hadithi kama ilivyo. Na hadithi hii imo katika vitabu vingi, hata sahihi Muslim ila sahih Bukhary. Lakini mimi naisoma kutoka kwenye kitabu cha **RAWDHATI NNADIYA**, sherh Durarul Bahiya. Kwa sababu kuna maelezo nitayahitajia baadae. Twaib!.

Ani Kuraibin, Anna ummal fadhli, baathahu ilaa Muawiyata bi Shaam, ayyi Syria. Faqaala qadimtu shaaama, faqadhaitu haajataha wastuhila alaiya Ramadhaan wa anaa bi Shaam.Ra'aitul hilaala laiatal jum'aa, thumma qadimtul Madinata fiy aakhir Shahar.

Fasa'alaniy Abdullah bin Abbas, thumma dhakara liy-L-hilaala. Faqaala mataa ra'aitumul hilaala?. Faqultu, Ra'ainaahu lailatal Jum'aa. Faqaala anta ra'aitahu? Faqultu naam!. Wara'ahun Naasu faswaamuw, waswaama Muawiya. Faqaala, laakin-naa ra'ainaahu lailata Sabt, falaa nazaalu naswuumuw hataa nukmila thalathiina aw naraahu.

Faqultu, al-laa taktafiy bi Ru'yati Muawiyah wa swiyaamuhu?. Faqaala, laa! Hakadahaa amaranaa Rusuulu Llaaah swallallaahu alayhi was-sallam. -Rawaahu jamaatu illa Bukhariyu wa ibnu Majah.

.Twaib! Twakifasir sasa kisa cha kuraib

.Ani Kuraib] kutoka kwa Kuraib. Anna Ummal Fadhli] kwamba mama Umal Fadhli Maelezo yakaendelea mpaka pale Ibnu Abbas alipomuuliza Kuraib"Mataa Ra'aitumul .?Hilaala] Muliuona lini mwezi huko

Faqultu] nikasema; asema Kuraib. "Ra'ainaahu lailatal jum'aa"] tuliuona usiku wa Ijuma. Faqaala]akasema, anta Ra'itahu ?] na wewe uliuona mwezi?.Faqultu naam] nikasena ndiyo!. Waraahu nnasu] na watu wameuona. Faswaamuu] na wakafunga hao watu, .waswaama Muawiya] na Muawiya akafunga

Faqaala] akasema; Ibnu abbas.Lakinnaa ra'ainahu lailata Sabt] Lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi. Falaa nazaalu naswuumu] hatutaacha kufunga.Hataa nukmila thalaathina] mpaka tutimize siku thalathini.Aw naraahu] au tuuone; huo mwezi. Faqultu, nikasema, asema Kuraib kumwambia Ibnu Abbas.**Sikiliza ibara hiyo inavyosema** !" Alaa Taktafiy bi ru'yati Muawiyah wa swiyaamih?]. Hivyo wewe;Ibnu Abbas hutosheki kwa kuuona Muawiya na kufunga kwake?. Faqaala] akasema Ibnu Abbas. Laa! Hakadhaa amaranaa Rasuulullaahi swallallaahu alayhi was-sallam" sivyo!].Sivyo!, Hivi ametuamrisha mjumbe wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu yake.

Sasa matatizo yamezuka kwenye ibara ya luga ya kiarabu, anaposema **Laa! hakadhaa .amaranaa rasuulu llaah**

Tuchukue **KISTATEMENT**; kimaaelezo. **Hapa ndipo palipozuka mushkeli ndugu zangu waislamu!**. *Ili kusisitiza anachokisema skh Yussuf Hamza akawa anarudia maneno*

huku akigonga meza; akaendelea: Mie sitaki nitoe tafsiri, wako wenyewe wenye lugha na mafani yao walioko nyuma yangu. Watakuja wenyewe baadae wakipata nafasi. Na sina muda mrefu nitampisha mwenzangu, lakini nataka nieleze tu wanazuoni walivyoifahamu .ibara hiyo

Mtoto uliye kushoto kwangu, hebu niletea kitabu kinachoitwa **RAWDHATUN NADIA**, sherh. Durarul Bahiya swafhat 331. Sitaki nisome kwenye karatasi, nataka nikisome hicho .kitabu hasa!, wenzangu wanione

Akawacha karatasi yenye maelezo ya kumuongoza, akapokea kitabu kilichofunuliwa tayari na kusoma;- Idhaa Ra'ahu] Watakapouna,ahulu baladin] watu wa mji fulani mwezi.Lazimma] itawalazimu, saairul bilaadil muwaafaqa] nchi zote. Italazimu nchi nyengine kuwafikiana uoni huo.

Ikiwa sivyo ninavyotafsiri mutakujanambia eenh!. Kiswahili chanipa tabu kidogo. Wanswahahul hadithil muswaarakha] imeeleza hadithi hii iliyo wazi,Bi swiyaami biru'yatih] kufunga kwa kuonekana kwake mwezi, wa ifttaari biru'yati] na kufuturu kwa kuonekana kwake. Hivyo ni sikukuu eenh!.Wa hiya khuttaabun lijamii'il umma] Asema hayo maneno hayo, ni khutba wanapewa umati wote wa Muhammad. Khutba hiyo ni kwa watu wote, umati Muhammad.

Faman ra'ahu minhum] basi atakayeuona mmoja wao; kati yao. Fiy ayyi makaani inakaana] Pahali popote patakapokuwa. Dhaalika ru'yatun lijamiihim] Uoni utakuwa wa watu wote. Wa amma al-istidlaali bi man stadala].Ama kutolea ushahidi, kwa yule anayetolea ushahidi.Bi hadithi Kuraibi in'da Muslim wa ghairihim] kutolea ushahidi kwa hadithi ya Kuraib iliyo kwenye kitabu cha Muslim na kwenye vitabu vyengine.

Li annahu stuhila alayhi] kwamba yeye aliandamiwa na mwezi wa Ramadhani.Wahuwa bi Shaam] na yeye akiwa yuko Shaam.Fara'ahu l-lhilaal lailatal jum'aa] akauona mwezi usiku wa Ijumaa.Faqadima Madinata] akafika Madina.Fa akhbara bidhaalika] akatoa habari hiyo kumpa Ibnu Abbas.Faqaala] akasema Ibnu Abbas.Lakinnaa ra'aainahu lailata sabt] lakini sisi tumeuona mwezi usiku wa kuamkia Jumamosi.Falaa nazaalu naswuumu] hatutawacha kufunga.Hataa nukmila thalaathiina aw naraahu] mpaka tukamilishe thalathini au tuuone, mwezi.

Thumma qaala hakadhaa amaranaa Rasuulallaah] kisha akasema hivi ndivyo alivyotuamrisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu yake.Walahu alfaadhun ghairu swahiihun] hadithi hii ina matamshi yasiyo kuwa sahihi.

Msikilize vizuri mtaalamu huyo!, ikiwa wataka kuja kumkosoa ili upate *POINT* ya kumkosoa.

Li annahu lam yuswarakh] hadithi hiyo haikuweka wazi;hakuweka wazi Ibnu Abbas. Bi anna Nnabiya] kwamba Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam. Amarahum bi an laa ya'amaluu bi ru'yati ghairihim] aliwaamrisha eti kwamba wasije wakatumia mwezi kwa uoni wa watu wengine. Haikuweka wazi hadithi hiyo, miongoni mwa watu wa habia mbali mbali na nchi mbali mbali.

Bal araada Ibnu Abbas bi ikmaali thalathiina aw yara'uh] lakini alitaka yeye Ibnu Abbas. .Kwamba hakika yeye aliwaamrisha watu kukamilisha siku thalathini au wauone mwezi

Dhanna minhu anna L-muraada bi ru'yati, ru'yat ahali mahalli] kwa kudhania yeye mwenyewe Ibnu Abbas kwamba muradi wa kuuona. Yeye alidhania kuwa uoni wenyewe ni kuuona mahali tu, lakini pahali pengine itakuwa labda haifai.Wa haadha khattaun bi istdlaali] asema mwenye kitabu hichi "Hili ni kosa linalomtokea mwanadamu yeyote .katika kutolea ushahidi"

Aw-waa Nnaasu bil habatti wal khalatti] Kosa hili limewaweka watu katika kuchanganyikiwa kwenye akili.Hat-taa tafarraquu dhaalika alaa thamaniati madhaahibi] Mpaka watu wametafautina juu ya jambo hilo katika madhehebu manane.
Hadithi ya Kuraibu imewachanganya watu, mpaka wametafautiana madhehebi manane.

Kwa hivyo ndugu zangu, mchangiaji atakayekuja kuchangia dhidi yangu kwanza itabidi atubainishie madhehebi yake miongoni mwa madhehebi hayo manane. Kwa sababu huko .mbele nenda kutaja maimamu

Labda nikusaidie tu, mwenzangu pengine katika kuttalii ilikupita, hujui ni madhehebi .yapi, mimi nitakupa madhehebi matatu tu

Wako waliotafautiana, wasema sie twafuata taqarubil bilaadi], na wengine wafuata .masafatul qasri], yanaani kilomita 89. wako na wanaofuata mattalai

Kwa hivyo utachagua iwapo ni moja kati ya hayo utatueleza, laa ni jengine utatafuta .mwenyewe

Tumeshaona kuwa hadithi ya Kuraibu imewagawa watu kwenye makundi manane. Hebu tunaglie hawa maimamu wetu, wako kwenye msimamo wa mgawanyiko huu?, au wako kwenye msimamo ule ule wa tangu asili, wa Mtume wetu Muhammad swalla llaahu alayhi ? wa ssallaam

Ndugu mwenye kitabu ningekuomba unipatie kitbu cha **AL MJMUI**, sherh Almuhadhabu lil imami Abuu Zakariya Yahya Sharaf Nawawiy, juzuu ya 6, swafhat 274; mlango unaosema **Madhaahibul Ulamau fiy maa idhaa ru'iya L-hilaalu ahalu baladi duuna ghairihim.**

Nataka kisoma kitabu hichi,sikiliza vizuri, ndugu yangu muislamu. Twataka wasikiliza nani?. Ni maimamu wetu !.Kwa sababu kuna wenzetu wengine watutupia dhana. Wasema hawa wanao funga kwa kufuata mwezi popote hawa ni mashia, ni makadiani, wengine hawa ni wahabi na majina mengine wanayotupakazia.

Lakini sasa wasikilize maimamu wetu halafu huo mpakazio wako uuegemeze huko. Kama .!hatuko huko basi ututoe. Twaib

Wa ani Laithi, wa Shaafi'iy, wa Ahamadi yalzamul jami'i .Qaala walaa a'alamuhu illa qaulul Madani'y, wa Kufiy, Malikan wa Aba hHanifa].

.!Nataka nifahamishe qaida ya lugha kidogo, ili isije ikatupita eenh
Tukisema Shaafi'iyu, maana yake ni Shaafi mwenyewe. Ukisema Shaafi'iyatu kwa twaau .marbutta ni wafuaasi wa Shaafi

Hapa atwambia Wa ani Laithi wa Shaafi'iyi wa Ahmad] kutoka kwa Laithi,imamu maarufu huyu katika madhehebi. Na Shaafi mwenyewe na kwa imamu Ahmad.

Yalzamul jami'i] Itawalazimu watu wote. Watu wa lugha wasema fi'ilul mudhwaari'i marfu'u bidhwamati yadul-lu alal asli].
Ibara hii kaitoa mkuu wa madhehebi ya Shaafi, imamu Nawawiy tuliyemtaja. Asema madhehebi ya Laithi, ya Shaafii na ya Ahmad,ya kwamba itawalazimu watu wote .ukionekana mwezi katika nchi Fulani. Halafu asema

Walaa a'alamuhu illa qaulu Madaani'y wal Kufiy, ya'ani Malikan wa Aba Hanifa] Wala haikuwa kauli ninayoijuwa isipokuwa kauli ya watu wa Iraq, inayokubaliana na kauli za .imamu Maliki na imamu Abu Hanifa

Kwa hivyo akusudia kutufahamisha kuwa na imamu Maliki na imamu Abu Hanifa .wamekubaliana kuwa mwezi ukionekana popote duniani, watu wote wafunge

Kasema yalzamu, sio kwamba ni khiyari; itawalazimu watu wote wafunge. Haya ndiyo madhehebi yetu twatangaza. Ndipo tulipotegemea. Sisi twategemea Shaafi, Maliki, .Hambali na Hanafi

Ndugu waislamu!, mambo haya nataka muyaelewe vizuri. Na hawa nao wana wafuasi wao. Shaafi ana wafuasi wake, Malik ana wafuasi wake, Hambali na wake na Ahmad naye .ana wafuasi wake

Nataka niwape nafasi na wenzangu, lakini nataka niwaambie hivi;- Wafuasi wa Maliki wote wamekubaliana na imamu wao, wafuasi wa Ahmad bin Hambali wote wamemkubali imamu wao. Wafuasi wa Abu Hanifa nao wamemkubali imamu wao. Isipokuwa wafuasi wa imamu Shaafi wamegawika sehemu mbili;**two kinds**

Wamegawika sehemu mbili. Kundi linalomkuli imamu wao na kundi lisilomkubali imamu wao. Kundi lisilomkubali imamu wao ndilo lililogawika madhehebu manane hayo .unayong'ang'ania weye

Nataka nizungumze kwa furaha leo, isiwe tena huyo !,huyo! Ansaar.Kwa sababu serikali .inawapenda sana ndugu zetu hawa. Kwa kifupi leo hatutishani, bali twashindana kwa hoja

Sasa ndugu zangu, nataka nihitimishe mada yangu kwa kuwasomea vitabu vilivyoungana .na haya nliyoyasema, mbali ya hawa maimamu

Kitabu kinachoitwa **RAWAAIHUL BAYYAAN** fiy tafsiril Qur'aan, yaani Rawaahil Bayyaan fiy tafsiir ay-yaatil Ahkaami. Baabu ikhtilaafil mattaali'i, juzuu ya 1, swafht 211. .Mwenye vitabu nitolee kitabu hicho

Sikilizeni vizuri, Rawaaihul Bayyaan ni maarufu, kutaja aya tupu za hukumu; ahkaam-.kwenye vitabu vyake. Kwa hivyo ukitaka hukumu yoyote ya aya utachukua kitabu hicho

Naisoma ibara kama ilivyo. Hapa atakuwa anataja kuthibitisha ile kauli yangu kwamba wale wafuasi wa madhehebi mbalimbali wamesema vile.

Anasema katika mlango wa 10, hal yu'utabaru ikhtilaaful mattaali'i fiy ujuudi swaum?]. Jee huzingatiwa tofauti ya matlai katika kufunga Ramadhani?.Dhahaba L-hanafiyatu walmalikiyatu wal hanabilatu, ilaa annahu laa ibratan fiy ikhtilaafil mattaali'i. faidhaa .ra'aal hilaala ahlu

Jamani naondoka sasa hivi !. Watu kule nawasika wasema waumia magoti, wasema khee .leo ni khatari !. Alaa kulli haal
Dhahabal Hanafiyatu] Wamekwenda watu wa Abu Hanifa. Walmalikiyatu] na watu wa Maliki. Wal hanabilatu] na watu wa Hambali, ilaa annahu] kwamba hakika. Laa ibratan] .hapazingatiwi kabisa. Fiy ikhtilaafil mattaali'i] kaitka kutafautiana matlai

Faidhaa raa'alhilaal ahlu baladin] watakapouona mwezi watu wa mji wowote. Wajaba swaumu alaa baqiyatil bilaadi] italazimu kufunga kwa nchi zote zitakazobakia.

Sikiliza vizuri neno alilotumia;**ITALAZIMU** !. Li qaulih] kwa neno lake Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam "swuumuw liru'yatih wa afttiruw li ru'yatih] fungeni kwa kuonekana kwake, na fungueni sikukuu kwa kuonekana kwake.Wa huwa khittaabun aamun lijami'i l-umma] nayo ni khitaabu iliyoenea kwa watu wote, kwa umati wake Muhammad swalla llaahu alayhi wa ssallaam

Faman ra'ahu] Basi yeyote atakayeuona. Minhum] kati yenu, nyinyi waislamu. Fiy ayyi makaani] pahali popote, Kaana dhaalika ru'yatun lahum jamia nh] utakuwa huo ni uoni .kwa watu wote

Haya! Hii utasema ni madhehebi ya Hanafi. Sasa nipatie kitabu kinachoitwa **FIQHU .SUNNA**, mujalad wa 1juzuu ya , swahifat 439, Baabu ikhtilaaful mattaali'i

-Nakisoma tena Fiqhu Sunna; ni kitabu maarufu, mijeledi mitatu **3; VOLUMES**
Ikhtilaaful Mattaal'i] kutafautiana matlai. Dhahabal jamhuur al ulamaai] wamekwenda .jamhuri. Ukisikia jamhuri ni wazee wetu wanne. Huwa washaingia na wengineo

Ilaa annahu laa ibrata bi ikhtilaafil mattaali'i] kwamba hakika hakuna mazingatio katika .kuhitilafiana matlai. Hayazingatiwi kabisa katika sheria

Famataa raa'al hilaala ahlu baladin] na popote watakapouona mwezi watu wa mji wowote. Ahalu baladin nimeifasiri ni watu wa mji wowote, kwa sababu imekuja naakira, haikuja ma'arifa.Wajaba swaumu alaa jami'il bilaadi] itawalazimu kufunga watu wa miji yote;nchi .zote

Hapa kwetu hata ukikusudia miji ya Chake Chake na Mkoani basi watu .watakurudisha.*Twaib!,alaa kulli haal*
Bi qauli Rasuuli] kwa kauli ya neno lake Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam.Atolea ushahidi jina la Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam.Swuumuu *li ru'yatih wa afttiruu li ru'yatih]* fungeni kwa kuonekana kwake na fungueni kwa kuonekana kwake.Na kweli Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alikuwa akifunga na kufuturu kwa kuonekana kwake.*Wa huwa khittaabun aamun li jamiil umma]* hiyo ni *khittaabu* iliyoenea kwa umati wote wa Muhammad.Hapa Mtume yuko Madina lakini awahutubia waislamu wote.

Faman ra'ahu minhum fiy ayyi makaan] basi atakayeuona kati ya waislamu hao ,pahala .popote.*Kaana dhaalika ru'yati lahum jamianh*] utakuwa uoni huo ni uoni kwa watu wote

Namalizia maudhui yangu niwapishe wenzangu kwa kitabu ambacho nasadiki kila mmoja **.**wetu anacho nyumbani kwake.Kitabu hicho kinaitwa **FAT*HUL MUINNU***
Hebu nifungulia ukurasa wenye habari hizo.Ikiwa mwanafunzi wewe umeusahau ukurasa huo, nitakupiga konzi,kwa sababu itakuwa huna mazingatio.**Kitabu kikaletwa kikiwa .tayari kimefunguliwa ukurasa wa 57.Akaendelea**

Tuko kwenye ***fathul* mu*innu***.Kitabu chenyewe hakina shaqli.Nikikosea irabu nisameheni.Asema:*Waidha thabata ru'yatuhu bi baladin*] na ikithibiti uoni wake katika nchi yoyote. *Lazzimaa hukmuhu Libaladil qariib]* hukumu yake italazimu nchi zilizo karibu.*Duuna l baiidu*] si nchi za mbali.*Wa yuth bitu L-baiidu bil ikhti laafil mattaali'i .walal aqsi*] na itathibiti nchi zilizo mbali kwa kukhtilafiana matlai

Walmurad bil ikhtilaafihaa] na muradi juu ya kukhtilafiana kwake.*An yataba'ada l-mahalaani li halli*] ni kutafautiana sehemu mbili kwa sifa.*Law ru'iya li ahlihimaa*].Lau ungeonekana mwezi katika moja ya sehemu hizo.*Lam yu'ra fil aakhar]* aghlabu .hauonekani katika nchi nyengine

Qaala fil anwaar] maneno hayo ameyasema katika kitabu kinachoitwa *An waaru Sania*.Taaj anapinga kwa kusema.*Laa yumkinu bi ikhtilaafib bi aqali min 24 farsakhan]* haiwezekani kutafautiana kwake kwa uchache wa farsakha 24.Farsakha moja ni meli .3..*Alaa kulli haal* si zaidi ya meli 80

Kwa hivyo, hawa wote wametafautiana ,huyu bwana wa matlai apingwa na huyu mzee wa masafa.Asema yeye hamkubali mzee wa matlai.Ataka tufuate masafa ya farsakha hizo.

Mambo si hayo!,sikiliza hapo mbele.*Wanabaha Subkiy]* Subkiy awatanabahisha.Imamu Subkiy awatanabahisha hawa wawili.*Watabiahu ghairahu*] na wakamfuata wengineo.*Alaa annahu]* kwamba hakika ya mambo yalivyo ,si hivyo.Asema:*Yalzamu mina ru'yati minal* baladi sharqiy] italazimu katika kuona katika nchi ya mashariki.*Ru'yatuhu fil baladi gharbiy]* *u*oni wake katika nchi za magharib*i.Minghair aqsi] NOT OPPOSIT**E**;*sio kinyume .chake

:Kwanini tusimuulize mtu akwambiaye hivyo?.Atajibu kwa kusema *Idhi lailu yad khulu fil bilaadi sharqiy]* wakati wa usiku huingia nchi za mashariki kwanza..*Wa kudhiat kalaamuhu*] Na kumbuka maneno yake.*Annahu mataa ru'iya fiy sharqi lazimmaa kullu ardhi bi nisbati amali bi tilka ru'iya]*.Wakati popote utakapoonekana katika nchi za mashariki italazimu nchi zote za magharibi kwa munasaba wa kufanyia kazi.Kwa maana ya kutekeleza kwa uoni huo.*Wa idh yakhtalafal mattaa*li'i] .japo wakitafautiana matlai

*S*asa hii inafuatana na jiografia.Ilikuwa aje mtaalamu wake hasa.Sitaki niendelee,lakini kwa kifupi ukiangalia ramani ya dunia,nchi za magharibi kwenye longitudo 45 tulipo sisi.Fuata **.**Makka mpaka utafika **Zanzibar**

Kwanza nataka niwatowe mashaka ndugu zangu ,kwani kuna baadhi ya watu husema sisi na Saudi Arabia tuna tafauti ya siku nzima.Kule ikiwa Alkhamis sisi huku huwa ni Ijumaa.Si kweli ndugu zangu!.Sisi na Makka ,hapa tulipo hatuna tafauti ya siku moja.Sisi na Makka hapa tulipo hatuna tafauti ya hata saa moja.Sisi na Makka hapa tulipo hatuna .tafauti ya hata sekunde moja

Watu wa jiografi wapo wanajua hivyo.Na jiografi si mambo ya kizungu;ni mambo ya .Mwenyezi Mungu ,ile ni ya kiislamu

Mie niliondoka Daaru Salaam saa 12 asubuhi kwa DC-9 ,tukafika Jeddah saa 4.30.Mwendo wa kutoka Jeddah mpaka Makkah ni saa 1.30 kwa basi.Lau si mambo ya kastamu basi Sala ya Ijumaa siku hiyo tungeisalia Makkah ilhali asubuhi tulikuwa .Tanzania

Saa zetu hatukubadilishapo tulipokuwa Saudi Arabia na sheikh Hilali ni shahidi.*Alaa kulli haal* ndugu yangu mtukufu; msikilizaji.Namshukuru Rabul Izza,aliyenipa uwezo wa kuihadhiri mada yangu hii, ambayo nimeileta mbele yenu.Napenda niwatanabahishe kuwa madhehebi yangu bado nimeganda kwenye kiti cha imamu Shaafi mpaka hapo utakapokuja .kuniondoa kwa hoja

Wa ilaa hunaa aquulu qaulu haadhaa wa astaghfiruLlaah waliy wa walakum. Wassalaam alaykum warahmatuLlaah wabaraka-hu.

Mwenyekiti;sheikh Kadhi wa wilaya ya Mkoani akachukua kipaza sauti na kusema kuwa kabla watu kwenda kuswali adhuhuri angeruhusu watu wachache wamuulize sheikh Yussuf ,ili wawekewe wazi pale ambapo bado walikuwa na mashaka napo.

Sheikh Yussuf akasema yeye haogopi maswali,lakini alivyopenda yeye wawachiwe watu wa upande wa pili watoe hoja zao,wasikilizwe.Kwa sababu wasikilizaji wana akili

timamu watapima hizo hoja.Zaidi ya hivyo alitaka awachwe akapate chai kwani tangu .asubuhi mpaka wakati huo alikuwa bado hajakunywa chai

Kwa maelezo hayo kadhi akamkubalia na watu wakachawanyika kwa mapumziko na .swala

HOJA ZA BAKWATA,SHEIKH MOHAMMED ADAM MAKAME

Baada ya masheikh na muhadhirina kuswali adhuhuri,msemaji akasimama na :kusema

Msemaji wa mwanzo;sheikh Yussuf Hamza katoa ushahidi wake.Sasa ni zamu ya :wachangiaji wa upande wa pili.Sheikh akasimama na kuendelea

Assalaam alaykum warahmatullaah taala wabarakathu.Jina langu ni Mohammed Adam .Makame.Nimesoma katika msikiti wa Mbigilini Uweleni kwa muda wa miaka 10 Sijaenda kwenye chuo chochote.Lakini Mwenyezi Mungu subhaanahu wa taala humpa .hikma yule amtakaye pasipokuwa sababu yoyote.Umri wangu ni miaka 30

Nikiendelea na mada,nitaanza kujibu hoja za sheikh Yussuf Hamza,moja baada ya moja .kwa muda nitakaoruhusiwa

Hoja ya mwanzo;sheikh Yussuf katoa hadith hapa ,hadith mbili.Kwanza kasema *idhaa ……ra'aitumul hilaal…* na hadithi ya pili *swuumuu Liru'yatih wa afttiruu Liru'yatih* Lakini hadithi hizi sheikh Yussuf hakuzimaliza .Na jambo lolote lazima lipatikane mwanzo .wake na mwisho wake,lisiwe *munqatta'a*

فوئل للمصلين Mfano Mwenyezi Mungu aliposema *Fawailun limuswaliina* basi sisi .tusingekuwa tukiswali.Lakini lazima yapatikane mambo yanayokuja mbele yake kule

Katika hadithi hii Ibnu Omar (r.a) kasema *sami'itu Rasuula Llaahi alayhi wasallam]* nimemskia mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake akisema:*idhaa ra'aitumuhu faswuumuu,waidha ra'aitumuhu fafttiruu]* mutakapouona huo mwezi .fungeni,na mutakapouona mufungue

Hadithi hii niliyoitoa iko katika **SUBULI SALAMI**,Vol 1,jz2.Katika nuskha yangu mimi ni ukurasa wa 151.*Fain ghumma alaykum*] kutakapotanda mawingu kwenu basi kamilisheni 30.Twauliza suala hapa, jee mawingu hayo yatanda ulimwengu mzima kwa .?wakati mmoja

Katika hadithi hiyo hiyo kwenye kitabu hicho hicho Subuli salami,mshereheshaji wa kitabu hicho asema *wal ma'ana idhaa ra'aitumuhu,ayyi idhaa wajadtmuhu fiy maa bainakum ru'iya]* Utakapopatikana baina yenu nyinyi uoni,yuko mmoja kauona,basi itakuwa mumeshauona.

Wayadullu alaa anna hadhihi ru'iya ,ru'iya jamii haadhihil bilaadi] Hakika kuonekana huku ni kuonekana kwa watu wa nchi ile.*Bilaadu* ina maana nyingi.Kuna *bilaadu* kwa

maana ya nchi, na *bilaadu* kwa maana ya mji.*Falyalzamul hukmu]* italazimu hukmu ya watu wale.Wala haizingatiwi kwa sababu wote ni watu wa nchi moja;haizingatiwi kabisa.

Anaendelea kusema katika sherh hiyo hiyo *waidhaa ra'aitumuhu;ayyi khittaabu linnaasi makhsuusiina]* Imezungumziwa watu maalum ,haikusemwa *jamiu nnaasu*.

Watakrabu luzuumu ahlu baladu ru'iya] Na ukamilifu wa kulazimu jambo hilo ni wale watu wa mji waliouna mwezi.*Wamaa yatassilu bihaa min jihati latiy samatiha]* Na nchi au miji inayokamatana katika pande zilizoshikamana.

Lakini hadithi ya 63 katika hiyo hiyo Subuli salami vol.1,jz2 wako wanaosema kuwa bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam anafahamisha kuwa kila kitu chetu kiwe kimoja kwa kusema katika hadithi ya 1 *baabu idain*.

An Aishata radhiallaahu anhaa,qalat ;Qaala Rasuulullaahi alayhi wasallam].Kasema bibi Aisha (r.a) kuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema.*Alfittru yawma yufttiruu nnaasi]* Kutoa zakatul fitri ni siku wanapotoa zakatul fitri watu.*Wal udh hiya yawma yudhwaahu nnaasu]* Na kudhwahi- kuchinja ni siku wanapodhwahi-wanapochinja watu.*Rawaahu Tirmidhiy*.

Kisha akaendelea sheikh kusherehesha katika hadithi hiyo;*wa fiihi daliilun]* kwamba kuna dalili nyingi katika hadithi hiyo.*Alaa annahu yu'utabaru bi thubuutil iddain an yuwaafiqu li nnaasi]* kwa hakika huzingatiwa zile idi mbili kwa kuwafikiana watu.Na lazima sheikh anafahamu .Kwa sababu wao ndio waliozisoma ndipo na sisi tukazisoma na kuzifahamu.

Ni watu gani?.Wa ulimwengu mzima tuwafikiane katika idi au ni vipi?.Siyo!, kwa sababu Ibnu Abbas hukmu ya mwezi wa Sham alipokuja bwana Kuraib akampa habari ya kuwa sisi tumeuona mwezi kule Sham siku ya Ijumaa .Alipokuja huku ,naye akasema sisi tumeuona siku ya Jumamosi.

Alipofika pale ina maana ni mwezi thelathiini,ni siku ya 31 kwa bwana Kuraib.Ibnu Abbas alimuamrisha Kuraib afunge siku 31 ili awafikiane na watu katika mji pale Madina.Utapata hiyo kwenye uk.wa 63 jz.2,Vol.1 .Kasema *innamaa wamaanaahu hadithu Ibnu Abbas,waqad qaala lahu Kuraib]* Na maana yake hadithi ya Ibnu Abbas,alimwambia yeye Kuraib.*Innahu swaamuw Muawiya wa ahlu Shaam]* Hakika wamefunga watu wa Shaam pamoja na Muawiya.*Bi thubuuti yawmul jum'aa]* Kwa kuonekana mwezi siku ya Ijumaa.*Wa qadima ilaa Madina fiy aakhir shahar]* Na akafika Madina mwisho wa mwezi.

Wa akhbarahu bi dhaalika] Na akampa Ibnu Abbas habari juu ya hilo;kwamba sisi tumeuona siku ya Ijumaa.*Wa qaala Ibnu Abbas lakinnaa ra'ainaahu lailata sabt]* Akasema Ibnu Abbas;lakini sisi tumeuona usiku wa kuamkia Jumamosi.*Falaa nazaalu naswuumuu hataa nukmila thalaathiin aw naraahu]* Hatutawacha kufunga sisi mpaka tutimize siku 30 au tuuone.

Hakukubali tu kufunga kwa kuwa Shaam washauona na Muawiya ni kiongozi wetu; wetu.Akasema hataa lazima na sisi tuuone *Qultu,al laa taktafiy bi ru'ayati* mtawala *Muawiya?]* Nikasema jee wewe hakukutoshelezi kuuona mwezi Muawiya na watu wote huko Shaam?.Akajibu *Laa! Hakadhaa amaranaa rasuula Llaah]*. Hivi ndivyo alivyotuamrisha Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam tufunge. Hii Laa kokote utakakoipeleka itakubali .Ukisema Naam pia itatosheleza kuwa ndivyo alivyokusudia Ibnu Abbas.Tufunge vipi?.Tufunge tukiuona na tufutari tukiuona.Sio kufuata watu wa Shaam tu.

Mtungaji ameendelea kusema .Hakika Kuraib alimtaka Ibnu Abbas atimize funga yake ingawa alihakikisha kuwa siku ile ni ya idi .Lakini kwa sababu sasa yuko Madina hana uwezo tena wa kufuata watu wa Shaam.

Dhati ya hadithi inafahamisha kuwa mwezi ni wa pale mtu alipo.Lakini wenzetu hawa inasikitisha sana.Ikiwa Ibnu Abbas hakuukubali mwezi wa Shaam ambapo ni karibu zaidi na Madina.Vipi sisi huku tuukubali mwezi wa Saudia ambako ni mbali zaidi?.

Ibnu Abbas si kwamba hakuukubali mwezi wa Shaam kwa ajili ya *ikhtilaaful mattali'i]* hakulisema hilo.Hakuukubali kwa sababu wao pale Madina walikuwa bado hawajauona mwezi.Ingawa sisi hapa na Saudia tunafunga na hatuna *ikhtilaaful mattali'i*.

Vile vile hadithi ya 6 uk. wa 153 Subuli ssalam ni dhahiri kuwa hadithi hii ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam yaonesha kuwa hakuwatoa watu Madina kupeleka habari nchi za mbali kila wakati ilipokuja habari ya kuonekana mwezi.

Kisha akaendelea sheikh kusherehesha katika hadithi hiyo;*wa fiihi daliilun]* kwamba kuna dalili nyingi katika hadithi hiyo.*Alaa annahu yu'utabaru bi thubuutil iddain an yuwaafiqu li nnaasi]* kwa hakika huzingatiwa zile idi mbili kwa kuwafikiana watu.Na lazima sheikh anafahamu .Kwa sababu wao ndio waliozisoma ndipo na sisi tukazisoma na kuzifahamu.

Ni watu gani?.Wa ulimwengu mzima tuwafikiane katika idi au ni vipi?.Siyo!, kwa sababu Ibnu Abbas hukmu ya mwezi wa Sham alipokuja bwana Kuraib akampa habari ya kuwa sisi tumeuona mwezi kule Sham siku ya Ijumaa .Alipokuja huku ,naye akasema sisi tumeuona siku ya Jumamosi.

Alipofika pale ina maana ni mwezi thelathiini,ni siku ya 31 kwa bwana Kuraib.Ibnu Abbas alimuamrisha Kuraib afunge siku 31 ili awafikiane na watu katika mji pale Madina.Utapata hiyo kwenye uk.wa 63 jz.2,Vol.1 .Kasema *innamaa wamaanaahu hadithu Ibnu Abbas,waqad qaala lahu Kuraib]* Na maana yake hadithi ya Ibnu Abbas,alimwambia yeye Kuraib.

Ani Ibnu Abbas r.a.Anna a'arabiya ja'a ilaa n-naiby swalla llaahu alayhi wasallam].Hakika hilo jitu la shamba alikuja kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam .*Faqaala inniy ra'aitul hilaala]* Akasema hakika mimi nimeuona mwezi .*Faqaala atash-hadu anlaa ilaaha illa Llaah?]* Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akamuuliza Jee wewe wamkubali Mwenyezi Mungu ?.*Faqaala naam.*Akasema ndio.*Qaala atash hadu anna Muhammada rasuulu Llaah?]* Jee wewe wakubali kuwa hakika Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu ?.

Baada ya kujibu tena naam.Qaala faadhin bi nnaasi *an yaswuumu ghadan]* Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akasema Ewe Bilali wape habari watu waje wafunge.

Ni wazi kuwa hadithi hii inafahamisha kuwa Bedui huyu hakuwa mbali na Madina.Kwa sababu jitu la shamba si lazima liwe lakaa mbali.Kwa sababu hakufika siku ya pili wala hakufika usiku mkubwa.Alimkuta Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam bado yuko macho ,yeye na maswahaba zake.Akawataka watu waendelee katika kesho.

Jee katika habari hizi Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akiwa yeye ni kiongozi wa watu;wa waislamu wote ,jee alitoa watu kuwapeleka kwenye miji kama ya Makka na Madina?.Ikiwa ipo hadithi hiyo kuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliwatoa maswahaba fulani na fulani kwenda miji kadha watupe !.

Tunaendelea!. Kwa hadith aliyoitoa muhadhiri aliyetangulia katika .**RAWAAIHULBAYYAAN** tafsiri ayaatil ahkaami minal qur'an jz I, swahifa ya 211

Kama alivyotaja hapo,*alhukmul aashir;Hal yu'utabaru ikhtilaaful mattaali'i fiy ujuubi*

.?*swiyaamu?].J*ee yazingatiwa *ikhtilaaful mattaali'i* katika kulazimu funga

Dhahaba L Hanafiya wal Malikiya wal Hambaliya annahu laa ibrata] Hao wamekwenda wakasema hakuna mazingatiwa kwa kukhitilafiana matlai..*Faidha ra'al hilaala ahlu baladin].*Watakapouona mwezi watu wa mji.*Baladi* kaitaja hapa kwa maana ya *naakira.*

Muhadhiri hapa anaijuwa sana nahau ,na katupa vitu sana.Asema watu wa mji.Mji gani?.*Wajaba swaumu alaa baqiyatil bilaadi]* Italazimu kufunga katika baki ya miji.Hapa kaitaja kwa *maarifa.*Ni miji ipi ?.Hii ni ya ile nchi iliyouona.Pengine nchi ina miji . mitano,sita....Tofauti na kwetu sisi hapa.Pengine sisi hatukuuona

Italazimu baki ya miji iliyobakia wafunge.Kwa tamko lake Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam;*swuumuw li ru'yatih wa afttiruu li ru'yatih]* Fungeni kwa kuonekana kwake na fungueni kwa kuonekana kwake.*Wa huwa khittaabun aamu li jami il umma*].Hili ni .tamko la *aamu.*Sheikh kaifanya ni *maarifa,*hakuifanya ni *naakira*

Ndipo pale Mwenyezi Mungu aliposema; *Nyinyi* ***mmekuwa bora ya Umma*** **waliotolewa** ***watu……(***Al Imran:110). Imekuja *Umma* hakusema *Al umma.*Ina maana ni *jam'u* ;kwa watu wote.Lakini hapa kasema *Lijami'il umma*,kaifanya maarifa kwa maana ni watu .maalum

*Faman ra'ahu minhum] B*asi yeyote atakayeuona miongoni mwao .*Fiy ayyi makaani]* Pahali popote .*Dhaalika ru' yati lahum jamianh]* Hiyo itakuwa ni kuonekana kwao wote.*Wadhahaba Shaafi'iyu]* Amekwenda imamu Shaafi.*Illa annahu yu'utabaru li ahali kullu baladin ru'yatahu*.Kwa hakika huzingatiwa kila watu wa mji. Haitoshelezi .kuonekana katika mji mwengine au katika nchi nyengine

Muhadhiri aliyetangulia ni dhahiri hakuifahamisha hadithi hii.Kwa hadithi hii hii sheikh kaenda kwenye kitabu cha ***BUGHYATUL MUSTARSHIDIINA*** *fiy takhliis fatawi*y kilichotungwa mwaka 1936 ukurasa wa 108. Amesemaje sheikh ?.*Idhaa thabata l-hilaal]* ;Utakapothibiti mwezi *fiy baladin*] katika mji.*Aamal hukmu jamiil buldaan].*Itaenea .hukmu miji yote.*Al latiy tahta hukmul haakim]* Iliyo chini ya hukmu (kadhi) wa pale

Hakusema *qadhil aam*,kasema kadhi wa pale.Kasema *tahta hukmu baladi ru'iya]*.Hata ikifika mbali huko!.Sheikh kasema mbona twafunga kwa kufuata Kigoma na wapi .huko.Ndio!; tuko chini ya hakimu mmoja,itakapolingana matlai

Kaendelea kusema sheikh,*walan yakun lil haakim wilayya]* wala haitakuwa pahali ambapo hakimu hana wilaya,*yajib swaum]* kulazimu kufunga.Haitakuwa kwa hakimu yuko Saudi Arabia,hana wilaya(utawala) hapa.Kwa hivyo hatuwezi kukubali funga yake au amri .yake.Ni lazima hakimu awepo hapa

Kuhusu habari za mbali kabisa!.....*kabla hajaendelea mwenyekiti;sheikh kadhi wa wilaya ya Mkoani akamkatisha kwa kumkumbusha ya kuwa muda wake umebaki dakika 5 :tu.Mwenyewe skh Muhammed Adam akaendelea na mada yake kwa kusema*

Muhadhiri;sheikh pale hakutwambia kitabu hichi kimetungwa lini na ni *ttaba'a* ya ngapi?.Kwa sababu gani?.Kwa sababu vitabu vinavyotungwa kipindi cha siku hizi ,kitabu kile kile lakini wanawajibisha.Kwa mfano kipo kitabu cha **Sahih Muslim**,kaifahamisha hadithi ile kwa kusema *yu'tabaru likuli baladi ru'yatahu*] yazingatiwa kwa kila watu wa mji kuuona kwao.Lakini katika Mukhtasar Sahih Muslim ambapo huyu yeye kanakili .hukumu zake kutoka Sahih Muslim,yeye kabadilisha

Katika hadithi hii hii; ya Kuraib yeye kaipa nguvu kwa kusema watu wafunge kwa kuenea habari ulimwengu mzima.Mwenyewe kajikaza hapa kwa kusema;*Wa fiyhi jawaazi admu badai ishtiya swiyaamu hataa yaraahu L mar'atu binafsihi L-hilaala]*.Imekosekana .kumaliza kwanza kufunga mpaka mtu auone ule mwezi kwa nafsi yake

Laakin an yu'utamadu alaa ru'yati L qaaimu bi muujibi nnaasi] Lakini hutegemewa kuonekana kutoka wasimamiaji wa mambo ya watu.*Ka mufttiyiina wa rijaalu d diyn fiy .ayaamina hadhaa]* Kama mufti atakapotoa habari na watu wa dini katika zama zetu hizi

Ukitazama kitabu hiki kina ttabaa ya 1977.Jee mtunzi aweza kutoa fat'wa kwa ajili ya zama zetu hizi zikakubalika?.Hizi si zama za *ahlu tad win*.Lazima tufuate vitabu .vilivyopita

Kwa hivyo twamuomba muhadhiri kitabu kile atoe ttabaa yake .Halafu aeleze. Kasema vile vile kuwa yakubalika katika vyombo vya habari vya kisasa vitakapoleta habari kuonekana mwezi Saudia au Makka.Kwa sababu Saudia ndiko watu walikomuhifadhi Mtume swalla .llaahu alayhi wa ssallaam ,na Makka ndiko iliko Kaaba, na Kaaba yetu ni moja

Kwa hivyo mwezi ukionekana kule Makka watu wote wafunge.Na ukionekana Madina watu wafunge vile vile.Kwa sababu kule Madina ndiko alikohamia Mtume swalla llaahu .alayhi wa ssallaam.Hii haijakuwa dalili ya kutosheleza,na alete dalili iliyowazi kabisa

Dakika ziko chache zilizobakia lakini napenda kuendelea kwa kusema katika kitabu **Fiqhu Sunna** kwenye ukurasa wa 368.Hiyo hiyo moja aliyoitoa *ikhtilaaful mattalii*;kasema mwenyewe *Innahu lazaalul ikhtilaaful mattaali'i*,halafu kaitoa hadithi yote ya Kuraib ,halafu hapa kasema *wa dhahaba ikrima wal Qaasim* mpaka mwisho*…..innahu yu'tabaru li ahli kulli baladin ru'yatahum]* Hakika huzingatiwa kwa kila watu wa mji wazingatie kuonekana kwao. *Walaa yalzamu ru'yatu ghairihim]* Wala hailazimu kuonekana kwa watu wengineo. Sheikh amekwenda chini tena kusema *wa qaala Tirmidhiyu haadhal hadith .hasan]* amesema Tirmidhiy hadithi hii ni hasan

Lakini asema *wal amalu alaa hadhaal hadith i-nda ahalul ilmi]* Na kuitendea kazi hadithi hii mbele ya watu wa ilimu.*An-na li kulli baladi ru'yatahum].*Hakika kila watu wa mji wana kuuona kwao.Na sheikh kaenda kwenye *IANATU TTAALIBIINA*.Naomba nielezee chapu chapu kwenye ukurasa wa 219,sababu sheikh alichanganyikiwa kidogo.Astahamilie .kidogo

Aliposema skh *wa nabaha Subkiyu]* Hapa ndipo palipomchachiza hasa.Ikiwa dakika .zimeisha naomba munivumilie kidogo ili sheikh Yussuf apate kuelewa

Amefahamisha imamu Subkiy *wataba'a ghairahu;*na wamemfuata watu wengineo.*Alaa yalzamu ru'yatu fiy bilaadi sharqiy ru'yatahum fiy bilaadi gharbiy]* Italazimu kwa kuonekana kwenye nchi za mashariki kufunga kwao kwa kuonekana kwenye nchi za .magharibi.*Min ghair aqsi;*Pasipokwenda kinyume

Kwa vipi ?.Kwa sababu kule Saudia ni mashariki ya mbali kabisa, karibu na magharibi. Huwezi kufuata huku mashariki ya karibu.*Idhi Lailu yad khulu fiy bilaadi sharqiy]* Kwa sababu usiku huingia kwenye nchi za sharqi kwanza.Kwa hivyo sisi huku hata wakitufuata hawapotezi kitu.Kwa sababu wao kule hata ukifika itakuwa ni usiku.Lakini jee sisi .?tukifuata katika nchi nyengine jua litakuwa liko vile

Tuangalie maudhui ya hadithi.Nitaikata kwa kwenda ndani ili kuifahamu hadithi, na sheikh hapo upate kuifahamu.Sheikh ushahidi wake kautoa hapo, ili wewe ufunge kwa .?kufuata nchi za mashariki na usifuate nchi za magharibi.Ushahidi kautoa vipi Asema *Wa annahu laa yalzamu min ru'yatih fiy bilaadi gharbiy bi ru'yati bilaadi sharqiy alaa haadhal hadith Kuraib]* Hakika yake kwa sababu hailazimu kufuata watu wa .mashariki kwa kuonekana magharibi kwa hadithi ile ile ya Kuraib

Kwa sababu gani?.Sheikh asema *Inna Shaama gharbiya bi nisbatil Madina* .Kwa sababu Shamu ni magharibi kwa kulinganisha na Madina.Madina iko wapi?.Iko mashariki!.*Falaa .[yalzamu min ru'yatih fiy Shaam ru'yati fiyhi*

Mwenyekiti wa semina;sheikh kadhi wa wilaya ya Mkoani akamkumbusha skh Mohammed Adam kwamba muda wake umekwisha.Lakini kabla mtoa mada kuondoka kadhi akamtaka ataje maelezo hayo alikuwa akiyatoa kutoka kitabu gani?.Naye akajibu .kwa kusema;**Hii ni Ianatu ttaalibiina juzuu ya 2 ukurasa wa 219**

Huo ukawa mwisho wa hoja za sheikh Mohammed Adam Makame.Mtoa mada kutoka .upande wa Ansaar akakaribishwa aje kujibu hoja hizo

HOJA ZA KIANSAAR SUNNA .
SHEIKH FOUM KOMBO FOUM.

Jina langu ni Foum Kombo Foum.Mzaliwa wa Muwambe Pemba.Nimesoma chuo cha kiislamu na nimesoma Madina kidogo.

Kwa sababu nataka kupinga aliyokuwa akiyasema sheikh Mohammed Adam na ni dhaifu .mno,sitachukua hadithi moja moja aliyoileta yeye.Bali nitaashiria tu ule udhaifu wa hoja

Kasema kuwa sheikh Yussuf hadithi alizokuwa akizitoa alikuwa hazimalizii.Tunapenda kumfahamisha kwamba inafaa afahamu ilmu inayofahamisha namna ya kutoa mawaidha na kutunga vitabu .Katika kutoa mawaidha na kutunga vitabu, unaruhusika kuchukua pahala unapopahitajia,na hilo si kosa.Vitabu vyote vya fiqhi ukivirejea vimetumia namna .hiyo hiyo

Kwa hivyo kama wewe ukiwa ni muhadhiri umesoma fani inayoitwa *Usuulu Da'awa* inayofundisha namna ya kutoa da'awa kwenye hadhara kama hizi, basi uchukue pahala panapohusu tu.Utakapopawacha utakuwa hukufanya dhambi hata, kama ni aya.Kwa sababu .hukupunguza aya kwenye msahafu bali umechukua tu pale panapohusu

Kwa maana hiyo, hoja hiyo aliyoitumia hapo ina udhaifu mkubwa, na haikubaliki kwa mwanachuoni yoyote.Hata vitabu vya imamu Shaafiy utakuta viko hivyo hivyo;hadithi vipande!,aya vipande!.

Jengine kasema 'Jee mawingu huwapo ulimwenguni kote?.Yanaweza yakatanda ulimwengu mzima?.".Jawabu tunamwambia hii ni qudra ya Mwenyezi Mungu.Kutanda au kutokutanda ni suala lake yeye.Linaweza kuwepo au kutokuwepo,usilikisie.Kwa kuendelea .hapa hapa, tunamwambia inawezekana kutanda mawingu ulimwengu mzima

Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema *swuumuuw liru'yatih wa afttiruu liru'yatih]* fungeni kwa kuuona baadhi ya waislamu na sio waislamu wote.Hapa inafahamisha kuwa kuna wengine watakuwa hawajauona huo mwezi.Hawajauona kwa sababu kuna mawingu ulimwengu mzima au hawajauona kwa vile Mwenyezi Mungu tu .hakuwabahatisha ,pamoja na kuwa hakuna mawingu

Fain ghumma] Lakini kama kutakuwa na mawingu,asema *fa akmilul idata thalathiina*] timilizeni hesabu ya thalathini .Kwa hivyo suala la kutanda mawingu na kutotanda ni kama . kuuliza jee mvua yaweza kunyesha au isinyeshe?.Ni suala la Mwenyezi Mungu

Katika kitabu ***Subulu salam*** mwanachuoni anatueleza hivi:*Dhaahirul hadith yadullu alaa annahu yalzamu ru'ya likul li waahid.*] Inalazimu kuuona kwa kila mmoja.*Laakin qaama l ijmaau*] Lakini imesimama ijmau, nayo ni makubaliano ya wanachuoni wote,si wanachuoni wa Tanzania tu ,ni wa ulimwengu wote.*Alaa ujuubi dhaalika*] Si lazima kila .mmoja auwone

Sasa hapa ni kwamba, makubaliano yanaeleza kuwa, si kila mmoja auone.Atakapouona mmoja itabidi wengine wafunge.Ikiwa wamezuiwa ni mawingu au si kwa kuzuiwa ni .mawingu.Ikiwa wamepata habari tu itabidi wafunge

Naendelea na suala lake, maana ya *bilaadi* .Asema maana ya bilaadi ni mji,na katika tafsiri iko kwa maana nyingi.Nakubaliana naye kuwa hili neno lina maana nyingi.Lakini katika .lugha ya kiarabu neno halina maana mpaka pale litakapokaa

Katika aya ya 1 ya surat Albalad (90:1):*Laa uqsimu bi haadhal balad*…,hapa ina maana ya mji.Lakini kwenye aya nyengine itabidi uangalie kama ina maana ya mji au laa.Tuje kwenye hiyo maana ya mji anayokusudia yeye,kwamba kila mji itabidi ufunge kwa kuuona kwake.Hii inatufahamisha kuwa watu wa Chake Chake na vitongoji vyake wafunge kwa kuuona mwezi,watu wa Mkoani na vitongoji vyake wafunge kwa kuuona kwao.Anatufahamisha watu wa Dari salama wafunge kwa kuuona kwao,na haitawalazimu watu wengine.Kwa hali hiyo Tanzania tutakuwa na baladi nyingi sana,ukionekana kwa .pamoja tu ndipo tutafunga pamoja

Ukisoma vizuri hicho kitabu utaona wanachuoni wasema *yalzamu Li jami'il umma]* inalazimu kwa umma wote.Kwa hivyo maana ya bilaadi iliyokusudiwa hapo ni nchi na siyo .mji

Hoja yake nyengine anasema *khittaabu liunaasi makhsusiin]* Maelezo haya ya hadithi yanawahusu watu maalum.Bila shaka anakusudia matlai au nchi.Tunamwambia kwamba *Idhaa jaa naasu alaa umuumih yusta'amalu bi umumih]* Itakapokuja nasu kwa umummi wake hutumika kwa umumi wake.*Hataa idhaa warada alkhusus*.Mpaka itakapopatikana hoja ya khususi.Tupe hoja inayosema ni watu wa mji fulani!.

Huko mbele umesema inawahusu watu wote,lakini kabla sijafika huko,nataka hapa utupe aya na hadithi zinazoonesha ni kwa ajili ya watu fulani tu . Tupe *ijmanh* au *qiyaas* zinazoonesha ni kwa ajili ya watu fulani tu.Kuna *qiyaas daliil* na *qiyaas baattil*,tunataka *qiyaas daliil* inayoonesha hadithi hiyo ilikusudia watu maalum tu.Bila hivyo hoja ya .khusus haisimami pahala pa umuumi

Hoja yake nyengine dhaifu ni ile hadithi inayosema *fittrukum yawma yufttiruuna n-naas]* Kwamba kutoa kwenu zaka ya fitri ni ile siku wanayofuturu watu wote.Hapa bila shaka Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alikusudia kutoa kwenu fitri ni ile siku wanayofuturu watu kwa mara ya kwanza,sio ile siku inayofuatia siku nyengine.Na ni ile .inayotokea Saudi Arabia na nchi nyenginezo

Ushahidi uko wapi?.Hadithi hii hii inaendelea kuonesha kuwa haya maneno yana uhusiano,inasema *wa udhwaahukum yawma yudhwaahy n-naas]* na kuchinja kwenu ni ile siku wanayochinja watu wote,siku ya mwezi kumi,yaani sikukuu ya Idul Adh-ha.Sikukuu .hii inaanzia pale Makka,pale ndipo chimbuko

Kwa sababu sikukuu hii ni baada ya Arafa,mwezi kumi.Ukitwambia ni siku nyengine basi hiyo siyo siku iliyokusudiwa.Ndipo pale Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliposema *wa Arafat kum yawma taquumu nnaasi]* Arafa yenu ni ile siku wanayosimama .watu,nayo ni kule Makka.Tanzania hakuna Arafa

Maneno haya yana uhusiano,kuwa siku wanayosimama watu Makka ndiyo Arafa yenu,siku ya pili yake ndiyo idi yenu al adh-ha,na ile siku ya mwanzo ya idi inayotokea ulimwenguni ndiyo idi yenu munayotoa fitri.Hii ndiyo sababu iliyotufanya tuseme hadithi hii ni ya umumi.Umumi maana yake ni kuwa hadithi inawakusudia watu wote,siyo watu wa pahala .fulani au wa madhehebi fulani

Kasema hadithi ya Ibnu Abbas yathibitisha kuwa watu wafuturu kila mmoja pao kwa kufuata matlai.Huu ni udhaifu wa hoja,kwa sababu yeye mwenyewe kathibitisha kwamba baina ya Makka na Madina hakuna tafauti za matlai,ni nchi moja.Kasema kule wana .kiongozi wao na sisi hapa Tanzania tuna kiongozi wetu,ndio maana tunasubiri hapa kwetu

Tunamjibu kuwa wakati yalipotokea haya kiongozi wa kiislamu alikuwa ni mmoja tu.Kiongozi wa Shaam na Madina alikuwa ni Muawiya.Madina ilikuwa ni sehemu tu ya

nchi ile,mji wake mkuu ulikuwa Shaam kama vile ambavyo Pemba ni sehemu ya Tanzania .mji wake mkuu ni Dar es salaam

Sasa ni kwamba unatwambia kuwa hapa Tanzania kila mmoja awe na kauli yake.Pemba kauli yake na Dar es salaam kauli yao.Laa ukitwambia inalazimika kwa kiongozi basi .Muawiya alikuwa ni raisi wa Shaam alikokuwa na Madina alikokuwa Ibnu Abbas Ikiwa munakubali kuwa habari inayopatikana Morogoro au Dar es salaam na sisi hapa tuifuate basi na habari iliyopatikana Shaam Ibnu Abbas naye ilimpasa aikubali na sio .aikatae.Tunarudia hadithi ni za umumi zinawahusu watu wote
Ilipotokea habari ya mwezi Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam hakuwatoa watu Madina kuwapeleka Makkah au sehemu nyengine.Tunakwambia kuwa Makkah na Madina ilikuwa ni nchi moja.Ikishapatikana habari Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam .alikuwa akitoa tangazo msikitini.Siku hizo ilikuwa hakuna simu

Ukisema ilikuwa atoe mtu na farasi apeleke habari,tunasema Makkah na Madina masaa yao yanalingana.Ikiwa hatuna cha kututhibitishia kuwa hakuwatoa watu kupeleka habari . basi ni bora tukae kimya tu
Jengine kasema; itafunga kati ya miji.Hiyo haiwezi kuwa hoja,kwamba ukionekana mwezi Wete,watafunga Chake Chake na Mkoani au na Unguja, yaani watu wa nchi ile .tu.Hilo haliwezekani

Ikiwa suala ni nchi,mbona mwapokea habari kutoka Mambasa !,na mbona mwazikubali habari kutoka Uganda na hizo sio nchi ile ile?.Lakini kitabu kinatwambia hapa,itabidi nikisome:*waqaala baadhu as haabinaa]* wamesema baadhi ya watu wetu.*taummu ru'ya fiy mawdhiy jaminh ahlil ardh]* Taummu maana yake ni kuenea.Imamu Nawawy asema katika .mwahala mwa watu wote,ulimwengu mzima.Hiyo ardh ni ulimwengu wote

Fa lihaadhaa naquulu innamaa lam ya'amal Ibnu Abbas bikhabari Kuraib,li annahu shahaada] Huo si ushahidi.Ibnu Abbas hakuitumia hadithi ya Kuraibu kabisa kwa sababu huo si ushahidi.Labda kuna sababu nyengine.Huyo ni imamu Nawawy anayetwambia hivyo.

Hii ni sherhe ya **Sahih Muslim** mjaladi wa 4 ukurasa wa 197 iliyoshereheshwa na imamu Nawawy,kitabu kina umri wa miaka 1200.

Halafu anasema ni umma maalum si nchi zote.Hii nimeshaieleza sitaki niirejee,lakini kwa kifupi hadithi ni za umumi,nyinyi tupeni ushahidi wa khususi.Zaidi ya hivyo Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alipokuwa Madina alikuwa akizungumza na swahaba mmoja basi ilikuwa akizungumza na waislamu wote, mpaka ulipokuja ushahidi kuwa jambo hilo lilikuwa likimuhusu swahaba huyo tu.Kwa hivyo *al ibrata lal umumi laisal khususi .salabiy*

Jengine kasema *aamal hukmu lijamiil buldaan*.Hapa umeshajibu mwenyewe,kuwa ukionekana mwezi huwa imeshaenea hukumu kwa nchi zote.*Aama* maana yake ni kuenea,ishaenea kwa nchi zote kama tunavyosema sisi kuwa bilaadu sio miji. Kusema

hivyo tumeashiria kuwa ni udhaifu mkubwa,isipokuwa kwa mwahala maalum .kunakohusikana

Kasema hakimu wa Saudia ni mwingine na huku sisi tuna mwengine!.Mbona mwafuata hakimu wa Kenya?,na kwanini mwafuata uhakimu wa Uganda?.Usionekane Nairobi mukafuata,basi subirini mpaka uonekane Tanzania mufuate hakimu wenu ndipo mufunge .kama kweli hiyo ni hoja..Enyi! hamuna hoja na wala hamukubali

Ameshangaa jee vitabu vinaweza kubadilika?.Kwa kuangalia vitabu vya nyuma na vitabu vya mbele yake.Katolea mfano **Sahih Muslim** na **Mukhtasari Sahih Muslim**.Lazima .ufahamu *mukhtasarul kitaabi wa itmaamul kitaabi*,ni mambo tafauti

Mtu anaweza akatunga kitabu leo na mwengine akaja kesho akakifupisha wala hajafanya kosa na hajabadilisha.Jina la kitabu hapo kushaambiwa kuwa ni **mukhtsar sahih muslim**,huo ni ufupisho,kosa liko wapi?. Watu waliosoma skuli wanafahamu kuwa ufupisho ni maneno mengi ukayapunguza kwa kuweka maneno kidogo yenye .maana,basi!.Kwetu sisi kitabu wala hakijaharibiwa

Hoja nyengine kasema kuwa mtunzi hawezi kutoa fatwa zama hizi.Hilo si sahihi.Ijmanh ya wanachuoni wote inasema kuwa ijmanh inathibiti tangu baada alipokufa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam mpaka kitaposimama kiyama.Ijmanh iliyofanywa wakati wa maswahaba ni sahihi na masheikh wa ulimwengu mzima wakikaa leo wakiamua kitu juu ya .kitu, nayo inaitwa ijmanh na inakubaliwa

Ijtihadi kwa minajili ya ijtihadi inakubaliwa iliyofanywa na maswahaba sawa na ijtihadi inayofanywa na masheikh wa leo.Kitabu kinakubaliwa kilichotungwa wakati wa maswahaba na kitabu kinachotungwa na mwanachuoni wa kileo.Wakati wa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kulikuwa hakujawa na vitabu,Yeye alikuwa akiwaambia tu .maswahaba zake iandikeni Qur'an
Tumepata kusikia kuwa huwezi kutunga kitabu mpaka upitie **Ibn Mahfudh**.Hilo si kweli,ndio maana hata huko kuna vitu vinavyopingana..Kitabu hutungwa tu kwa elimu ya mwanachuoni na ijtihadi yake. Akikosea wengine wanamsahihisha.Tupeni ushahidi .mwengine wa kuonesha kuwa kitabu hakiwezi kutungwa na mwanachuoni wa kileo

Mwenyekiti wa semina,skh kadhi wa wilaya ya Mkoani akamkumbusha mzungumzaji,skh Foum ya kuwa muda wake ulionzia saa 7.57 ulikuwa umekwisha.Skh Foum akaomba ..apatiwe dakika 3 tu ili amalizie majibu yake.Akaendelea

La mwisho la msingi,mlikuwa mukisema kufunga Ramadhani kwa kuonekana mwezi popote haijuzu,ni haramu,ni bidaa na ukadiyani.Lengo letu tupeni kitabu chochote,aya au hadithi na nambari zake kuwa mwezi ukionekana Marekani haijuzu kuufuata au .mutuoneshe kuwa Ramadhani haitathibiti kwa kufuata huko

Wassalaam alaykum warahmatullaah wabarakat-hu.

HOJA ZA BAKWATA.

SKH SALEH MOHAMMED SALEH.

Alhamdulillaahi rabil aalamin wa swalatu was salaam alaa rasuuli Laah wa alaa as haabih ajmaiin.Jina langu ni Saleh Mohammed Saleh mkaazi wa Kengeja Watukufu waislamu,mengi tumeyasikia yaliyozungumzwa na madhumuni ya shughuli yetu ya leo na namna mtoa hoja alivyoeleza hoja yake.Kama tulivyosikia katika kanda chanzo cha shughuli yetu hii ni matatizo ya watu wa Kengeja.Matatizo hayo lazima tusiyasahau, na ni yapi?.

Matatizo hayo yalikuwa haya haya ya mwezi.Baada ya kuangalia watu wa Kengeja ni nani?.Tulijiona waislamu wa Kengeja tuliopo wengi wetu ni waislamu wa madhehebi ya kisuni tunaomfuata imamu Shaafiy.Tunao na ndugu zetu wa kiibadhi.Haidhuru tulikuwa nao ndugu zetu wa kishia kidogo lakini kwa sasa hatunao.

Tukiona jambo lolote lile sisi waislamu wa kisuni;wa imamu Shaafiy, ambalo ni tafauti na maelekezo ya masheikh zetu hao, basi lazima tutake kujua na tuhoji.Kadhalika tukiona kitu ni tafauti na Ibadhi kwa mtu anayejiita ni muibadhi lazima tufanye wasi wasi na tutake kuuliza.Hapo ndipo tulipoanzia.

Twajua wanavyuoni huko walikopita,wacha wanavyuoni hata maswahaba walitafautiana kwa rai.Katika tafauti hizo za rai kwa mujibu wa madhehebi tunazozifuata sisi kuna nyengine zakubalika na nyengine hazikubaliki.Sasa mtu akitwambia rai hii mimi naifuata kwa sababu mimi ni Shaafi lazima tupige *question mark* na tuulize kwanini wakati vitabu vya imamu Shaafi havisemi hivyo?.

Katika mtindo huu uliojitokeza wa watu kuiga iga mambo kulitutia mashaka,na haukuanza leo wala haukuanza Kengeja.Binafsi yangu baada ya kuiona hali hii katika miaka zaidi ya 10 kwa vijana wa Kengeja wenye mwendo huu pale Unguja, nilifanya wasi wasi na nikampelekea barua ndugu yangu mmoja,sifichi ilikuwa ni ya kumkataza Nilimkataza asiache utaratibu ambao wanakubaliana wanavyuoni tunaowafuata.Bahati nzuri, ndugu yangu yule alinileta barua ya sababu zake za kufuata.Kwa bahati ninayo hapa.

Sheikh saleh akaitoa barua hiyo na kuashiria kipande maalum kwa kusema.

Aliniambia katika utafiti alioufanya aligundua kuwa hata marehemu sheikh Abdullah Saleh Farsy naye alifuata mwendo huu,alifuata habari hizi.

Hapo niliona Looh! haya mambo saasa yataka kuja ndani yake ushindani.Niliacha na sikushughulika naye.

Sasa kwa kuwa hapa twazungumzia *fiqhi*,itabidi tuzungumzie mambo ya kisharia na ndio maana itanibidi kidogo nijibu hoja za huyu mwenzetu, ndugu yetu aliyetangulia pale alipomkosoa mtoa hoja wa upande huu, kuwa hatufahamu tafauti ya da'awa na sharia Napenda tufahamieni kwa ukumbi huu kuwa tunachokizungumzia sio da'awa.Ukumbi huu twazungumzia sharia,kwa sababu aya inayozungumzia kufunga ni katika aya za ahkaam siyo aya ya da'awa.***Yaa ayyuha Lladhiina aamanuu kutiba alaykum swiyyaam***…..mpaka mwisho wa aya (2:189).Aya hiyo ni katika **ayatul ahkaam**i,yazungumzia hukumu za kufunga.

Vile vile alimuuliza mtoa hoja hapa, kuwa atoe hoja zinazokubalika kuwa mambo haya ya kuandama mwezi yanahusiana na kikundi maalum.Mimi namjibia hapa kwa niaba yake kwa kuwa hatapata tena nafasi.Khususi hii tuifuatayo sie, wanayoifuata masheikh zetu, wanaifuata khususi kutoka kwa mwenyewe Ibnu Abbas ambaye ni Ibnu ammi yake Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam

Sisi hatuwezi tukawa tuna hoja zaidi kuliko ile.Sasa ikiwa atatoa hoja mtu wa Mkoani,wa Kengeja ,wa Wete au Kichaka ambayo ni tafauti na ya mwenyewe Ibnu Abbas.Hapo itakuwa ni maelezo mengine.Hoja yetu ni kuwa mwenyewe Ibnu Abbas,swahaba anayekubalika alieleza wazi kwa Kuraib kuwa yeye ataendelea na utaratibu ule ule .uliokwishaelezwa,sitapoteza muda kuifafanua tena hadithi

Lakini hoja yetu ni ile ile ya Ibnu Abbas kuwa yeye alimwambia yule mjumbe kuwa mimi nitaendelea na hesabu yangu hii hii.Mtoa hoja aliuliza habari ya Arafa,hii sio mada yetu.Akauliza pia habari ya Uganda na wapi na wapi….Twasema!, katika vitabu vya sharia vinazungumza wazi kuwa zikiwa sawa matlai,kwa hivyo na hii Afrika ya Mashariki ina .matlai zilizo sawa

Halkadhalika kasema kuwa amri ilipokuja Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alisema *swuumuu*, kataja kwa jumla.Twamjibu ya kuwa katika Surat jum'aa Mwenyezi Mungu kasema:***Enyi mlioamini! Ikiadhiniwa sala siku ya Ijumaa ,nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu ,na wacheni biashara .Hayo ni bora kwenu lau .(kama mnajua.(62:9***

Hiyo nayo imekuja kwa jumla vile vile.Jee watu wote duniani waswali sawa sawa?.Wengine waswali Ijumaa wakati wengine waswali magharibi muda ule ule wa Ijumaa.Kwa hivyo kuja jambo kwa jumla haina maana kuwa jambo hilo lizagae ulimwengu mzima!.Katika jumla ile halkadhalika Mwenyezi Mungu kawahutubia watu wote,wanawake wamo,watoto na watumwa wamo.Lakini halafu hao wameambiwa .hawana ulazima wa kuswali Ijumaa

Kwenye aya haikuelezwa hivyo. Imekuja ***Yaa ayyuhaa Lladhiina aamanuu***…..basi!.Jee wanawake si waislamu,watoto wadogo na watumwa si waislamu?.Sio hivyo!,wote hao ni waislamu lakini kuna tafsiri zinazofafanua mambo.Ikiwa mtu hajapitia kwenye mambo ya tafsiri, akayaingia mambo ki pamba mbavu tu, ndipo pale tunapofikia kupelekewa asksari misikitini kukataza watu wasiswali sala za idi.Hayo .hatutaki yatokee tena hapa kwetu Kengeja.Ndio maana tukampelekea kadhi

Kwa kufupisha ili nipate kwenda kwenye jitihadi za maulamaa wetu nitamuanza sheikh Abdullah Saleh Farsy ambaye naye kanaambiwa alikuwa akifuata mtindo huu.Katika kitabu chake alichokiita **Swaumu na maamrisho yake** ukurasa wa 46 asema hivi,*heading* .yake ni **KUFUATA WATU WENGINE KATIKA KUFUNGA**

Akifikia nchi iliyo mbali na nchi aliyokuwapo, akawakuta watu ndio kwanza wanaanza kufunga,au wamo katika kufunga au bado hawajaanza kufunga au wamo katika sikukuu.Lililo juu yake yeye kwa kauli yenye nguvu katika madh-hebi ya kishaafi na madh-hebi nyenginezo,ni kutupa hukumu ya nchi aliyokuwepo na afuate .hukumu ya nchi aliyoingia

Huyo ni skh Abdallah Saleh Al Farsiy-almarhum.Lakini huyu ni mwanachuoni wa karibuni,tumwache.Yeye huyu kayachukua kichwani mwake au kayachukua kwa watu gani?.Aliye na sherh ya ***KASH FATU SAJAA*** afungue ukurasa wa 116 ataona .alipoyachukua hayo

Kitabu kilionekana kuchakaa sana na karatasi zake kuachana,lakini sehemu husika :aliyoiwekea alama kabl, aliipata na kuisoma

…Waidhaa ruiya L-hilaal bi mahhali Laazimaa hukmuhu mahaali kariiban

Mtu na aangalie huko, alipoyachukua skh Abdallah Saleh Farsy,mimi sitaendelea tena huko, kwa sababu muda sina.Nataka kumtetea sheikh wetu anayeambiwa alikuwa akifuata mipango hii.Halkadhalika utakwenda kwenye kitabu kiitwacho **MAWAAHIBU**

SWAMAD,ukurasa wa 71-72 yameelezwa haya haya.Aliyenacho kitabu cha **ANWAARUL MASAALIK** ambacho ni sherh ya **UMDATU SAALIK** afungue ukurasa .wa 119

Mwenyekiti;sheikh kadhi wa wilaya ya Mkoani akamtaka sheikh Saleh afafanue kidogo yaliyoandikwa kwenye kitabu hicho, naye akajibu kwa kusema

Sawa nitafafanua inshaAllah,lakini nilikuwa nahesabu muda,naogopa musije mukanikatia .kabla mambo hayajesha na hata sijafika kwenye Qur'an na Hadith

Kwenye ukurasa huo wa 119 sheikh atwambia ***Fain taqaarabaa aammal hukmu wa illa fa llaa.***Bee hapo ina *alif* kuonesha ni miji miwili.Ikikurubiana miji,pale palipoonekana na **.**pasipoonekana hukmu yake huenea.Isipokurubiana **fa llaa**

Kwa hivyo katika hukumu mimi sitaki nihukumiwe ni hawa watoto.Nataka nyinyi mahakimu munihukumu ikiwa haya niyasemayo ni sahihi au haya wasemayo hawa watoto ndiyo sahihi

Akisema hivyo,akachukua rundo la vitabu alivyoweza kuchukua kwa mkono wake na kuviangusha upande wa meza ya mwenyekiti na wenzake.Halafu akainua kitabu kingine na kuendelea:

Naam!,halkadhaalika twende kwenye **ALYAQUUTIN NAFIIS** ukurasa wa 64,utakutia sheikh kanayasema maneno hayo hayo,kuwa ***wa yuthbitu dukhuulihi alaal umuumi bi ahadi amrain,istikmaali shaabaan thalaathiin yawman wa shawnih in da haakim biru'yati aadil hilaal aw ilmih an bayna mustadih.Wa alaal khusuusi man taraahu ……..aw thubuuti fiy mahhali mutafaqa mattlaa-ahu ma'a mattlainh .mahallahu*]Walioafikiana matlai yao.Hivi ndivyo wanavyotwambia wana wavyuoni

Hapa napitia kidogo katika fiqhi,kwa sababu hii ndiyo hukmu tunayozungumzia,ya kisharia.Zinazungumzwa hapa hadithi na aya za Qur'an.Kabla kuzifikia aya na hadithi hizo .kwanza tujue taratibu za kifiqhi ni zipi katika madh-hebi ya imamu Shaafiy

Katika madh-hebi ya imamu Shaafiy wapo maimamu wanne (4),wawili waliokuja kabla waitwa ***salaf,*** na wawili waliokuja baada ya hao waitwa ***khalaf*** .Imamu Yahya bin Zakariya Annawawiy na imamu Rafii hawa ndio Salaf.Maimamu wanne hao katika madh- ..hebi ya kishaafiy wakiafiqiana kitu hakipingwi tena

Waliokuja baada yao ni imamu Ramli na imamu Ahmad bin Hajjar Al Haitham.Maimamu wawili hawa nao wakiafikiana katika fatwa ya kishaafi huwa jambo hilo halina mushkeli tena.Huo ndio utaratibu unaotumika ,lakini kwa wale wanaosoma .fiqhi!.Kwa wanaosoma lugha utaratibu huo hawataujua

Kwa hali hiyo ikanibidi nitafute angalau kitabu kimoja.Nimekuja na **NIHAAYATUL MUHTAAJ;ILAA SHERH AL MINHAAJ**.Kitabu hiki kimetungwa na sheikh,mmoja kati ya wale wawili wanaokubalika sawa sawa.Huyo ni Mohammed bin Abdul Abbas .Ahmad ibnu Hamza;Ibnu Hishaam.Huyu ndiye yule imamu Ramli

.Huku akiwa amekishikilia kitabu hicho juu kwa mkono wake akaendelea kwa kusema

Huyu katika elimu ya kifiqhi ya madh-hebi ya imamu Shaafiy kaitwa vipi?.Huyu ni ***shahiir bi shaafiy saghiir***].Umashuhuri wake huyu aambiwa huyu ndiye Shaafiy mdogo.Katika utaratibu wa kifiqhi yeye akifutu masuala mengi kinachopewa umuhimu wa .mwanzo *(priority*) ni hiki **NIHAYA,**na ndiyo maana nikaja nacho

Watu wengi ambao sio wasomi wa fiqhi wakitajiwa vitabu hutoka na fikra aah!, lakini viko vitabu.Vitabu vina utaratibu wake.Kitabu hiki sifa yake nyengine ni kuwa ndicho kitabu peke yake walichokutanika wanaachuoni mia nne (400) alipokitunga mwaka 1004

H,sio kama sisi tuliokusanyika leo hapa..Wanachuoni hao walitoka pande mbali mbali .duniani,wakakisahihisha na kikakubaliwa
Leo tukiona mtu ayapinga yaliyomo katika mabwana hawa lazima tuwe na wasiwasi kwa sababu wengine wanaoyapinga ni katika watoto wetu,wengine ni ndugu zetu ,na Mwenyezi Mungu atwambia katika Qur'an ambayo tunayoambiwa tuirudie alipowasifu watu ambao :ni waislamu na wanaofuatwa na watoto wao kuwa
Na wale walioamini na wakafuatwa na vizazi vyao katika imani,Tutawakutanisha nao hao jamaa zao,wala hatutawapunja kitu katika {thawabu za} vitendo vyao;kila mtu .atalipwa kwa kile alichokichuma...AT-TUUR:21
Kwa ufupi ni kwamba watu wenye kuamini na wakafuatwa na watoto wao,katika mambo yao hayo ya dini, basi moja kwa moja Mwenyezi Mungu atawakutanisha peponi.Mzee wa Kengeja akiona kuwa yeye yuwafunga leo kwa nguzo ya nne ya kiislamu,na mtoto wake au nduguye kanafunga jana au juzi,au yeye afunga leo na mwanawe leo afuturu lazima apatwe ni wasiwasi kuwa huyu mwanangu vipi afuata mwendo wangu?.Mwendo huu tuliowakutia hawa masheikh.Sisi wazee wetu ni hawa .masheikh
Sasa kuna hoja moja yenye kutolewa ambayo na mimi naikubali,yenye kusema kuwa ziko hoja nyingi zinazotolewa ya kuwa mwezi ukiandama popote pale ulimwenguni watu .?wafunge.Naam! hiyo iko kweli na wataalamu wazungumza.Lakini ni nani hao
Najibu lile suali kuwa *wengine watutuhumu kuwa sie ni nani,ni nani*……Ndiyo!ni .kweli.Nakileta kitabu hiki hapa
.Akakionesha kitabu kidogo cheupe halafu akasema
Kwanini nikakileta kitabu hiki,kwa sababu hiki ni kitabu cha kishia chaitwa **KITABU CHA SWAUMU**.Aliyekitunga ni Said Mohammed AlMahad Al Musawiy.Huyu ni Shia na .kitabu chote ni cha kishia
Humo kazungumza hivi:***Vile vile ikiwa umethibiti mwezi kwenye mji mmoja kwa watu wa mji wa pili haina faida,isipokuwa mji huo uwe karibu na mji wako au mji mwengine, yaani ufuq al matlai.***Halafu akafafanua kuwa ufuq ni matlai.Sasa hapa nataka .muweke masikio yenu wazi musikie ***Agaakhui haafiki maelezo hayo***
Agaakhui ni mwanachuoni mkubwa wa kishia.Hiki kitabu nilichokileta si cha kisuni,isije ikadhaniwa kuwa ni cha kisuni,kuwa huyu Agaakhui kazuliwa ni masuni wenzake.Kwa hivyo huyu mwanachuoni mkubwa wa kishia hawafiki maelezo hayo.Yeye anavyowafiki ni kuwa mwezi watu wafunge popote utakapoonekana kama hivi watu wanavyofanya.Huu ni .ukurasa wa 49 kwa aliye na shaka
Kwa hivyo wanaokwenda na rai hizi,sisi hatukatai.Lakini wafuata fat-wa ya Agakhui na .wenzake
Kadhi akamkumbusha skh Saleh kuwa kwa mujibu wa muda wake zilikuwa zimebaki .dakika 4 tu.Akaitikia inshaAllah halafu akaendelea
Tukirejea elimu ya musttallahul hadith yasema kuwa tukiambiwa swahaba kasema tumeamrishwa jambo kadha au tumekatazwa jambo kadha, hiyo huwa ni hadith marfu'i.Hiyo huwa ni hadithi isiyo na shaka na yenye kukubalika kwa sababu imeungana na bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam mwenyewe.
Ibnu Abbas ni swahaba,na yeye ndiye aliyesema kuwa ***Hakadhaa amaranaa rasuulu Llaah***.Amri ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam haipingwi,na Mwenyezi Mungu …: katika Qur'an katwambia

Na anachokupeni Mtume chukueni,na anachokukatazeni jiepusheni nacho.Na mcheni .Mwenyezi Mungu .Hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.- 59:7

….: Katika aya nyengine Mwenyezi Mungu katwambia tena

***Basi nawatahadhari wanaokhalifu amri yake ,usije ukawapata msiba au ikawapata .adhabu chungu.* 24:63**

Mtume ndiye aliyeamrisha hivi.Sisi hatukumsikia,sisi si maswahaba.Waliomsikia ni maswahaba.Alimsikia Ibnu Abbas akamfuata na wakamfuata mabwana hawa na wenzao waliotangulia.Na hii ndiyo hali tuliyokuwa nayo kabla ya kuja hawa wajaji wa sasa, wa kutoka nchi mbali mbali wanaotaka kutuletea hapa kwetu mambo ambayo wataka yaingie kwenye vichwa vya watoto wetu.Na yakishaingia katika vichwa vya watoto wetu huwa .hawarudishiki tena

Sisi tunalolitaka wakazi wa Kengeja ni kuwakinga watoto wetu,wale ambao hawajaingia .basi wasiingie.Twajua kuwa wale washaoingia kuwatibu huwa huwapati

Kwa hivyo haya yashazungumzwa ulimwenguni na yatazungumzwa.Masheikh wote .pamoja na mufti wa Makka kashatia saini

Nataka mujue kuwa mwaka huu,Jumapili mwezi uliandama Uturuki na ikawa Uturuki mwezi mosi ni Jumatatu.Mbona Saudi Arabia hawakuifuata Uturuki?.Ikiwa hoja yangu hiyo tu itapingwa basi mimi nitawafuata hawa.Nyinyi munaohukumu ulizeni ulimwenguni, jee haukuandama Jumapili?.Mwaka 1993 tarehe naisahau kidogo, mwezi uliandama Libya .mwanzo,mbona Saudi Arabia hawakuifuata Libya?.Na kadhaalika

Kutokana na ulimwengu ulivyo, nchi zote zilizo mashariki mwezi huandama mwanzo.Japan mwezi huandama mwanzo,mbona Saudi Arabia hawawafuati?.Mambo yashajibiwa ni wana wavyuoni,lililobaki sasa ni vijana wahangaishwa tu.Mimi siwalaumu kwa sababu tabu kubwa ni kusoma.Watu waamini kuwa kusoma lugha labda ndiko .!kusoma,Kusoma lugha ni mbali

Wakati ambapo skh Saleh alikuwa kahamasika sana kutoa hoja zake,mwenyekiti;sheikh kadhi wa wilaya ya Mkoani akamuarifu kuwa muda wake ulikuwa umekwisha.Skh Saleh .akaomba apatiwe dakika 3 zaidi.Akapatiwa dakika 2 na akaendelea

Tukirejea katika Qur'an,nimefurahi sana kwa khutba ya sheikh Yussuf aliyoitoa hapa.Katueleza vile vilivyo, kuwa turejee katika Qur'an.Sasa Qur'an hiyo hiyo baada ya **….**kuirejea ndipo hawa masheikh zetu walipotwambia kuwa

Fas'aluu ahla dhikri in kuntum Laa ta'alamuuna;…..]Basi waulizeni wenye ilimu ikiwa nyinyi hamujui-.Qur.16:43

Haya mambo,ya kuwa mwezi ukiandama wapi tufuate vipi,sisi haya hatuyajui kwa hivyo tuwaulize nani?,ni hadi tuwaulize masheikh zetu.Masheikh zetu ndiwo hao Shaafiy,Nawaawiy na wenzi wao.Washatujibu,mambo yanakwenda safi kabisa ulimwenguni. Kiasi cha miaka 10-15-20 hapa kwetu Afrika Mashariki mambo yalikuwa saafi mpaka baada ya kujiliwa ni hawa wageni walipoleta fikra zao namna hiyo, ndipo .mambo yalipochafuka kiasi hicho

Sisi ahlu dhikri wetu ni wanawavyuoni wetu,na twalazimika kufuata wanavyuoni wetu.Anayewapinga hawa akatoa hoja hizi na zile,jawabu yake kaitoa imamu Maalik bin Anas, katika kitabu chake ambacho nishasikia hapa kikitajwa tajwa.Bora nikisome .muniachie kidogo

Imamu Maalik katika ***Bulughul Maraam*** katwambia katika dibaji yake ***Iyyaakum bi raayyi rijaal]*** Atutahadharisha na rai za watu tu, zenye kuzushwa na akina mimi na wenzangu ***,illa an ajmauu alayhi***;ila watakapokutanika, wakafanya nini?***,watabauu maa***

unzila ilaykum min rabikum wa maa ja'a an nabiyyikum.Wain lam tafhamuu fa salimu li ulamaaikum].;Sikilizeni viruri hapo,Na kama hapatafahamika twende kwa .maulamaa wetu

Sasa sisi tumepata wasi wasi jambo la mwezi, twende wapi?;ni kwa maulamai wetu,sio twende kwenye Jiografi.Mtoa hoja hapa alisema kuwa hapa na Saudia hakuna tafauti ya hata sekunde moja,nikajua huyu mtu hajui Jiografi.Haiwi hapa na Unguja ambapo moja ni nyuzi 5 kusini na 6 kusini (*5degreeSouth and 6degreeSouth*) kuna tafauti ya dakika 1,itakuwa hapa na Saudi Arabia!.Lakini najua fani hii ya Jiografi kaizungumza tu kama hizo nyengine kumbe hajazisoma.Hapa ndipo panapozuka matatizo.Kwa asiyesoma ataona hapa eenhe! panatolewa hoja.Lakini kwa aliyepata chumba cha 10 tu katika Jiografi yake .basi atakubaliana na mie kuwa hiyo si kweli

Naam! Twaendelea,***falaa tujaadiluuhum]*** Imamu Maalik atwambia wala musijadiliane nao hao wanavyuoni wenu.Akaendelea ***fa innal jadla fiy diin min baqai nifaaq]*** Kwani kujadiliana katika dini ni mabaki ya unafiki.***Qaala ibnul Qaasim bal huwa nifaaq kullih]*** Akasema Ibnu Qaasim huyo, kuwa bali huo ni unafiki kamili.Jambo akishasema mwanachuoni unayemkubali ni basi.***Li annal jadlu bil baattil fil haq manh'al ulamaai kal jadlu manh'a rasuul]***Kujadiliana na mwanachuoni kwa batili katika haki ni kama kujadiliana na Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam.Madam kashasema Shaafiy au .Nawawiy sisi tushatosheka hatutaki mjadala tena

Hofu hiyo sisi wengine twaiogopa.Sisi bwana kadhi mara nyingi tulitakiwa mjadala kama huu, lakini tukawa hatutaki.Hapa tumekuja kwa heshima yako na tumefuata wito wako.Mambo yetu sisi Ahlu sunni wal jama'a yapo tayari na ndio maana hata hao waliokufa sina haja nao.Masheikh wakubwa tulionao wana mwendo huo na ndio maana sisi .!twawafuata wao ,mambo kwisha

Tungekuwa twataka mjadala wa haki kweli tusingewakusanya watu namna hii.Tungempelekea mufti wetu tu tukamuuliza ati mwezi ukiandama popote yafaa watu wafunge?,akitujibu ,basi tungetosheka, mambo kwisha!.Lakini hatuwakubali hao,twafuata vichwa vyetu tu visivyokuwa na kitu.Matokeo yake twawapoteza wale wengine wasiojua vyema.Mtu akishasema kiarabu twaona ndio tayari,wale wajua sheria,kumbe kile ni .kiarabu tu

Kwa hivyo sisi hoja zetu zimo kwenye vitabu,kwenye Qur'an,ambayo hiyo hiyo tauliyoambiwa tuirudie.Na sitaki niendelee kutumia muda wenu zaidi.Mwenyezi Mungu .atuwafiqishe katika kheri ***wa jazaakum LLaahu kheir***

HOJA ZA ANSAAR SUNNA.
SKH SALIM MSABAH.

B*aada ya skh Saleh kumaliza hoja zake,msemaji akamkaribisha mchangiaji wa pili wa :upande aliouita wa skh Yussuf,naye akaanza kwa kusema*

Jina langu ni Salim Msabah Mudhwaary.Mzaliwa wa Zanzibar,Unguja na naishi .Zanzibar ;Unguja mjini

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumswalia bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam. Kwa hakika tungependa kumpongeza sana kadhi wa mkoa huu wa Kusini Pemba kwa kuweka kongamano hili,ambapo kwa hakika kama waislamu tungekuwa tunaweka makongamano kama haya katika mambo yetu ya dini, basi mara nyingi tungefikia uamuzi.Au kwa uchache umma wa kiislamu ungeelewa mambo mengi yanayowatatiza.Mwenyezi Mungu amuwafikishe na atuwafikishe na sisi.

Ama kuhusu uchangiaji wa mada na mchangiaji aliyetangulia,mzee wangu;Mwenyezi Mungu atukutanishe kwenye jambo la haki.Katika kuirudi hoja ya mchangiaji wetu hapa,amesema kwamba mazungumzo hayakuwa kwenye masuala ya da'awa,yalikuwa ni kwenye masuala ya sheria.Kwa hivyo sheikh Yussuf alipoisoma hadithi nusu au kipande;hakuimaliza, alikuwa kakosea kwa sababu yuko kwenye mazungumzo ya sheria .siyo mazungumzu ya da'awa,na sheria haisomwi nusu nusu bali husomwa nzima
Jawabu yangu katika kumuelewesha mzee wangu namwambia kitu kimoja. Kitabu cha ***Bidayatul Mujtahid wa nihayatul Muqtasid,*** hiki ni kitabu cha Sharia si kitabu cha da'awa.Huyu bwana mwenye Nihaya kaiandika hadithi kama alivyoisoma sheikh Yussuf,hakuimaliza na pahala ni pa da'awa si pa sheria!.Kwa hivyo ikiwa bwana mwenye ***Bidaya wa Nihaya*** alikosea ni kosa lake,si kosa la sheikh Yussuf.Yeye itakuwa kakosea tu .kama alivyokosea sheikh wake
Ama kwa upande wa aliposema kwa nini sisi tunasema huu mwezi unawahusu baadhi ya watu tu,wakisha kuuona wafuate mji wao au nchi yao.Hii ni kwa hadithi ya Kuraib.Kwa .sababu kataja hadith ya Kuraib nitaiakhirisha mpaka mbele, nitavichanganya pamoja
Mzee wetu kasema,masheikh au maimamu wa kishaafi akina sheikh Nawaawiy, Ramli,ibnu Hajar Al haitham,ibnu Hajar al Askaalaniy,Raafiy na wengineo .aliowataja.Masheikh hawa wakishakubaliana katika jambo hawapingwi
Jawabu!;kwa msimamo wa kiislamu tunavyofahamu sisi hakuna mtu ambaye hapingwi katika kauli yake.Wasiopingwa ni Mwenyezi Mungu tu na Mtume wake Muhammad .swalla llaahu alayhi wa ssallaam,na watakapokubaliana waislamu wote
Kama ilivyokuja katika hadithi ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam : ***aa tajtamiu ummatiy aLaa dhwalaaLa***] au kama ilivyokuja kwenye hadithi nyengine inayotegemewa katika mambo ya *ijmainh,* kwamba na wakikubaliana waislamu wote,au wanazuoni katika tareikh fulani, juu ya jambo.Hawa ndio hawawezi kupingwa.Lakini kwamba wamekubaliana maimamu au wanazuoni wa kishaafiy tu, haina maana kuwa hawawezi .kupingwa.Hili si katika msimamo wa kiislamu
:Sheikh pia kasoma aya katika suratun Nuur
***…Basi nawatahadhari wanaokhalifu amri yake ,usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu.]* 24:63.**
Kasoma na aya nyenginezo zinazoonesha kuwa twaa ni kwa Mwenyezi Mungu tu na Mtume wake,lakini waliobakia wote wanaweza kukosea.
Imamu Malik kasema ***Maa min swaahibil qauli illa yuukhadhu min qaulih wa yurad illa swaahibi haadhal qabri]*** Hakuna mtu mwenye kauli isipokuwa inachukuliwa au inarudishwa ila kauli ya mwenye kaburi hili.Imamu Malik alikuwa akiashiria kaburi la .Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam pale Madina
Mwenyewe imamu Shaafiy rahimahu Llaahu Taala amenukuliwa kwenye kitabu cha **MAJMUI** cha imamu Nawawiy rahimahu Llaahu taala katika ukurasa wa 63 wa juzuu ya kwanza kwa chapa tulizonazo sisi.Kasema imamu Shaafiy; **Idhaa wajad tum fiy kitaabiy khilaafa sunati Rasuuli Laahu swalla Llaahu alayhi wa sallam fakhudhuu min sunati Rasuuli Laah wad-da uu maa qultu]** Mukiona katika maandishi yangu kinyume na sunna ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam basi semeni kwa kufuata sunna ya Mtume .swalla llaahu alayhi wa ssallaam na wacheni hichi nilichokisema
Kwa hivyo inaonesha kauli ya imamu Shaafiy nayo inaweza kuachwa ikithibiti hadithi ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam .Sasa iweje masheikh tu katika madhehebu tu

ya kishaafiy,maimamu wanne wasipingwe.Hili nadhani katika dini wala halipo,labda .sheikh atatusaidia kutuongoza,pengine sisi vijana mengi hatuyajui

Ama kwa upande aliosema hoja tulizozitoa katika aya na hadithi za *umumu* kuhusu suala la mwezi,pale Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliposema: ***Fungeni kwa kuuona mwezi na kuleni kwa kuuona mwezi na ikiwa utafichikana kwenu kamilisheni thalathiini***.Sisi tulisema ni *aamu*; kwa waislamu wote.Yeye alitoa hoja kwa kusoma aya iliyo katika surat Jum'aa; ***Enyi mlioamini! Ikiadhiniwa sala siku ya Ijumaa ,nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu ,na wacheni biashara .Hayo ni bora kwenu .(lau kama mnajua] 62:9***

Hii ni kwamba sala ya Ijumaa imefaradhishwa kwa waislamu wote;***Yaa ayyuhaa Lladhiina aamanuu]*** *Enyi mulioaimin*….na mara nyingi Qur'an imezungumza kwa kauli hii.Wanaingia wanawake,wanaume,wakubwa,.. wadogo.Wanahusika watumwa na waliokuwa huru. Akasema lakini mbona hawa wengine mfano wanawake si lazima kwao .kuswali Ijumaa?.Mtoto mdogo si sala ya Ijumaa tu,hata huko kuswali tu, kwake si lazima Alichotaka kusema hapa ni kuwa ikija *khittabu* ya *umumi* si lazima iwahusu watu wote,wengine huwa wanavuliwa.Tunamwambia ya kuwa, hao wanaovuliwa huvuliwa kwa hoja,kama vile samaki baharini wanavyovuliwa kwa mshipi na nyavu.Bila nyavu na mshipi huvui!.Sasa tupe nyavu na mshipi vilivyovua kuwa suala la mwezi litawahusu baadhi ya watu tu na wengine hauwahusu. Ukitupa nyavu na mshipi,sisi tuko pamoja na .wewe.Maadhali hukutupa vitu hivyo,tunakuwacha

Kwa sala ya Ijumaa, tunakwambia na wengine nyote, turudi kwenye vitabu vya hadithi.Ziko hadithi zinazoonesha mwanamke si lazima kwake kuswali sala ya Ijumaa,na kwa mtoto mdogo si lazima kwake kuswali.Haya mambo hayataki dalili,kila mtu anayajuwa,yamo kwenye vitabu vya fiqhi na hadithi.Kwa hivyo ziko dalili za kuyavua .?hayo.Sasa dalili za kuyavua haya masuala ya mwezi ziko wapi

Kuhusu tukio la sheikh Abdallah Saleh Farsy, napenda kuwaambia wote waliohudhuria pamoja na waheshimiwa waliopo, kuwa katika hoja za muhadhiri hakutajwa sheikh Abdullah Saleh wala halikutajwa suala lake.Nadhani na katika mzozo wa Kengeja pia suala hilo halikutajwa.Ikiwa yeye amelileta kwa mujibu wa barua aliyopelekeana yeye na mwanawe,basi hoja alizokuwa akizitoa alikuwa anamjibu mwanawe hukoo,lakini alikuwa hazungumzi na hadhara hii.Laa ikiwa amelileta kwa njia ya faida tu,basi sijui iwapo ilitolewa nafasi ya kuleta faida za nje au kuchangia mada iliyozungumzwa tu.Hili .twamuachia muheshimiwa kadhi

Kwa upande wa kauli yetu kwamba mwezi ukionekana upande mmoja ulimwenguni,basi funga itaswihi kwa upande mwengine wowote ulimwenguni.Anasema hii ni kauli yeye aliyoiona kwenye kitabu cha kishia, huku haiko.Kwa hivyo sisi msimamo huu tumeuchukua kwa mashia.Tunamwambia!,ikiwa yeye msimamo huu kauona kwa mashia,jee tukimthibitishia kutoka vitabu vyengine visivyokuwa vya kishia,yaani vya kisuni, kumuonesha kuwa msimamo huu hata huku uko ,atakubali kuwa hatukuyachukua hayo kwa mashia tu?.Bali tumeuchukua msimamo huu na kwa hawa hawa wanazuoni wa .kisuni

Akikubali hivyo,tunamwambia jee mwenye **Fiqhu Sunna** ni Shia ?.**Majmu'u** ya Nawawiy, jee huyu naye ni Shia?.Kwenye sherh ya **Sahih Muslim** ya imamu Nawawiy kasema;**Waqaala** ***baadhu ashaabinaa idhaa ra'aw ahlul baladi alhilaala, taummu ru'yatu Li jami'i ahlil ardhi.]***……**Kwa watu wote wa ardhi**,na ardhi ni dunia,sio ile nchi

moja.Sasa jee huyu imamu Nawawiy ni shia?.Mzee wangu!,msimamo huu haukuchukuliwa .kwa mashia.Umechukuliwa kwa akina imamu Nawawiy,na hao ni magogo wa kishaafiy
Kama alivyosema skh Yussuf Hamza,kwamba yeye anaendelea kumfuata imamu Shaafiy,na sisi sote tutaendelea kumuheshimu na kumfuata imamu Shaafiy kwa yale yote ya haki na tutamuacha pale alipokwenda upande.Yeye ni binadamu anakosea, na kila mtu anakosea.Kusema anakosea si kwamba tunamvunjia heshima,laa!. Yeye ni mwalimu wetu.Mimi binafsi naona haya kusema imamu kakosea ,lakini hakuna budi, hasa kwenye .hadhara za watu wengi
Ukisema imamu kakosea kwa watu wengi hujenga fikra kuwa umemkosea heshima .imamu.Hatupendi,lakini mtu utafanyaje,lisilobudi hutendwa.Kata pua uunge wajihi
Kuhusu kwamba sisi na Saudia tunatafautiana kwa *mattaali'i*,kutafautiana kwa *khuttuutu ttuuli*,yaani tunatafautiana kwa *longitude*.Sheikh Yussuf alipozungumzia suala hili,hakutaja *general* Saudia,isipokuwa alitaja makhsusi Makka.Alisema yeye katika safari yake alifika .Makka
Imetokea mara nyingi hasa hapa na Makka kuwa tuko sawa sawa kidakika.Hakusema Saudia nzima ndiyo tuko sawa kidakika.Hili suala liko wazi,hata Tanzania tunatafautiana kidakika katika kuzama na kuchomoza jua.Hili linakubalika kwa wote.na hili la dakika silo lililozungumziwa.Kwa sababu suala la dakika linahusiana na kuzama na kuchomoza jua.Sisi tunazungumzia suala la swaumu ambalo linahusiana na kuonekana mwezi na .kutokuonekana mwezi.Haya ni mambo mawili tofauti, hatuwezi kuyachanganya
Siku ina masaa 24 ambazo ni dakika chungu nzima.Tunapozungumzia tafauti ya masaa si sawa na kuzungumzia tafauti ya masiku.Ulimwengu mzima siku ni moja tu,lakini masaa ni tafauti.Sheikh Yussuf hakuzungumzia kabisa kuwa Saudia na hapa ni sawa sawa,tuondoe pupa.Alichozungumza ni kuwa Makka na hapa nyakati zetu ni sawa,hii ni kwa sababu .tupo kwenye mstari mmoja
Ama pale aliposema kuwa tumekatazwa kufanya mjadala katika mambo ya dini,khususan kuwauliza wanazuoni,na kwamba hilo ni katika unafiki.Kwa kweli maelezo yake ikiwa ni sahihi basi hayakukaa mahala pake.Kwa sababu sote tuliokaa hapa tupo katika kujadiliana ingawa kwa nia nzuri.Kwa maana hiyo sote sisi ni wanafiki.Hasha Lillaahi!, sio .hivyo.Naamini katika sisi hakuna mnafiki
Mwenyezi Mungu kasema :***Enyi mlioamini!Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu,walio katika nyie (waislamu wenzenu).Na kama mkikhitilafiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume ,ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.Hiyo ndiyo .kheri,nayo ina matokeo bora kabisa.- 4:59.***Hapo sioni kuwa kuna kosa
Sasa kuhusu hadithi ya Kuraibu.Mimi sitorudia kuieleza kwa kiarabu.Lakini sheikh Yussuf kasema kuwa,mpaka Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam anaondoka duniani ilikuwa kisa hiki cha Ibnu Abbas na Kuraib, ilikuwa bado hakijatokea.Mpaka makhalifa wanne waongofu wameondoka ulimwenguni kisa hiki kilikuwa bado hakijatokea.Sayyidna Abubakar,Omar,Uthman na Ali **radhiaLlaahu anhum ajmaiin** mpaka wameondoka .duniani kisa cha Muawiya,Ibnu Abbas na Kuraib kilikuwa bado hakijatokea
Kwa maana hiyo *fatwa* hii ya kila mtu na mwezi wake, kama kweli imetolewa,basi imetolewa na Ibnu Abbas,na Ibnu Abbas naye hakuitoa fatwa hii mpaka baada ya kufa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam na maswahaba wanne.Hivyo tujue *fatwa* hii asili .yake hasa, ni pale Ibnu Abbas alipojiwa na Kuraib kutoka Shaam

Kwanza ina maana kuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam hakutoa fatwa ya kuwa kila mmoja na mwezi wake. Maneno yake ni yale yale kuwa ukionekana mwezi watu wafunge na ukionekana watu wale;ni kwa waislamu wote.Hii ndiyo hadithi ambayo haina mushkeli wowote na ndiyo ambayo itakuwa na nguvu ki istidlaali kuliko hiyo hadithi .(aliyoitegemea Ibnu Abbas (r.a

Ama pale aliposema katika hukumu za *mustwalahul hadithi* kuwa hadithi hii ni ***marfu'u***.Tunakubali ni kweli swahaba akisema ***amaranaa,umirnaa*** au ***nuhiinaa*****,**hadithi inakuwa ***marfu'u hukman***,yaani imeinuliwa kihukumu kupelekwa kwa Mtume swalla .llaahu alayhi wa ssallaam

Pamoja na hivyo tunamwambia sheikh wetu,kuwa tukirudi kwenye fani ya mustwalahul hadith,kuna ***marfu'u swarahatan*** na ***marfu'u hukman***.Kuna hadithi imerufaishwa moja kwa moja kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam.Hizi ni zile swahaba anaposema ***sami'itu rasuulu llaahi swlala llaahu alayhi wa sallam*** au ***qaala swalla llaahu alayhi wa ssallam***.Kwa maana nimemsikia Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam . au Mtume ..swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema kadha

Na pale swahaba anaposema tumeamrishwa au Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam .ametuamrisha, hii ndiyo ***marfu'u hukman*** kama alivyosema mwenyewe hapa Sasa nataka kuweka sawa.Inapotokezea kutokuelewana au unapotokezea mgongano.kati ya hadithi mbili,moja imenasibishwa na Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam moja kwa moja;***marfu'u swarahatan*** na nyengine imenasibishwa kwa njia hiyo,kuwa tumeamrishwa,yaani ***marfu'u hukman***.Katika hali kama hii basi hadithi yenye nguvu ni **.**ile iliyosogezwa kwake moja kwa moja;***marfu'u swarahatan***

Kwa hili la mwezi hadithi zote ni zile zilizosogezwa kwake moja kwa moja;yaani ***marfu'u swarahatan***.Mfano ***swuumuw liru'yatih wa afttiruw liru'yatih fa in ghumma alaykum fa akmiluu iddata thalathiin]*** Fungeni kwa kuuona mwezi na fungueni kwa kuuona,na pindi yakitanda mawingu juu yenu kamilisheni hesabu ya siku thalathini.Hadithi hizi ni moja kwa moja kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam .Ama zile zinalenga tu .kuwa tumeamrishwa

Inawezekana kweli ndivyo alivyowaamrisha Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam ,au pengine ndivyo alivyofahamu tu Ibnu Abbas juu ya kuamrishwa.Sasa hadithi isiyokuwa na mushkeli na yenye nguvu kiistidlaali ni hii iliyonasibishwa na Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam moja kwa moja,**Fungeni kwa kuuona na kuleni kwa kuuona…..** kuliko ile .iliyotegemewa na Ibnu Abbas katika dalili.Hadithi hii ndiyo ya kushikwa

Hata hivyo tumuangalie tena yeye Ibnu Abbas, aliposema ***Ha kadhaa amaranaa rasuulu Llaahi swalla llaahu alayhi wa sallam]*** Hivi ndivyo alivyotuamrisha Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam.Hapa pana suali mwanafunzi yeyote anaweza kuuliza.Wewe pia ukija leo ukaniambia Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema wakati wa kuswali funga mikono penye kifua,au chini ya kifua au penye kitovu.Mimi nitakuwa na haki ya kukuuliza wapi Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliposema hivyo.Sasa hapa imekuja tu kuwa Ibnu Abbas kasema ***Hivi ndivyo tulivyoamrishwa na*** ***. Mtume*** **swalla llaahu alayhi wa ssallaam**

Suali linakuja,waapi Ibnu Abbas ameamrishwa na Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam,au wapi Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam ametuamrisha sisi waislamu?.Ilivyokuwa hatuna wa kumuuliza,Ibnu Abbas amekwisha kufa,na ilivyokuwa Kuraib naye alipoona mwalimu wake keshasema vile ***ha kadhaa amaranaa….*****.**,akamuheshimu mwalilmu wake,akashindwa kumuuliza.Wale wanaotetea

msimamo huu ,kuwa kila mmoja afunge kwa kufuata mwezi wake,tunawauliza;ni wapi .? Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliposema
Ikiwa jawabu hatuna,basi itakuwa Ibnu Abbas kasema maneno bila kuyafafanua.Ilivyokuwa hakufafanua,sisi tutamuwacha Ibnu Abbas na msimamo wake .mpaka siku ya kiyama ,naye inshaAllah atakuwa yuko katika haki
Kwa upande mwengine hadithi ya bedui ambayo mwenye ***Bulughul Maraami*** kaieleza na hata sheikh kaitaja hapa.Hata katika vitabu vyengine ambavyo sisi tunavifahamu imetajwa vile vile. Hii ni hadithi ya bedui aliyekuja kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akamwambia kuwa mimi nimeuona mwezi.Mtume swalla llaahu alayhi wa .ssallaam akamuuliza jee unashuhudia?,akatoa shahada mbili
Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akaukubali mwezi ule, akamwambia Bilal awatangazie watu wafunge.Hadithi hii kaipokea mwenyewe Ibnu Abbas,angalieni vizuri hapo.Yaani Ibnu Abbas kapokea hadithi kutoka kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kuwa Bedui alikuja kwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akasema kuwa kauona mwezi na Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akaukubali mwezi huo, bila kumuuliza bedui pahala alipotokea wala masafa yake.Hakumuuliza ikiwa alitoka Shaam .au pahala gani pengine
Kweli inayumkini kuwa alikuwa akitoka pahala pa karibu,lakini inayumkini pia kuwa alikuwa akitoka pahala pa mbali.Muhimu ni kuwa yeye hakumuuliza anapotokea.Kwani ikiwa hivyo inakuawaje?.Watu wa ***usuulul fiqhi*** wanasema Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam anapokuwa hajauliza suali pahala ambapo inayumkini kuuliza ni***;tarkul istifswaari fiy makaanil ihtimaali yuujibul umuuma fil baqaali]*** Ikiwa Mtume atawacha kuuliza pahala ambapo inayumkini alikuwa aulize.Basi inaonesha hii hukmu ni *aam*,haina mipaka.Ukipenda kaangalie kwenye ***AL IHKAAM FIL AHKAAM LIL ANBIY*** ,jz 2 **.**,mlango wa Al ***Umuumu wal khusuusi***
Ilivyokuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam hakuuliza anatoka wapi,basi kwa mujibu wa ***usuulul fiqh*****,** inaonesha ni popote anapotoka mtu.Hii kaipokea mwenyewe Ibnu Abbas.Sasa ikiwa Ibnu Abbas kapokea maneno kuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alipokea habari kutoka kwa bedui kuwa kauona mwezi na wala asimuulize pahala alipotokea.Halafu Ibnu Abbas huyo akapokea habari kutoka kwa Kuraib,akasema anatoka Shaam na wameuona mwezi Shaam,naye Ibnu Abbas akaukataa.Hapa itakuwa kitendo cha Ibnu Abbas kimetafautiana na yale ambayo yeye ameyapokea kutoka kwa .Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam
Watu wa ***mustwalahatul hadith*** wanasema swahaba akipokea hadithi,lakini akatenda kinyume na alivyopokea ,basi ***al ibratu fiy maa rawaahu***.Kinachoangaliwa ni kile alichopokea sio vile alivyotenda.Ushahidi ni Abu Hurayra kama ilivyokuja katika .***Muwatta*** ya imamu Malik
Abu Hurayra (r.a) katika masuala ya mbwa anapotia mdomo wake katika chombo cha mmoja wenu, anasema basi akioshe chombo hicho mara saba,na mara moja wapo akioshe kwa mchanga.Hivyo ndivyo alivyopokea Abu Hurayra.Lakini kama ilivyo kwenye Muwatta kupitia kwa mkwewe Saalim ibn Muswayab ,kuwa yeye Abu Hurayra .alishuhudiwa akikosha mara tatu tu
Rai ya maimamu na wanazuoni ni kukikosha mara saba na sio mara tatu.Wameona bora wafuate vile alivyopokea Abu Hurayra na sio vile alivyofanya.Kwa sababu .binadamu!,anaweza akapitiwa kwa kusahau,akafanya kitu tafauti na vile alivyofahamu

Kwa hivyo Ibnu Abbas ikiwa kaukataa mwezi wa Shaam,wa Kuraib na huku yeye kapokea kuwa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliukubali mwezi wa bedui bila kumuuliza alipotokea.Hii inaonesha tufuate yale aliyopokea Ibnu Abbas,kuwa tufuate mwezi kutoka popote.Tuangalie tu aliyeleta habari hizo ni muislamu?.Iwe katokea .Saudia,katokea Ulaya au popote pale.Ilimradi tu anashuhudia shahada mbili
Kile kitendo cha Ibnu Abbas tumuwachie mwenyewe.Kama vile ambavyo Abu Hurayra .kaachiwa mwenyewe kitendo chake na kufuatawa yale aliyopokea
Kabla sijamaliza nakumbusha tu kuwa wachangiaji waliotangulia sikuona kuchangia kwenye tafsiri ya Qur'an, juu ya ile aya ***Faman shahida minkumus-shahara falyaswumhu-(2:185).*** Sheikh Yussuf kasisitiza sana kuwa ***faman shahida*** maana yake ni .?atakayeuhudhuria,sio atakayeuona.Jee hii maana yake ni kuwa tumeridhika na tafsir hiyo Mpaka hapa nataraji na mimi itakuwa nimechangia vya kutosha.Wassalaam alaykum .warahmatu Llaah

HOJA ZA BAKWATA.
Skh ALI ABDALLAH AWESI.

B*ismillaahir Rahmaanir Rahiim.Alhamdulillaahi Rabbil aalamiin,wa swalatu wassalaalm .alaa sayyidina Muhammad wa alaa aalih wa swahaabih wa ssallam. Amma ba'du*
Mimi hapa ni Ali Abdallah Awesi,natoka Mtambile.Mimi sijasoma chuo chochote .isipokuwa kwa masheikh zangu hawa munaowaona hapa
Nasimama kuchangia hoja ya kuwa hapana ruhusa kufunga mwezi wa Ramadhani .uandamapo Saudia au kwengine mpaka na sisi hapa utuhudhurie au tuuhudhurie
Hoja hii naungana na maalim Yussuf alipoisoma aya ya Qur'an katika suratul Baqara,aya ya 185.Siisomi aya yote ila nitasoma pale tulipo na haja napo sasa hivi.***Qaala Llaahu taala]*** Amesema Mwenyezi Mungu aliyetukuka:***Faman shahida minkumush-Shahra fal-yasumh .***
Kijana pale aliuliza mbona haijasemwa au ndiyo tumeridhika nayo.Ndiyo!,tafsiri ya maalim Yussuf ni nzuri sana kuwa **Hadhwara** ina maana ya **Shahida,**na akatia nahau nyingi sana. Lakini alisahau kusema katika ***Faman*** neno ***man*** **ni** *harfu jaari wa .tabyiid.*Mwenyezi Mungu kasema basi atakayeuhudhuria katika nyinyi waislamu afunge Siyo mwezi ulioandama huko, haujaindama hapa Kengeja wala haujatuhudhuria ,halafu .!aamrishwa mtu hapa na kwengine afunge.**NO**
Mimi sitakwenda ndani sana.Kijana wa Muwambe alikuwa asema ataka apate aya ya kuwa mtu afunge kwa mwezi.Aya ni hii,isome na izingatie vizuri.Mwezi ati waindama .huko hapa bado haujatuhudhuria, halafu mtu afunge.Hapo bado kabisa
Tumuangalie sheikh Ibnu Kathiir,sahifa ya 186 jz ya 1 kwa hichi changu mie.Katika kuifasiri aya hii asema;***Haadha ijaabu laaziman]***Aya inayokuja hapo asema ni wajibu wa .lazima.Ndugu zangu mie sijakuwa fundi sana wa irabu,nikikosea nijazieni sio municheke Kufunga ni wajibu wa lazima ***alaa man shahida istihlaalan shahra]*** kwa yule aliyeuhudhuria mwandamo wa mwezi.Siyo mwezi uindame huko halafu umuamrishe .mwezako afunge hapa.Hapana
A*yyi kaana muqiiman fil baladi.]* Kuhudhuria kwake huyo ni kuwa ni mkaazi katika mji.***Hiina dakhala shahru Ramadhan]*** Wakati ukiingia mwezi wa Ramadhani.Hapo .!ndipo afunge.Si hivyo hapana kufunga,ngoja uuone ndipo ufunge

Sheikh Ibnu Kathiir asema ***wa huwa swahiihu fiy badanih*]** na hali ya kuwa awe *ni* mzima kwenye mwili wake.Ikiwa utaingia mwezi na yeye yupo kwenye mji ule, lakini hajiwezi kwa ukongwe.Mpikieni. Hatutaji habari ya kutoa fidia,twataka habari ya kufunga .kwanza

Tumuulize Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam ,tusikie asemaje kuhusu aya hii.Isikilize vizuri hadithi hii,uizingatie na uifanyie kazi.***Ani Abu Hurayra,ani Nabiya swala llaahu alayhi wa sallam qaala*** Kutoka kwa Abu Hurayra alimsikia Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akisema;***Swuumuu li ru'yatih wa afttiruu li ru'yatih]*** Fungeni kwa kuonekana mwezi (kama alivyofasiri skh Yussuf),na futuruni au kuleni kwa kuonekana mwezi.Wengine watasema mbona yarudiwa hiyo hiyo.Ndivyo alivyosema .!Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam

Hadithi ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam wenzangu haijesha hapo.Asema ***Fain ghumma alaykum]*** Na kama kikija kiwingu juu yenu kikauficha mwezi**.*** ***Fa akmiluu .idda Shaabana thalathiin]*.** *Kamilisheni hesabu ya Shaabani siku thalathini*

Bwana mmoja (mshairi) asema Wa ***arsalal anbiyaa ka mustafaana.Yudrikuh bi swidik wa tabligh wal amaana***].*Wameletwa mitume wenye utambuzi, ukweli na uadilifu wa kufikisha ujumbe*.Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alikwishajua kuwa kuna miji itazibwa ni kiwingu,mwezi wawe hawauoni,ndipo watatumia ***Fain ghumma***

Mwenyezi Mungu atwambia katika Qur'an 2:208

Enyi wale mlioamini!,Ingieni katika hukumu za Uislamu zote,wala msifuate nyayo za .shetani.Kwa hakika yeye kwenu ni adui aliye dhahiri

Usiitoe hadithi nusu,isome yote waislamu waisikie vipi Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam alisema.Usichukue upapendapo tu kwa kutaka watu wafuate hoja zako ilhali hadithi haijakwisha. ***Fain ghumma***] na kiwingu kikitanda juu yenu…Hadithi hiyo wameipokea Bukhari na Muslim.

Mimi jamani sina vitabu vingi,kwa sababu vitabu vyataka pesa na mie ni mnyonge wa pesa,sina.Lakini Qur'an ipo.Turudi kwenye **Fiqhu Sunna**,tuangalie alivyofasiri aya kwenye sahifa ya 404 kwa kile changu.Hapo pametajwa ***jamhuur*,**ya kwamba pale pana maneno ya masheikh waliokubaliana yaliyompendezea kwa habari yake, ya kutaka watu .wafunge kwa kuandama kule.Lakini wallaahi palipompinga hakupasema

Maneno yaliyopo pale hakuyataka yeye,lakini mimi nitayasoma muyasikie.Angalieni kwenye hiyo hiyo **Fiqhu Sunna** ikiwa zitalingana zenu na yangu,lakini yangu sikuichukua.Baada ya **jamhuur** kusema hii aya ni aamu,ya watu wote wafunge na hadithi, .pana maneno juu ya ***ikhtilaafu almattaali'i***

Haya hakuyasema,yasikilizeni.***Wadhahaba Akramatu wa Kaasim ibnu Muhammad wa Saalim wa Ishaaqu wa swahiihu indal Ahnaafi wa anil mukhtaaru inda Shaafi'iy]*** Mabwana Akrama na Kassim ibn Muhammad na skh Salim na Is-haaka na sahihi mbele ya mabwana wa Hanafi wameyakubali hayo.Pamoja na mambo yaliyoteuliwa na yaliyo mazuri kabisa kutoka kwa bwana Shaafy.***Li annahu yu'utabaru li kulli baladin .ru'yatahu]*** Hakika pana kila mji na kuuona kwao

Vijana wakubwa kwa wadogo tusomeni dini yetu, tusidanganywe.Mtu akija akikusomea kipande utajuwa pale keshapawacha, hudanganywi!.Hadithi inaendelea ***wala yalzamuhu ru'yatu ghairuhum***.] *Wala haitawalazimu watu hao mwezi wa kuonekana Uchina*. Mwezi .?huo hautuhusu sie!.Kwanini ikasemwa hivyo

Hadithi ya Kuraibu ishazungumzwa sana leo,ila na mimi nairudia tena,kwa kuwa ni hadithi nzuri mno,haidhuru yapinduliwa pinduliwa.***Bimaa rawaahu min Kuraib]*** Kwa lile

lililopokelewa kutoka kwa Kuraib.***Ataitu ilaa Shaami wastahala alaiya al hilaala lailatal jum'aa wa anaa bi Shaami]***.*Nilikwenda Shaamu na mwezi ukaniandamia na mimi nikiwa kijiji cha Shaamu usiku wakuamkia Ijumaa*.Ni mwezi gani huo?,sio wa Shaaban,ulikuwa ni .wa Ramadhani

Thumma qadamtu ilaa Madina fiy aakhiri shahar. Kisha nikaelekea Madina mwishoni mwa mwezi.**Fasaalaniy Ibnu Abbas**] *Akaniuliza Ibnu Abbas*.Huyu ni mwanamme huyu.Sayyidna Omar alikuwa akimchukua kwenye hafla zake,maswahaba wakamwambia vipi wewe wamchukua huyu,sisi hatumchukui.Akawaambia huyu si mtoto .wa kuchezea.Sikukusudia kutoa yote hayo,lakini huyu ni mwanamme fatwa zake tutumie Katika kuniuliza kwake asema Kuraib **Fadhakara anil hilaala**] *Akaniuliza kuhusiana na mwezi*.**Mataa ra'aitum alhilaala?]** ***Ny****inyi muliuona lini mwezi?*.**Faqultu ra'ainaahu lailatal jum'aa]** Nikamjibu sisi tuliuona usiku wa kuamkia Ijumaa.**Faqaala anta? ra'aitahu ?].A**kaniuliza jee wewe uliuona?.**Faqultu naam,wa ra'aahu nnaasa waswaamuu waswaama Muawiya].*****N****ikamwambia ndio nimeuona,na watu waliuona wakafunga na akafunga Muawiya*.**Faqaala lakinnaa ra'ainahu lailata sabt].*****B****wana Ibnu .Abbas akasema lakini sisi tuliuona usiku wa kuamkia Jumamosi*

Sikiliza fatwa za Ibnu Abbas aliposema **Falaa nazaalu naswuumuu hataa nukmila thalathiina au naraahu]** *Hatutaacha kufunga sisi kwa kuuona kwenu huko, mpaka tukamilishe siku thalathiini za Shaabani au tuuone*.Na kweli walifanya hivyo mpaka walipokamilisha thalathini.**Faqultu alaa taktafiy bi ru'ayatu Muawiya wa swiyaamih?]** *Jee hutosheki kwa kuonekana kwake na Muawiya na kufunga kwake?*.**Faqaala Laa! hakadhaa amaranaa Rasuulu Llaah swallallaahu alayhi wa ssallam]** *Akasema bwana Muawiya Laa! Sitosheki .Hivi ndivyo alivyotuamrisha bwana Mtume rehema na amani .zimshukie*

Alivyoamrisha Mtume ni vipi?.Ni hivi ***Swuumuu li ru'yatih wa afttiruu li ru'yatih]*** Fungeni kwa kuonekana mwezi ,na futuruni au kuleni kwa kuonekana mwezi. ***Fain ghumma alaykum Fa akmiluu iddata Shaabana thalathiin]*** *Na kama kikija kiwingu .juu yenu kikauficha mwezi****.****Kamilisheni hesabu ya Shaabani siku thalathini*

Ikiwa hamjui alivyotuamrisha Mtume basi ni hivyo.Na ndivyo alivyotuamrisha Mtume .swalla llaahu alayhi wa ssallaam

Rawaahu Ahmad wa Muslim wa Tirmidhiyu,wa qaala Tirmidhiyu hadhaa swahiihu, hasan] Mabwana waliopokea hadithi hii ni bwana Muslim,bwana Ahmad na bwana Tirmidhiyu.Lakini wallaahi vitabu hivyo mie sina,ukiniambia nipa Tirmidhiy .sinayo.Naviona humo humo kwenye Fiqhu Sunna.Lakini ukitaka utaona ,watu wanavyo Tirmidhiy asema **wal amalu alaa hadhal hadith in-da ahlil ilmi anna likulli baladi ru'ayatahu]** ***K****uifanyia kazi hadithi hii kwa watu wa ilmu ni kuwa kila watu wana maoni .yao*.Kwa hivyo tusomeni ndugu zangu

Kwenye **MUGHNIY ALMUHTAAJ** ukurasa wa 422 kuna hadithi ya Ibnu Abbas alipomuamrisha Kuraib **bi dhaalika** (kufunga),kuwa madamu kushafika hapa kwetu .utafunga.Hapana kula !,kwa sababu sisi bado tuko kwenye funga

Mie vitabu vingi sina,lakini aya za Qur'an hizo na hadithi hii.Zikiniishia *point* zangu .bwana kadhi nitakwambia hata ikiwa dakika zangu ishirini hazijesha

Kwa hivyo hadithi ndizo hizo jamani.Tuzisome,zituingie mwilini na akilini tukiondoka hapa kila mtu ajue lake.Kwa hoja hii ya kufunga, mie nataka nifike hapa,na watu wafahamu vizuri wasijeondoka vibaya.Wafahamu ya kuwa kufunga kila mtu ana matlai ya .!kutoka kwake.Ukihudhuria mwezi kwetu tufungeni

.*Wassalaam alaykum warahmatu Llaah*

HOJA ZA ANSAAR SUNNA.
.SKH SAID

Bis*millahir Rahmaanir Rahiim*.Mimi jina langu ni Said,mzaliwa wa mji huu wa Kengeja .na kwa sasa naishi Unguja
Kwa hakika nitajitahidi kutoa hoja kutokana na wazungumzaji mbali mbali.Kwa hivyo .inawezekana nikashika hoja ya huyu halafu nikaruka kidogo kwa hoja ya huyu
Mchangiaji wa mwanzo kabisa alizungumza kuhusu kufunga siku 31.Alidai kuwa Ibnu Abbas alimruhusu Kuraib kufunga siku 31 alipowasili pale Madina.Hii kwanza ni kwenda kinyume na mafundisho ya bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam .Kwa sababu bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema siku katika mafundisho ya uislamu .ni 29 mpaka 30
Ipo hadithi ya bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam inayosema ***Ani Ibnu Umar radhiallaahu anhuma****a]* Kutokana na hadithi ya Ibnu Umar radhi za Mwenyezi Mungu ziwafikie.***Qaala rasuulu Llaahi swalla Llaahu alayhi wa sallam]*** Mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehema na amani zimwendee kasema.***Inna ummatuna ummiyat laa naktub walaa nahsub]*** Hakika umma wetu ni umma ambao aghlabu yetu hatuandiki wala hatuhesabu.Yaani wengi wetu hatukujifundisha kuandika wala kuhesabu.***As-shaharu hakadhaa wa hakadhaa/*** Mwezi unakuwa hivi na mara nyengine unakuwa hivi.***Yaaniy maratan tisan wa ishuruun wa maratan thalathuun]*** Yaani mara nyengine huandama .siku 29 na mara nyengine huandama thalathini.Hadithi hii ameipokea Bukhari
Hapa Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam anatuthibitishia kuwa mwezi ni siku 29 au 30.Na ikiwa tutakubali kuwa Ibnu Abbas alimfungisha au alimruhusu Kuraib kufunga siku 31 basi itakuwa yeye kaenda kinyume na hadithi ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kwa kumfungisha siku ya sikukuu kama ilivyokuja katika hadithi ambapo Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kasema;***Ani Abi Said Alkhudhuriy qaala anna Nnabiy swallaLlaahu alayhi wa sallam nahaa ani swiyaamain]*** Kwamba hakika Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam amekataza kufunga katika siku mbili. ***Swiyaami yawmal adh-.haa wa swiyaamil fitri/*** Kufunga katika idi mbili.idul adh-haa na siku ya idul fitri

Kadhi akamtaka ataje ushahidi wa kitabu hadithi hiyo inapopatikana.Skh Said akasema ni kutoka ***FATHUL BARRI****,hata hivyo akasema ukurasa alikuwa ameghafilika nao,lakini :ni hadithi mashuhuri dondoo yake angetoa baadae,halafu akaendelea*

Pia katika hadithi ya Kuraib pametajwa ***aakhir shahar***,ya kuwa Kuraib alifika katika mji wa Madina katika mwisho wa mwezi.Sasa mwisho wa mwezi hapa tumethibitishiwa na wenzetu upande wa pili ya kuwa ilikuwa ni mwezi 30.Wapi wameipata; haikutajwa.Ila sisi .tunasema ikitajwa *aakhir shahar* kuna uwezekano wa namna mbali mbali
Kwa hadithi ya bwana Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam, aakhir shahar pana uwezekano kuwa ni mwezi 21,22,23 mpaka 29 au 30.Hadith mashuhuri ambayo mafhum yake inasema kuhusiana na mwezi wa Ramadhani kwamba ***awwaluh rahma,awsattuh maghfira wa aakhiruh itqun mina nnaar/*** Mwanzo wake ni rehma,katikati yake ni .maghufira na mwisho wake ni kuepushwa kutokana na moto

Hapo hadithi ya Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam inatubainishia wazi kuwa hata mwezi 21 au 22 za kumi la mwisho ni *aakhir shahar,*na wala hakuna maelezo yaliyokuja .kwa uwazi kusema kuwa aakhir shahar ni tarehe gani

Mwenyekiti,sheikh kadhi wa Mkoani akamuonya skh Said kuwa hadithi anazozitaja awe akizitolea ushahidi wa vitabu.Mwenyewe akajitetea kuwa wao walitaraji kuwa hadithi hizo ni mashuhuri kwa hivyo hawakujitayarisha kwa hilo.Hata hivyo akaahidi kutolea madondoo mwishoni,na akaendelea

Sasa nakuja kwenye suala la matlai.Mzungumzaji mmoja alisema lipo suala la matlai.Sisi na Saudia ni matlai mbali mbali,hivyo ikiwa sisi tutawafuata Saudi Arabia basi tutakuwa ni matlai tofauti.Iwapo tutafuata Tanzania yetu ndiyo itakuwa matlai yetu ni moja sawa .sawa.Yaani nchi yenye hakimu mmmoja
Kuhusu suala hilo tunasema,ikiwa tutafuata hoja ya matlai, basi tutazusha migogoro mingi katika jamii ya kiislamu.Kwanza kabisa ni tukio la kuhama Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam kutoka Makka kwenda Madina.Chanzo hasa cha tarehe ya hijria kinajulikana.Iwapo tutaanza kufuata matlai itakuwa tunaparaganya ile tarehe hasa .iliyoanzishwa katika hukumu ya kiislamu
Nitatoa mfano,mathalan iwe katika nchi ile ambayo ina matlai tafauti na sisi.Iwe kwao leo ni Jumatatu mwezi mosi Muharram mwaka 1425.Halafu iwe kwetu siku ile ile ni Jumapili mwezi 29 au30 Dhul Hijja.Kwa hivyo itakuwa wale wenzetu wameshaingia .mwezi mwengine na mwaka mwengine.Sisi itakuwa tuko nyuma siku moja ama siku mbili Ikiwa leo mathalan atazaliwa mtoto,hatuwezi kuainisha mtoto yule kazaliwa tarehe gani.Kwa hivyo huu ni moja ya migogoro ambayo inatokea.Halkadhalika kama tulivyosema ya kuwa mwezi una siku 29 au 30.Ikiwa tutakubali suala la matlai,basi kama tunavyoambiwa kuwa sisi tunafungua kwa siku 28,basi na wao tunaweza tukawaambia .kuwa wanafunga mpaka mwezi 1 au mwezi 2
Hii ina maana kuwa iwapo tutaendelea kuzusha habari ya matlai basi tutakuwa na Ramadhani zaidi ya moja na tarehe zitakuwa zinakwenda mpaka zaidi ya tarehe 30 ambacho ndicho kikomo cha mwezi,mambo ambayo hayakubaliki katika hukumu za .kiislamu
:Katika kuuelezea mwezi mtukufu wa Ramadhani Mwenyezi Mungu kasema
Hakika sisi tumeiteremsha (Qur'an) katika Laylatul Qadri (Usiku wenye cheo .kitukufu).97:1
Yaani usiku mmoja katika mwezi wa Ramadhani Mwenyezi Mungu kauchagua kuwa ni mtukufu na ndiwo ulioteremshwa Qur'an.Katika moja ya hadithi za Mtume (s.a.w) kaeleza ya kuwa usiku huu uko katika siku yoyote ya Ramadhani lakini hasa hasa katika kumi la .mwisho na tarehe moja wapo kati ya 21,23,25,27 na 29
Tujaalie Ramadhani ya mwaka huu Mwenyezi Mungu kahukumu Lailatul qadri itokee mwezi 29.Sasa jee siku hiyo itakuwa ni ya kule Saudia au ya hapa kwetu?.Labda tukubaliane kuwa ipo hadithi nyengine isemayo kuwa Lailatul qadri inaweza kutokea pia mwezi mwezi 16 au 28.Vyenginevyo tukubaliane kuwa Lailatul qadri huingia upande .mmoja tu wa dunia na upande mwengine huikosa
Vile vile mzungumzaji mmoja alizungumzia suala la swala ya Ijumaa.Ingawa .mwenzangu aliijibu hoja hiyo,lakini na mimi naomba niitolee ufafanuzi zaidi

Tunasoma katika Qur'an;***Enyi mlioamini! Ikiadhiniwa sala siku ya Ijumaa ,nendeni upesi kwenye dhikri ya Mwenyezi Mungu ,na wacheni biashara .Hayo ni bora kwenu lau kama mnajua.(62:9).***Akauliza kwani sisi tunaswali swala ya Ijumaa kwa wakati mmoja?.Na sisi tunamuuliza jee katika hii Tanzania tunaswali swala ya Ijumaa kwa wakati .?mmoja

Sisi na Kigoma kama tulivyoambiwa kuwa ni wenye hakimu mmoja. Tunaswali swala hii kwa tafauti ya saa nzima.Sisi hapa tunaswali kabla yao kwa saa nzima,au baada ya saa 1 ndipo na wao huswali.Kwa hivyo suala hili haliafikiani na hadithi.Tofauti ya saa ni tofauti na tofauti ya siku.Siku ni moja ya Ijumaa lakini inatafautiana kwa masaa.Hii inakubalika,na .Qur'an imethibitisha hayo

Pamezungumzwa kuwa mwaka huu mwezi ulionekana mwanzo Uturuki na wasaudi hawakufunga.Sisi hatuna taarifa hiyo.Tunamuuliza yule muhadhiri atupe ushahidi wapi yeye aliipata taarifa hiyo kuwa Uturuki ndio waliouona mwanzo mwezi..Hata kama waliuona sisi hatukupata taarifa,lau kama tungepata taarifa basi tungefungua au kama ni .!mwezi wa Ramadhani basi tungefunga

Kwa sababu njia zilizotajwa ni mbili tu;ama kuuona mwezi au kusikia taarifa za mwezi. Haiwezekani watu wote ulimwenguni wauone mwezi,kama ni habari wala haiwezekani kuwa Wasaudi wote wapate habari.Lakini wale watakaopata habari wanaingia kwenye .jukumu hili

Katika wahadhiri,mmoja alizungumza kuwa hizi hoja zetu ni za kitoto na kwamba hawa watoto wa leo wanaleta hoja ambazo wazee wetu hawakuzifuata.Lakini hapakubainishwa utoto wenyewe ni upi hasa.Kwa sababu ingawa ni hoja zinazotolewa na sisi watoto,lakini hoja zetu tumezitoa kwenye vitabu hivyo hapo;vya watunzi wenye kutumainiwa.Kwa .hivyo iwapo ni kutolewa maanani basi wangetolewa hao walioviandika badala yetu sisi Iwapo huu ni utoto kwa vile ni mambo yaliyotokezea tu ambayo siku za nyuma watu hawakuyazoea.Nitaleta hoja ambayo huenda iko nje kidogo ya maudhui yetu.Hapa Unguja na Pemba kwa miaka isiyopungua elfu moja,tunajuwa kuwa ndugu zetu wa ki ibadhi walikuwa hawaswali swala za Ijumaa.Lakini ulipokuja ubainifu juu yao sasa wanaswali swala hizo.Tunauliza jee ndugu zetu hawa nao wameleta jambo la kitoto?.Kwa sababu hili ni jambo ambalo kwa muda wa miaka 1000 hatukulizoea.Wazee wetu wengine sisi, mpaka .wamekufa hawakuiswalipo swala ya Ijumaa

:Sheikh Said akachukua umbo duara la dunia halafu akaendelea

Kuhusu suala la wakati pametajwa kuwa sisi na Makka na Madina bila ya hoja ni kwamba tuko tofauti.Sisi tunasema kisayansi sisi na Makka na Madina tuna wakati mmoja.Sayansi si ya wazungu bwana!,ni katika asaasa za Mwenyezi Mungu.Allah(s.w) ndiye aliyeiumba .na ndiye anayeisimamia

Tukitaka kujua,wale ndugu zetu wa Jiografia wanatufahamisha kuwa sisi Unguja na Pemba ukichora mstari wa l*ongitude* unaotoka juu mpaka chini utaona zinaangukia kwenye longitude moja na Makka na Madina.Madamu ziko kwenye longitude moja basi muda wao unakuwa ni mmoja .Ukienda mashariki muda unaongezeka na ukienda .magharibi muda unapungua

Katika Tanzania yetu hii hii tuna mapishano ya takriban saa nzima baina ya Dar salaam na Kigoma.Na kwa hapa Zanzibar;Unguja na Pemba wakati wetu ni mmoja na Saudia.Ushahidi ni kwamba wale wanaosikiliza redio ya Jeddah kwa lugha ya Kiswahili ambayo hutoa matangazo yake kila siku kuanzia saa 2 kamili asubuhi mpaka saa tatu

kasoro dakika 10.Kila mara wanapofungua husema saa zetu hapa ni sawa na za huko .kwenu Afrika Mashariki
Hivi karibuni katika redio hiyo walitoa swali wakauliza;Eleza tafauti iliyopo baina ya time za GMT za Saudia na London na Saudia na huko kwenu Afrika Mashariki.Baadae suali hilo likajibiwa kuwa sisi Saudia,Makka, Madina na Jeddah hatuna tafauti ya hata .dakika moja na nchi ya Zanzibar;Unguja na Pemba
Mwenyekiti,kadhi wa wilaya ya Mkoani akamkumbusha mzungumzaji skh Said ya kuwa .muda wake umebakia dakika mbili tu.Bila kujibu mzungumzaji akaendelea na mada yake
Na pia mzungumzaji mmoja alizungumzia suala la mipaka,kuwa sisi Tanzania tuna mipaka yetu.Yaani imetajwa ki nchi.Sasa hapa twataka tuthibitishe kuwa sisi waislamu hatuhusiki na hii mipaka iliyopangwa na wazungu katika mwaka 1884 walipofanya ile .*Berlin conference;*walipojihalalishia ukoloni katika kinyang'anyiro cha Afrika
Wasomi wa historia watakumbuka kuwa wazungu ndio waliozigawa nchi na kusema hii iwe Uganda, hii iwe Kenya na kadhalika.Leo hii sisi waislamu tumekuwa tunafuata vile .!vile walivyogawa wazungu.Uislamu hautambui mipaka ya wazungu jamani
Tunauliza swali,leo Namanga ya Tanzania wakiuona mwezi jee waislamu wa Namanga ya Kenya wasifunge?,ati kwa sababu tu kule wana hakimu wao mwengine na huku tuna hakimu mwengine.Lau kama wazungu wangeigawa Tanzania kuwa ni nchi moja au ingekuwa Afrika yote ni nchi moja ,jee bado tungekubali habari ya matlai?.Kwa hivyo .haya ni mambo yanayoleta migogoro, pindi tu tunapoleta suala la matlai na mipaka
Katika ushahidi wa aya,palizungumzwa sana katika kufafanua aya isemayo ***Faman shahida minkumus-shahara***. Mzunngumzaji akasisistiza sana kuwa tufunge watu wa nchi ya hapa na si nchi ya huko.Mimi si mtaalamu sana wa kufafanua nahau namna hii,lakini tunamuuliza ni nahau,mantiq au lugha gani hiyo isemayo kuwa *minkum* hii ni nchi ya hapa .?na si nchi ya huko
Mwisho kabisa namalizia na suala la Kuraib.Hapa imetajwa kuwa huyu Kuraib alikwenda Madina kwa ajili ya kutembea.Hii ni hali ya kubabaisha na hapa tumekuja kuzungumzia hoja za kisomi.Sisi tunasema Kuraib hakwenda Madina kwa lengo la kutembea bali alirudi nyumbani, kwa sababu yeye alikuwa akiishi Madina na alikuwa ni mtumishi wa Ibnu .Abbas
.Mpaka hapa *assalaam alaykum warahmatullaah wabarakat-hu*

.HOJA ZA BAKWATA
SKH ALAWY OMAR SALIM.
Assalaam alaykum warahmatullaah.Jina langu ni Alawy bin Omar bin Salim kutoka .Kanambe-Ole
Elimu yangu ya dini niliipata nilipokuwa mdogo kwa marehemu baba yangu, sayyid Omar bin Salim.Hakuchukua muda alifariki,na mimi nikaendelea kupata mafunzo hayo ya dini kwa wanafunzi wake.Wamojawapo ni akina skh Ahmad bin Ali,skh Ali bin Kombo,na .kutoka kwa skh Jabir bin Hamad.Wote ni masheikh maarufu Ole
Baada ya hapo katika hali ya kuwa baba yangu na mama yangu walikwisha kufa,Mwenyezi Mungu akanipa ilhamu na uwezo mpaka nikaweza kusafiri kwa nafakha yangu mwenyewe kwenda Hadhramaut nchini Yemen kwenye chuo cha skh Abdallah bin Omary Shaafiy na skh Muhammad bin Omar Shaafiy.Hawa ni mabwana mashuhuri walioandika ***Alyaquutin Nafiis***,nuskha zake tunazo nyingi sana hapa nchini kwetu Pemba .na hata na Unguja

Kwenye chuo hicho niliweza kudumu kwa muda wa miaka mitano.Walimu wangu walikuwa ni sheikh Salim bin Muhammad bin Saleh,sheikh Mahfudh Bukhery na sheikh Said bin Salim Bukhery.Pia nilipata mafunzo kutoka kwa sayyid Ahmed wa .Unguja.Wakati skh Said bin Slim alikwishafika kutoka huko,si chini ya miaka 10 Niliporudi kutoka masomoni nikawa niko nyumbani.Nikaendelea na mafunzo yangu ya dini bila kukata,pale pale nilipoanza kwa sheikh aliyebakia wakati huo,ambaye ni sheikh Ahmad bina Ali mpaka kufa kwake.Baada ya hapo nikaendelea na kutafuta elimu .kwengineko,wakati huo huo nikafanya na kazi ya ufundishaji kama wenzetu Sasa;tukiingia katika shughuli yetu hii iliyotuleta hapa,ni kuwa mengi yameshazungumzwa,lakini tumeona kuwa yote yanarudia kwenye meza ya hadithi na Qur'an pamoja na fatwa za wanawachuoni.Kuyatolea tena fatwa hapa sio pahala pake .kabisa,na sio fursa kufanya hivyo.Isipokuwa tu,kuna tatizo la hadithi kidogo Hadithi ni jambo lenye kumahanika na kurefuka sana.Tatizo jengine la hadithi ni katika uaminifu.Inaweza kuwa mtu anayeniletea hadithi ikawa ni mtu ninayemuamini,nikaichukua hadithi ile nikaitumia kwenye fatwa zangu.Au ikawa mtu yule mimi simuamini na nikaidhoofisha hadithi yake.Lakini akatokezea mtu anayemuamini yeye, ambaye akaitumia hadithi ile kwenye mambo yake na akaiweka kwenye maandishi yake.Pia inatokea anayeletewa hadithi ikawa haijamuathiri akaidhoofisha,akakataa kuiamini na kuitumia.Tunaweza kutoa matatizo mengi ya hadithi lakini mimi sitaki .kuendelea sana kwenye suala hili,kwanza nasema si fani yangu

Muhadhiri mmoja alisoma aya ya Qur'an inayohusu kuandama mwezi,isemayo: ***Faman shahida minkumush-Shahra fal-yasumh.(2:185)***.Hii ni sawa kabisa.Kwa alivyoitumia yeye muhadhiri,kasema kuwa shahida si kwa maana ya kuona ina maana ya ***hadhwara*****.**Na akasema *hadhwara* ikiwa *mudhwaariu* inakuwa na maana ya *ishraari*.Ni sawa kabisa.Yaani ikitokana na mwanaadamu ***Ash-hadu an laailaaha illa Llaah*** inakuwa ni *ishraari,*lakini kasema Mwenyezi Mungu ***Shahida Llaahu annahu Laa ilaaha illa .huwa*****.**Hii kwake haikuwa na maana ya ishraari.Ilikuwa na maana tafauti kabisa

Hayo ni matumizi ya kilugha.Ni jambo la kawaida mtu kumtazama msemaji wa hapa, ni nani?.Sasa kama italingana kwa kumtazama ni nani msemaji,au kwa kutazama tafsiri ya .msemaji na mwendo wa maneno yake

Kwenye aya hiyo hiyo ***ya (2:185***), mhadhiri wa mwanzo kasema mwezi mchanga hauitwi ***shahar*****.**Ni kweli mwezi mchanga hauitwi shahar.Hii nitamjibu kwa jawabu mbili.Maana moja ya shahar ni ya kuazima, mfano inaposemwa *Liyash-har bih minal warai*;Hii nayo ni **.shahar**,kwa vile jambo kuwa limezagaa kwa watu ndipo ikapata jina lake **shahar** Mwezi mchanga unaitwa **hilaal** kama iliposemwa ***man stahala***.Kwa kusema tu kuwa mwezi umeonekanika ndipo ukapewa jina lake.Kwa hivyo majina yote mawili yanatumika kwa maana ya mwezi mchanga.Alisema kuwa mwezi vile vile unaitwa **Qamar**.Ni kweli mwezi unaitwa **qamar**,lakini hauwezi kuitwa hivyo isipokuwa kwa kukamilika lile duara **.**lake kuanzia mwezi 8 na kuendelea.Hapo ndio kweli unaitwa **qamar**

Hadithi aliyotoa muhadhir kuwa,huwa tunafunga Ramadhani kwa sababu ya ***ru'iya*****.**Lakini aliacha kitu,pale Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam aliposema ***Fain ghumma alaykum Fa akmiluu idda Shaabana thalathiin] Na kama kikija kiwingu juu yenu kikauficha mwezi.Kamilisheni hesabu ya Shaabani siku thalathini***.Hili lakini .limeshazungumzwa.Hii ni kusema hivyo ndivyo ilivyo

Nafikiri sana kuwa iliposemwa ***Fain*** *ghumma* ***alaykum*** basi hii *ttabaan* ilikuwa na maana ya pale mwezi ulipoonekanika au pale pahala ulipotafutwa.Kwa sababu hakuwezi kuwa na

mawingu ulimwengu mzima.Ikiwa kwetu kuna mawingu basi kwa wenzetu kuko safi.Ndipo Mtume swalla llaahu alayhi wa ssallaam akasema ***Fain ghumma alaykum*** ..Ikiwa watu hawakuuona mwezi timizeni siku 30 za Shaaban

Jamani tufahamu kitu kimoja,kuwa ulimwengu ni ulimwengu ,na ulimwengu una binaadamu.Binaadamu tunatakiwa kumuabudu Mwenyezi Mungu.Ili kuadhimisha ibada kwa Mwenyezi Mungu kila dakika tumetafautishwa.Kama ulivyotafautishwa ulimwengu, .na nyakati za ibada nazo zimetafautishwa.Hii ni hekima yake Mwenyezi Mungu

Jee adhuhuri itakapoingia Saudi Arabia au Masri au Maskat au wapi..,kweli sisi tutatakiwa kuswali adhuhuri ile.Au sisi twatakiwa kufanya ibada moja tu ya kufunga?.Isitoshe,ibada ni jambo lenye mipaka, nyuma na usoni,hususan ibada ya funga ya Ramadhani.Huwezi kufunga Ramadhani mwezi wa Shaaban au mfunguo pili au mfunguo .tatu.Ni lazima ifike ndipo ufunge

Ramadhani nayo ina mwanzo na mwisho.Hapa katikati yake kuna mambo ya *mubaha* na *mahrumaat*.Tumeambiwa ukionekana mwezi Saudi Arabia au nchi yoyote ulimwenguni,sisi hapa Zanzibar na Afrika mashariki tufunge pia.Tunauliza jee wakati wa .?kufuturu na kujizuia kula na mengineyo kuanzia alfajiri nako tutafuata nchi hizo

Iwapo tutafuata nchi hizo kwa uhalali wa kuanza kula na uharamu wa kujizuia, kwanini Mwenyezi Mungu hakutukalifisha kutafuta habari zao kwanza ?.Naomba kujibiwa maswali .yangu hayo

Tuanapozungumzia *mattaali'i* au ibada ni lazima tujuwe kuwa kuna masharti.Hakuwezi kuwepo ibada nje ya sharti.Ibada zina *arkaani,* ibada zina masharti na suna zake.Ibada vile vile zina *makruhaat* na ina *maf'ulaat* .Lazima ujue *makaruhaat* za ibada na vivunjo vyake.Yaani huwezi kufanya mambo fulani wakati ukitekeleza ibada hiyo.Hiyo ndiyo .ibada,haiwezi kuwa ibada ovyo tu,ni lazima izungukwe na vitu hivyo ndipo iwe ni ibada

Hapa imezungumzwa sana habari ya kuandama mwezi wapi na wapi huko.*Mattaali'i* sikumbuki imezungumzwa wapi na vipi.Lakini jee ni kweli ibada hii haina masharti ,iwe ikishapatikana habari kuwa mwezi umeandama pahala fulani iwe ndio basi !.Twasema ibada ya funga ilivyokuwa ni ibada,inamuhusu au inamuwajibikia mtu kuitekeleza kwa .kupatikana sharti zake na kuingia wakati wake kwa pale mtu alipo tu

Ikiwa mimi niko hapa, sasa hivi ni Alasiri,basi Maskati ni magharib.Mimi hata nikifa sasa hivi sitoulizwa kwa kutoisali magharibi iliyoingia Maskati.Ikiwa hivyo ndivyo ilivyo .?itaniwajibikiaje sala hiyo

Muhadhiri hapa alizungumzia habari ya saa za zoni.Kwenye ibada tunatumia saa za .jua.Saa za zoni ni saa za kubahatisha,ni saa za kazi tu,hazitufai sisi katika ibada zetu

Muhadhiri huyo huyo aliyenitangulia kataka tujibu maswali yake,ingawa yeye hakujibu hata hoja moja ya mwenzetu aliyetangulia.Kasema ikiwa tutafuata *mattaali'i* italazimisha *kuta-adadi* Ramadhani,yaani Ramadhani zitakuwa nyingi,kila watu watakuwa na .Ramadhani zao

Mimi si mtaalamu sana lakini mwenzetu huyu kasahau kuwa katika ulimwengu wetu huu kuna nchi zina tafauti baina ya usiku na mchana.Ikiwa si tafauti ya usiku mzima au mchana mzima, basi angalau nusu usiku au nusu mchana.Hii ni mfano baina yetu na watu .wa Marekani

Kwa mujibu wa uislamu ulivyo ***ttabaan*** waislamu wako Marekani.Wako wenye kufunga huko.Sasa jee wao wana Ramadhani nyengine wanayofunga na swala zao?.Au ni Ramadhani na swala zetu hizi hizi?.Ikiwa Ramadhani *ita taadadi,* kwani Lailatul qadri

watakuwa na yao?,si itakuwa ni hii hii yetu!.Lakini ni kwamba ibada mtu hutekeleza kwa .mujibu wa pale alipo mwenyewe

Kwa kusema hivyo tuangalie mfano wa **zakatulfitri**.**T**wajua kuwa zaka hii ni wajibu mtu kuitekeleza pale lilipomtulia Jua.Na haitoshi pale lilipomtulia jua tu,bali pale mtu anapokaa.Sio kuwa limenitulia Kengeja nitoe kwa Kengeja yote.Wajibu ni kwa pale .ninapokaa

Mwenzetu alipokuwa akitolea ushahidi kwenye **Ibnu Kathii**r,katumia neno ***Muqiim*** **.**Akataja na habari ya **maarifah** na **naakira,**kwamba ikija *naakira* basi inawahusu watu wote,sio watu maalum.Kama sijasahau ni kuwa **ismu** yoyote iliyokuwa *naakira* ikija kwa mara ya pili kwa *maarifah* basi huwa ni ile ile,si nyengine.Hapo hakuna *kuta .adad*,inakuwa ni ile ile

Mwenyezi Mungu kasema:….. ***Kamaa 'arsalnaa ilaa Fir-'awna Rasuulaa [Kama tulivyompeleka Mtume kwa Firauni]-73:15.*** Kwenye aya inayoifuatia akasema **.**tena:***Fa-'asaa Fir-'awnur-Rasuula [Lakini Firauni alimuasi huyo Mtume]-73:16***

Hatuwezi kusema kuwa Firauni alipelekewa Mtume mwengine halafu akamuasi Mtume mwengine.Mtume ni huyo huyo Musa (a.s).*Maarifah* ikirudi kwenda naakira hupelekea *kuta adad* isipokuwa sehemu moja tu ndani ya Qur'an, pale Mwenyezi Mungu anaposema ***Fiy samawaat*** au ***ilaa Fil- ardh.*** Hizo ni ***muqarabina bi taadad***.Hatuwezi kupata au .kufuata maana ya kilugha ilivyo au kawaida ya kinahau ilivyo

Kwa sababu tukifanya hivyo au tukifuata hivyo itasababisha kubatilisha misingi ya Qur'an,na sivyo ilivyo.Itapelekea mambo mengine kabisa.Hukuna mbingu ya Mungu mwengine na ardhi ya Mungu mwengine.Hii ni mifano ambayo si ghalibu kutokea,kwa hivyo hunyamaziwa na wanawazuoni.Ni ***maafuwan***

Mwenyekiti akamkumbusha sheikh Alawy kuwa amebakiwa na dakika nne tu.Akaitikia hewallah,halafu akaendelea

.

Sasa jambo lililobaki, ni kushikamana na vitabu vya kale.Ikiwa ni kweli tunashikamana na madhehebi ya Shaafi,basi ni wajibu wetu kushikamana na vitabu vya Shaafiy au as-haabu Shaafi-iya.Haidhuru wakati mwengine kwaweza kuwepo kauli ya Shaafiy mwenyewe lakini as-haabu Shaafi-iya wakawa wanaipinga ,au wenyewe as haabu Shaafi-.iya wakawa wanachukizana

Muhimu ni kuwa ipo misingi ya kifiqhi. Wakitokezea masheikh wawili wakapingana katika kuswihi kwa ibada,mmoja ataka ibada hii isifanyike kwa aibu kadhaa,kadhaa.Mwengine ataka ibada hii itekelezwe kwa dharura kadha na kadha.Katika .hali kama hii anayefuatwa ni yule mwepesi ili ibada ile ipate kutekelezwa

Ushahidi upo katika utoaji wetu wa zaka.Kwa mujibu wa mdhehebi ya Shaafiy,hapa hakuna mtu wa kupewa zaka.Lakini jee ndiyo tusitoe zaka,Tutamjibu nini Mwenyezi .Mungu wakati yapo madhehebi mengine yenye kujuzisha kutoa zaka

Kwa upande wa madhehebi ya Imami Shaafiy haijuzu kuswali swala ya Ijumaa hapa.Idadi kwa upande wake ina matatizo.Ukifuata mulimotajwa habari hizo utapata kauli zaidi ya 15.Kwanini tusifanye takalid tukawafuata as-haabu Shaafi-iya wanaojuzisha kuswihi kwa .?ibada hiyo

Ibnu Hajar na imamu Ramli wana tafauti kuhusu mtoto aliyekufa na hakuwahi kuhitaniwa.Ibnu Hajar ataka mtoto huyo azikwe bila kiswaliwa kwa vile swala haiswihi mpaka kwa kuondoka najis,na huyu hatupati kumuondosha najisi yote Ndipo pale

tuliposema sharti iko nje ya ibada, lakini matatizo yake yazuia kuswihi kwa ibada. Lakini sisi hatufanyi hivyo, ni kwanini?,Ni kwa sababu ya kufuata aliye mwepesi,na wote hao ni ..as-haabu Shaafi-iya

Namalizia na kuhusu kufunga.Wenzetu wametaja mengi,juu ya kuandama mwezi huku na kule, na kufunga siku ya sikukuu kuwa ni haramu.Tujue anayefunga siku hiyo kwake si Idi .,huwa ni kufunga kwa kawaida tu

Hiki nilichonacho mkononi ni kitabu cha sherh ya ***SAFINATUN NAJAA***,kinaitwa **KASHFATU SAJAA**.ukurasa wa 116.Kasema;***Idhaa ru'iya l hilaal bi mahalin laazima hukmuh mahalan qaariban minhu [Utakapoonekanika mwezi pahali,italazimu hukmu .[ya kuonekanika huko pahali palipo karibu na hapo***

Wa yudhkar qurbuh;[Hupatikana ukaribu huo].Bi itihaadil mattla'i;[Kwa kuwa makazi yao ni mamoja].An yakuuna ghuruubi shamsi wal kawkab wa ttuluu'ihaa fiy baladain bi waqtin waahida; [Kama kwamba utuaji wa jua na mwezi,utuaji wa nyota [na utokaji wao katika nchi mbili hizo ni wakati mmoja

Haadhaa in-da ulaamai falaq;[Hawa ni watu wa elimu ya jiografi,yaani wajuzi wa mambo ya nyota].Wa ladhiy in-da fuqahaau;[Na kwa yale waliyonayo watu wa fiqh].An laa takuuna maa bainahumaa bi 24 farsakhan;[Masafa baina ya miji miwili hiyo yasije yakazidi masafa ya farsakh 24].Min ayyi jihat kaamil;[Kwa pande zote .[unapotokea

Kwa pande zote za ulimwengu unapotokea.Unapotulia mpaka pale,kaskazini mpaka pale, na unapotokea mpaka pale,na upande wa magharibi ni mpaka pale.***Wa a'alam anna mattilaa ihil ulaa fiy baladi sharqiy;[Elewa kuwa mwezi unapoonekanika jua linapotokea upande wa mashariki].Laazima hukmuh fiy baladi gharbiy,duuna aqsi; [Hulazimika uono wake kwenye mji ulio magharibi yake,na wala si vyenginevyo].Y***aani .ukionekanika magharibi haifiki hukmu yake Afrika mashariki

Sasa yaja masuala mengine.***Walaw saafara muswaam;[Lau kwamba atasafiri mtu aliyefunga].Ilaa mahali baiidin min mahali ru'yatih;[Kwenda pahali palipo mbali na pale alipouona kwa mara ya mwanzo].Wafaqa ahluh bi swaumil aakhir;[Atawaafiki watu wa pahala hapo kwa saumu].Walaw iida qabla safarih;[Hata kama alikula idi kabla ya safari yake hiyo.].Thumma adrakahu swaaimiina fa amsaka ma'ahu;[Halafu [akawakuta wale aliowaendea bado wanafunga,atajizuia pamoja nao***

Yeye anakuwa hana kufunga tena.Wakati yeye ni muislamu ashike adabu,watu waliopo hapo kwao ni Ramadhani.Inabidi awe pamoja nao.***Wain taama thalathiina;[Japo kuwa .yeye kashatimiza siku thalathini].***Anakuwa yeye na wao ni hukumu moja

Aw saafara ilaa mahali baiidin rui'yat ih;[Au ikiwa atasafiri kwenda pahali pa mbali ambapo umeonekanika mwezi wa mfunguo mosi].Iida ma'ahu;[Atakula idi pamoja .[nao

Hapa hatusemi kuwa amekula siku ya Idi,isipokuwa amekula Idi kwa ruhusa ya kuwa ni sikukuu kwa kuchanganyika na watu wa pale,na yeye atahukumiwa kwa hukumu ya watu .aliochanganyika nao.Hii yote ni kusema kuwa Ibada mtu yamuhusu kwa pahala alipo

Inaendelea kusema ***;Wa qadhaa yawman in swaama 28 yawman;[Na atalipa siku moja ikiwa atakuwa amefunga siku 28].Wa in swaama 29 laa qadhaa lahu;[Ikiwa .[alikuwa amefunga siku 29 hatalipa tena***

Haadhal hukmu laa yakhtasw bi swaumi faqat; [***Hukumu hii haihusu kufunga pekee].Hataa law swalla l maghrib wa saafara ilaa aakhir;[Hata akiwa amesali***

magharibi na akasafiri kwenda mji mwengine].Fa wajada lam taghrub wajaba bil [iaada;[Akakuta kule magharibi bado haijaingia,Itamlazimu arudishe ,aswali tena
Hiyo yote inatia mkazo kuwa ibada mtu inamuhusu pale alipo.Hao ni masheikh .waliokuwa wametia umuhimu wa Qur'an na hadithi.Wanachukua *qiyaas* na *ijma-inh* Hakuna kitabu chochote duniani amabacho kimetungwa kwa rai za mtu mmoja pekee.Mtungaji wa **BAFADHILI** alipomaliza aliipeleka Makka,akarejeshewa akaambiwa haisomeki,akaipitia tena akaipeleka Madina.Mwenzetu alipokuwa akijibu suali hili aikuwa .hana *Isnadi* nalo,ilikuwa tunakwenda na rai zake tu

Kufikia hapo mwenyekiti wa semina akamkatiza skh Alawy kuendelea kwa vile dakika tano za nyongeza zilikuwa zimekwisha.Naye akamalizia kwa kusema

.Kwa hivyo nashukuru,asante sana **Wa jazaakumu Llaah khair**

.Baada ya hapo ukumbi ukachawanyika kwa ajili ya swala ya Alasiri
Waliporudi mada ya mjadala wa mwezi ikafungwa kwa hoja za mchangiaji wa mwisho kutoka upande wa Ansaar Sunna;skh Kombo Bakar Kombo wa kutoka mkoa wa kaskazini Unguja ambaye kwa wakati huo alikuwa anaishi mjini Unguja.

- *HOJA ZA ANSAAR SUNNA*
- *SKH. KOMBO BAKAR KOMBO*

Mimi nitachangia hoja kujibu wale wanaohoji kufunga kwa kufuata mwezi unaoonekana popote duniani.
Napenda kuwaeleza masheikh zangu walio mbele yangu na hadhara yote kwa jumla, ya kuwa mpaka sasa hatujapewa hata hoja moja inayoonesha kuwa kufunga kwa kuonekana mwezi popote duniani,kwamba jambo hili ni makosa.
Hoja tunazozipata ni zile zinazosema kuwa vijana wetu musiache msimamo wetu waliouzowea wazee wetu.Kwani ni nani mwenye msimamo kwenye dini ya Mungu.Mwenye msimamo katika dini hii kwanza ni Mwenyezi Mungu mwenyewe.Yeye ndiye aliyemtuma mjumbe wake awafundishe watu namna ya kuisimamisha dini yake.
Kusema 'jambo letu hili' ni makosa,ni lazima utumie hoja kuonesha Mungu na Mtume wake wamesema kadha..kadha.Ndiyo maana Mungu kasema katika Qur'an:
Enyi mlioamini!Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu,walio katika nyie (waislamu wenzenu).Na kama mkikhitilafiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume ,ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho.Hiyo ndiyo kheri,nayo ina matokeo bora kabisa. 4:59
Kwa utaratibu huo tu ndipo suluhisho letu litapatikana.Kwa kusema tunafuata hoja za mababu zetu nataraji waislamu waliohudhuria hapa watakuwa hawakupata kitu cha maana. Jamani !,sisi tumetoa hoja nyingi sana kutoka Qur'an na sunna.Kila anayekuja kuchangia hakuna aliyeweza kupinga kuwa hadithi *kama swuumuu liru'yatih* si ya umuumi.

Hoja nyengine iliyoletwa dhidi yetu ni kuwa mbona nyinyi adhuhuri ikiingia Saudi Arabia au magharibi hamuswali kwa kufuata huko?.Kwa kweli hoja hii naiita ni ya kitoto na si ya kielimu.Kwa sababu katika dini hii kila ibada ina taratibu zake.Kwenye swala Mwenyezi Mungu kasema katika Qur'an 17:78;ya kuwa simamisheni swala kwa kuchenguka jua.

Aliyeko Marekani ataswali adhuhuri kwa kuchenguka jua Marekani,aliyeko Yemen ataswali kwa kuchenguka jua Yemen,aliyeko Saudi Arabia hivyo hivyo na kwengineko.Kuhusu kufuturu na kufunga Mwenyezi Mungu kasema tena kwenye Qur'an 2:187…***Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu weupe wa alfajiri katika weusi wa usiku.Kisha timizeni saumu mpaka usiku….***

Wanachuoni wamefasiri kuwa timizeni saumu mpaka usiku kuwa ni mpaka jua litakapozama..

……

Sehemu ndogo katik hoja za skh .Bakar Kombo imekosekana kutokana na matatizo ya mkanda wa video.Umalizapo kusoma mjadala huu tuma kura yako juu ya nani aliyeshinda kwa hoja kati ya Bakwata na Ansaar Sunna.Kila baada ya muda apendandapo Allah aliyletukuka tutakuwa tukichapisha matokeo.Tuma kura yako kupitia uongofu@islamicalendartides.com